Nipashe
Alhamisi Oktoba 17, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580051
www.ippmedia.com
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## TMA yatahadharisha mvua kubwa kunyesha nchini kote

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wakurugenzi ruksa kusimamia uchaguzi

**MAHAKAMA** ya Rufani yatengua uamuzi wa Mahakama Kuu, kesi ya Bob Wangwe...*Endelea ukurasa wa 2*

**YALIYOMO**

UKURASA WA 4
**SERIKALI YATOA UFAFANUZI HUKUMU MAHAKAMA ICSID**
MAHAKAMA ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro...

UKURASA WA 16 & 17
**MAAJABU MAKUBWA YA MKUNGA ASIYESOMEA**
"SIJAUSOMEA ukunga darasani, lakini nimeokoa maisha ya maelfu...

UKURASA WA 26
**WADAU WAJADILI MFUMO UAGIZAJI MBOLEA PAMOJA**
SERIKALI imeelezea kuridhishwa na mfumo...

## Wawekwa kitimoto mbele ya Magufuli

UKURASA 3




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Sera, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenister Mhagama (kulia), akiwa kwenye bodaboda baada ya kuzindua MastaBoda ambao ni mpango maalum wa Benki ya NMB kwa kushirikiana na Master Card ambao utawawezesha waendesha bodaboda kukopa pikipiki. Wengine ni Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna na Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma Makao Makuu ya Usalama Barabarani, Mrakibu wa Polisi, Abel Swai. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

## Kanda ya Ziwa yataja siri kung'ara matokeo la saba

UKURASA 2

**MICHEZO** FIFA YASHAURI TFF SASA ISUKWE UPYA UK. 32 **MAONI, KATUNI UK.6**

## Mil. 16.9 wajiandikisha uchaguzi wa S/Mitaa

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imesema idadi ya watu waliojiandikisha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa imefikia asilimia 74.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tamisemi, Selemani Jafo, jijini Dodoma jana.

Akizungumzia hali ya uandikishaji, Jafo alisema hadi kufikia juzi, umefikia asilimia 74 ambapo watu milioni 16.9 wamejiandikisha huku Halmashauri ya jiji la Arusha ikiwa chini ya asilimia 50 na kuwataka viongozi wake kujitathmini.

"DC (mkuu wa wilaya), DED (Mkurugenzi wa Halmashauri), msimamizi wa uchaguzi na watendaji wana jambo la kujitathmini kwa kuwa hadi jana (juzi) wana asilimia 37. Pia kwa Manispaa ya Moshi wao wapo juu ya asilimia 50 ambapo wana asilimia 51 wamejitahidi kidogo," alisema.

Alieleza kuwa anaamini Arusha watajipanga vizuri kwa muda uliobaki kufanya hamasa ili idadi iongezeke.

Jafo alisema Mkoa wa Dar es Salaam unashika nafasi ya kwanza kwa kuandikisha kwa asilimia 89, ukifuatiwa na Pwani 86%, Tanga 81%, Mtwara 80% na Lindi 77%.

Hata hivyo, alisema pamoja na kwamba mikoa yote imevuka asilimia 50, lakini mikoa ambayo kasi yake hairidhishi ni Kigoma ambao umeandikisha kwa asilimia 57, Kilimanjaro 58%, Arusha 66%, Shinyanga 66%.

Jafo alisema ofisi yake haijatoa maelekezo yeyote ya kuwanyima huduma za msingi wananchi wasiojiandikisha kwenye orodha ya daftari la wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Kauli hiyo aliitoa baada ya kusambaa kwa 'clip' ikionesha mmoja wa maofisa akiwataka wananchi wajiandikishe kwa kuwa mtu yeyote ambaye hatajiandikisha hatatambulika kwenye huduma zote za msingi.

Jafo alisema kuna watu wanasema watu wanalazimishwa jambo ambalo si kweli na kwamba kanuni zipo wazi hakuna mtu anayelazimishwa.

Wakati leo ni siku ya mwisho kwa wananchi kujiandikisha, baada ya serikali kuongeza siku yatu za ziada, wadau wa masuala ya kidemokrasia wamezungumzia kusuasua kwa watu kujiandikisha ni kukosekana kwa elimu ya kutosha na hofu ya kasoro zilizojitokeza katika chaguzi zilizopita.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga na Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, walisema elimu ya kutosha haikutolewa kabla ya kuanza kwa kazi ya uandikishaji.

Henga alisema serikali ilipaswa kutenga muda wa kutosha wa kutoa elimu kwa jamii, kuhusu umuhimu wa

INAENDELEA UK. 8

# Wakurugenzi ruksa kusimamia uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania, imetengua uamuzi wa kesi iliyofunguliwa na Bob Wangwe katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, uliowazuia wakurugenzi wa halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na jopo la majaji wa Mahakama ya Rufani likiongozwa na Jaji Augustine Mwarija. Wengine katika jopo hilo ni Stella Mugasha, Richard Mziray, Rehema Mkuye na Jacobs Mwambegele.

Kutokana na uamuzi huo, wakurugenzi watendaji wa halmashauri za wilaya, wakurugenzi wa halmashauri za miji, manispaa na majiji kusimamia uchaguzi kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ama ambavyo wamekuwa wakifanya kwa miaka kadhaa iliyopita.

Makahama Kuu katika uamuzi wake, kupitia kesi iliyofunguliwa na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Wangwe, na wanaharakati wa haki za binadamu, ilisema wakurugenzi hao kusimamia uchaguzi ni kinyume cha kifungu Na. 7 cha Sheria ya Uchaguzi.

Uamuzi wa Mahakama Kuu ulitolewa na jopo la majaji Dk. Atuganile Ngwala, Dk. Benhajj Masoud na Firmin Matogolo.

Katika uamuzi wao, walikubaliana na hoja za mawakili wa mlalamikaji huku wakitolea mifano ya baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri ambao walishiriki kura za maoni ndani ya CCM katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Kwa mujibu wa jopo la majaji wa majaji hao, kitendo cha wakurugenzi hao, ambao baadhi yao ni wanachama wa vyama vya siasa, hususan Chama Cha Mapinduzi (CCM), kinaifanya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na uchaguzi mzima kutokuwa huru kwa mujibu wa Katiba.

Jopo hilo la majaji wa Mahakama ya Rufani, katika uamuzi wake, lilikubaliana na madai ya serikali kupitia kwa Wakili wake Mkuu, Dk. Clemet Mashamba,

INAENDELEA UK.8



Mwonekano wa sehemu ya ujenzi unaoendelea wa barabara za mpishano (Ubungo Interchange), katika eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Kanda ya Ziwa yataja siri kung'ara matokeo la saba

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya kutangazwa kwa matokeo ya darasa la saba huku Kanda ya Ziwa ikiongoza kitaifa, wadau mbalimbali wa sekta ya elimu katika kanda hiyo, wamefunguka siri ya mafanikio hayo.

Matokeo hayo yaliyotangazwa juzi na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Taifa, (Necta), Dk. Charles Msonde, yalionyesha mikoa tisa ya kanda hiyo imeingia kumi bora kitaifa na kumtoa mshindi wa jumla ambaye ni Grace Manga kutoka Shule ya Msingi Graiyaki, mkoani Mara.

Mikoa mingine ya kanda hiyo ambayo watahiniwa wake wameingia 10 bora kitaifa ni Geita, Shinyanga na Mwanza.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, wadau hao wakiwamo maofisa elimu, HakiElimu na Mkuu wa Mkoa, walieleza siri ya mafanikio hayo kuwa ni utayari wa walimu kufundisha, chakula kwa wanafunzi na zawadi kwa washindi.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Mohamed Kahundi, alitoa siri ya mafanikio ya mkoa wake kuingia kumi bora katika matokeo hayo kuwa ni juhudi za walimu kufundisha na kujitoa katika kazi.

"Tuliwataka wakati wakifundisha wawe wanatoa mazoezi mengi kwa wanafunzi na wamekuwa wakifanya hivyo. Kila tunapofaulisha kama mkoa tumejiwekea utaratibu wa kutoa zawadi kwa walimu, wanafunzi hivyo hii nayo ni njia nyingine ya kuongeza ufaulu.

"Kama mwaka husika tutashindwa kutoa fedha taslimu kwa walimu na wanafunzi huwa tunawapa barua za shukrani."

Kahundi alitaja njia nyingine ya kuongeza ufaulu mkoani humo kuwa ni chakula kwa wanafunzi ambao wanafanya mitihani ya kitaifa kuanzia wa moko darasa la nne, la saba, kidato cha pili na cha nne.

"Kwa miaka minne mfululizo tumeendelea kuilinda nafasi yetu ya mkoa kwenye mitihani ya taifa, kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2015 tumekuwa tukiingia kwenye kumi bora kitaifa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, katika ukurasa wake wa Facebook, aliandika kuwa, katika matokeo hayo mkoa huo umeshika nafasi ya nane kitaifa kutoka nafasi ya 22, mwaka jana.

"Kwa dhati ya moyo wangu, nawapongeza sana wapendwa walimu wetu, wazazi na kwa upekee wanafunzi wetu ambao walikubali kuifanya elimu kuwa ajenda namba moja ya mkoa wetu, tulikubaliana awamu hii tuingie 10 bora na tumeingia, tukiwa na ufaulu mzuri wa asilimia 86," Mtaka aliandika.

Mkuu wa Miradi HakiElimu, Godfrey Boniventura, akitoa maoni ya taasisi yake, alisema ni kweli wanawapongeza wahitimu,

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# RC, DED wawekwa kikaangoni mbele ya Rais

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi na viongozi wa Wilaya ya Nachingwe, jana waliwekwa kikaangoni mbele ya Rais John Magufuli kwa madai ya kushindwa kusimamia miradi ya maendeleo.

Mbali na Zambi, wengine waliowekwa katika wakati mgumu na kutakiwa kujieleza ni Mkuu wa Wilaya ya Nachingwe, Rukia Muwango na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya, Bakari Mohammed.

Zambi na viongozi hao wengine waliitwa mbele ya Rais kutakiwa kutoa ufafanuzi wa kina baada ya kuwapo malalamiko yaliyotolewa na Hashim Mkanjaluka.

Mwananchi huyo alimweleza Rais Magufuli kwamba iko miradi mbalimbali ambayo imekwama katika wilaya hiyo na kwamba viongozi hao wanamficha bila kueleza ukweli.

"Maelezo mazuri ya viongozi wetu dani ya wilaya hii si kweli. Kwanza nakabidhi usalama wangu mikononi mwako, inawezekana ukiondoka nikabaki kwenye kibano. Kwanza kuna miradi mbalimbali haijatekelezwa, kipo kituo cha wajasiliamali," alisema na kuongeza:

"Soko ambalo walimpa mkandarasi hajamaliza, kuna redio ambayo ilinunuliwa na hela ya walipakodi lakini vimefungiwa hakuna kinachoendelea, hatuna maji, yalikuja na mwenge na yameondoka na mwenge."

Baada ya kueleza hayo, Rais Magufuli alimwita mkurugenzi kujibu malalamiko hayo ya wananchi, ambaye alikiri kuwapo kwa miradi ambayo haijakamilika.

"Ni kweli tuna stendi ambayo inaitwa stendi mpya ambayo iligharimu Sh. milioni 200. Tuliifungua Agosti na imeanza kufanya kazi, ambayo imejengwa sehemu ya kupumzikia wasafiri na mabanda 12 ya biashara," alisema.

"Sisi tulikuta imefungwa na tukaanza kuwekeza kwa kuongeza mabanda kutumia mapato ya ndani

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli akifurahia na wananchi wa Lukuledi wilayani Masasi, mkoani Mtwara jana, wakati akiendelea na ziara yake mikoa ya Kusini. **PICHA: IKULU**

# TMA yatahadharisha mvua kubwa kunyesha

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua kubwa kuanzia leo na kesho.

Kwa mujibu wa utabiri uliotolewa jana na Mamlaka hiyo, baadhi ya maeneo ya ukanda wa Pwani, mikoa ya Dar es Salaam na Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba kutakuwa na mvua nyingi.

Utabiri huo umeonyesha pia kuwa mvua hiyo itanyesha katika mikoa ya Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro.

Mamlaka hiyo ilisema kuwa uwezekano wa kiwango cha athari kinazoweza kutokea ni cha wastani.

Alizitaja athari hizo kuwa ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji, ucheleweshwaji wa usafiri, kusimama kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

# NMB yazindua malipo ya MasterCard QR kwa bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua malipo ya kimtandao kwa huduma za bodaboda.

Mfumo huo wa malipo ni wa kwanza nchini unaowawezesha abiria na wateja wa bodaboda kulipa nauli zao kwa kutumia simu zao za mkononi na fedha hizo kwenda moja kwa moja kwenye akaunti ya NMB ya dereva husika.

Huduma hiyo iliyozinduliwa jana ni mwendelezo wa juhudi za kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanatumia huduma za benki sambamba na kuhamasisha utunzaji fedha kwa njia salama na za uhakika.

Akizungumza kwenye uzinduzi

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
05-10-2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 13-10-2019 kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Chang'ombe, gari hizo zenye namba za usajili:

   **T 636 DFA / T 887 DJB**
   **T212 BTE/T 574 BZB**
   **T653 DFA/T 900 BAZ**
   **T195 BTE/T837 DJB**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **27** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.0** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.1** |

3. Njia itakayotumika: Dar es salaam Port hadi Chang'ombe kupitia Mandela road, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215454002



IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
COMMERCIAL DIVISION
AT MWANZA
TAXATION COMMERCIAL CASE NO. 05 OF 2019

I & M BANK (T) LTD. ....................................PLAINTIFF/DECREE HOLDER

*Versus*

1. EMMANUEL JUSTINE NYERERE T/A MAFUTA DISTRIBUTORS
2. REVINA JOSEPH MHONGE

.....DEFENDANTS/J/ DEBTORS

SUBSTITUTED SERVICE BY PUBLICATION

TO: 1. EMMANUEL JUSTINE NYERERE T/A MAFUTA DISTRIBUTORS
2. REVINA JOSEPH MHONGE
NEAR NGANZA FISHERIES ROAD NYEGEZI - MWANZA

**TAKE NOTICE** that Decree Holder has instituted an application for execution of decree against you with particulars of claim set out in application for execution of decree filed in this Court.

Your are hereby summoned to appear in this Court in person or by an advocate or an agent duly authorized on **7th** day of **November 2019 at 09:00 a.m.** when this application for execution of decree be for hearing.

**TAKE FURTHER NOTICE** that should you default to enter appearance in Court on the day and time mentioned above, the application for execution of decree will proceed and Ruling may be given in your absence.

Given under my and seal of the Court this 10th day of October 2019.

DEPUTY REGISTRAR
Deputy Registrar
Commercial Court
P.O. Box 693
MWANZA

115463502

# Ujerumani yamwaga bil. 20/- kuboresha afya

**Na Gwamaka Alipipi**

UJERUMANI imeipatia serikali ya Tanzania Euro milioni nane (Sh. bilioni 20) kwa ajili ya mradi wa kuboresha teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Akizungumza wakati wa hafla ya kutiwa saini kwa mkataba huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema mradi huo utaimarisha Tehama katika NHIF kwa kuwekeza katika vifaa vya kisasa na mfumo madhubuti.

"Uwapo wa Tehama utawezesha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuboresha utoaji wa huduma kwa wanachama na hatimaye kufikia lengo la kutoa huduma za afya kwa Watanzania," alisema. James alisema uimarishaji wa mfumo wa Tehama katika masuala ya bima ya afya kutaleta manufaa katika usajili wa wanachama wengi zaidi ikijumuisha sekta isiyo rasmi.

Alisema pia itaboredha namna ya kuwatambua, kuwasajili na kuwalipa watoa huduma, kuboresha utendaji wa NHIF kwa kuongeza matumizi ya Tehama katika shughuli za kila siku.

James pia alisema itasaidia kujenga uwezo kwa watumishi wa NHIF pamoja na kuhuisha mifumo ya Tehama kupatikana na kuwapo kwa mifuko miwili inayotoa huduma za bima ya afya.

"Serikali ina mpango wa kuwa na mfuko mmoja wa bima ya afya utakaojulikana kama Single National Health Insuarance Fund (SNHIF) ambao itakuwa lazima kila Mtanzania kujiunga," alisema James na kuongeza:

"Mchakato wa kutekeleza azma hii uko katika hatua mbalimbali serikalini. Hili litawezekana kwa kuunganisha mifuko mbalimbali ya bima ya afya iliyoko nchini kama Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na NHIF, SNHIF itapanua wigo wa huduma kwenda vijijini na maeneo ambayo hayajafikiwa, hivyo kutakuwa na uhitaji mkubwa wa uboreshaji wa Tehama."

James alisema si mara ya kwanza kwa Ujerumani kuisaidia Tanzania kupitia misaada na kwamba sekta zilizopokea misaada ni maji, nishati, uhifadhi wa maliasili, usimamizi wa fedha za umma na kujengewa uwezo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Alisema kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, serikali ya Ujerumani iliahidi misaada ya Euro milioni 213 (sawa na Sh. bilioni 533.14). Naye Kaimu Balozi wa Ujerumani nchini, Jorg Herrera, alisema msaada huo utaboresha huduma ya afya kwa Watanzania wengi.

Alisema serikali ya Ujerumani inatambua juhudi zinazofanywa na serikali ya Tanzania katika kupanua sekta ya afya, hivyo kuwasukuma kutoa msaada huo.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (wa pili kulia), akikagua mradi wa wodi mpya za wazazi katika Hospitali ya Mwananyamala, jijini Dar es Salaam jana, uliogharimu Sh. bilioni 2.1. Kushoto ni mhandisi wa kampuni iliyoshika kandarasi ya Mist Engineering (MISTECO), Moses Moyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**






# Serikali yatoa ufafanuzi hukumu Mahakama ICSID

**Na Romana Mallya**

MAHAKAMA ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID), imeiamuru Tanzania kulipa Dola za Marekani milioni 185 pamoja na riba kwa madai ya uharibifu ilioufanya kwenye Benki ya Standard Chartered (Hong Kong) kuhusu mzozo wa akaunti ya IPTL Escrow.

Hata hivyo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas jana kupitia ukurasa wake wa Twitter, alitoa ufafanuzi wa hukumu hiyo na kusema kuwa deni hilo siyo la serikali bali ni la Kampuni ya Kufua Umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL).

Katika maelezo yake Dk. Abbas alisema kuwa serikali itahakikisha wanasimamia utawala wa sheria ili IPTL ilipe deni lao.

"Nimekuwa nikiulizwa kuhusu kesi zilizoamuliwa za Benki ya Standard Chartered (Hong Kong) dhidi ya Tanesco na sasa serikali. Msingi wa kesi zote mdaiwa si serikali wala Tanesco, ni deni la Benki dhidi ya IPTL walilorithi miaka mingi kutoka wakopeshaji wa Malaysia."

"Kwa muktadha huo na kisheria serikali na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) ziliunganishwa tu kama kanuni za kisheria zinavyomruhusu mdai kuwaunganisha wahusika wengine kwenye kesi ili kuhakikisha au kupata uhakika kuwa analipwa madai yake," alifafanua.

Dk. Abbas aliwatoa wasiwasi Watanzania kuwa serikali haidaiwi na haijawahi kukopa Standard Charterd ya Hong Kong.

"Ila kama Baraza la Usuluhishi lilivyoamua, tutahakikisha tunasimamia utawala wa sheria kwa kuona IPTL wanalipa deni lao," alisema.

Hukumu ya kesi hiyo ilifanyika Oktoba 11, mwaka huu na jopo lililosikiliza shauri hilo liliundwa na David Unterhalter kutoka nchini Afrika Kusini, aliyeteuliwa na mlalamikaji na Kamal Hossain kutoka nchini Bangladeshi aliyeteuliwa na mlalamikiwa.

Julai 11, mwaka 2016 Unterhalter aliteuliwa baada ya kujiuzulu kwa Stanley Burnton kutoka Uingereza.

Wawakilishi wa mlalamikaji walikuwa ni Herbert Freehills kutoka Uingereza na wa mlalamikiwa ni kampuni ya uwakili ya Crax Low Partners na Rweyongeza and Company Advocates za jijini Dar es Salaam.

Mwaka jana pia, mahakama hiyo ya ICSID iliikataa rufani ya Tanesco ya kupinga hukumu ya kuilipa Benki ya Standard Chartered Dola za Marekani milioni 148.4 sawa na Sh. bilioni 336.

Katika kesi hiyo, Rais wa ICSID, Claus von Wobeser alitupilia mbali hoja za Tanesco za kuitaka mahakama hiyo kutengua uamuzi wa awali ulioipa ushindi benki hiyo ya Hong Kong, nchini China.

Fedha hizo ni madai ya malipo ya umeme baina ya Tanesco na IPTL iliyopewa zabuni ya kufua umeme wa dharura kuanzia Mei 26, mwaka 1995 huku ikidaiwa na benki hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Makonda aandaa tuzo kwa walimu, watumishi afya

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameandaa tuzo kwa ajili ya walimu na watumishi wa afya waliofanya vizuri ili kuwatia moyo wa kuendelea kuboresha sekta hizo katika mkoa wake.

Makonda aliyasema hayo jana alipotembelea ujenzi wa jengo la ghorofa nne la wodi ya wanawake linalojengwa katika Hospitali ya Mwananyamala na kusema kuwa ataanza kutoa tuzo hizo Desemba, mwaka huu.

“Kama ambavyo tulishaanza kutoa askari polisi wa mkoa wetu waliofanya vizuri katika kazi zao kwa kuwafanyia sherehe, mwaka huu mwezi Desemba tutatoa tuzo kwa walimu na watumishi wa afya wakiwamo wauguzi na wakunga kwa kazi nzuri wanazofanya na kulitoa kimasomaso jiji letu,” alisema Makonda.

Alisema walimu wanahitaji pongezi kwa kufanya vizuri katika matokeo ya darasa la saba mwaka huu na hivyo kuung'arisha mkoa wa Dar es Salaam.

“Tunawashukuru sana walimu, ambao wamefanya kazi kubwa kuhakikisha wanatutoa kimasomaso kwenye matokeo haya ya darasa la saba pia ni njia nzuri kufanya vizuri tena katika matokeo ya kidato cha nne na sita,” alisema Makonda.

Kuhusu sekta ya afya Makonda alisema, watu milioni 6.8 walitibiwa katika jiji hilo katika kipindi cha mwaka jana.

Alisema pia wanawake 126,000 walijifungua katika hospitali mbalimbali za mkoa huo na kwamba idadi hiyo inatokana na juhudi za serikali na watumishi wa afya wa mkoa huo na ndio sababu ya kuandaa tuzo hizo.

Kadhalika aliwapongeza wakazi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye daftari kwa ajili ya kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

## Kamati za Bunge kujadili ripoti ya CAG

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KAMATI za Kudumu za Bunge zinatarajia kuanza vikao Oktoba 21, mwaka huu, huku miongoni mwa shughuli zitakazofanyika ni pamoja na uchambua wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2018.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Bunge, Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, kamati hizo zitaanza shughuli hizo hadi Novemba Mosi, mwaka huu. Taarifa hiyo ilieleza kuwa kamati husika zitachambua taarifa ya CAG kuhusu hesabu zilizokaguliwa za serikali za mitaa na serikali kuu.

Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), kwa mujibu wa taarifa hiyo, itapokea na kujadili taarifa za ziada zilizokuwa zimeombwa na kamati hiyo kutoka Benki ya Posta Tanzania (TPB), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Kampuni ya Usimamizi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (Kadco), Tume ya Umwagiliaji, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA), Wakala wa Usafiri wa Mabasi yaendeyo Haraka (Dart). Pia kamati hiyo, itapitia ukaguzi wa fungu 43 la Wizara ya Kilimo, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), Ukaguzi wa Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB), ukaguzi fungu la 28 la Jeshi la Polisi, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), na fungu la 61 la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kamati hizo pia zitapokea na kujadili taarifa ya mapendekezo ya mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21. Pia kutafanyika uchambuzi wa taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika mashirika na taasisi mbalimbali nchini.

Taarifa hiyo ilieleza pia kutakuwa na taarifa za utekelezaji wa majukumu ya wizara na taasisi mbalimbali za serikali na kuchambua sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa 16 wa Bunge.


NMB
Karibu yako

Masta BODA

Safiri **Ki-Masta** zaidi
**Lipa kwa Mastercard QR**
Kupitia **NMB Mkononi**

Piga *150*66#
au Pakua **App**
Download on the App Store
GET IT ON Google Play

Kwa Taarifa zaidi piga
0800 002 002

#JiungeNaMabadiliko

mastercard



www.nmbbank.co.tz
215463601

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunapoitafakari Siku ya Chakula tuyatazame haya

**OKTOBA** 16 ni Siku ya Chakula Duniani ambayo kwa mwaka huu inahimiza umuhimu wa kuhakikisha lishe bora na endelevu inapatikana kwa wote na kwa gharama nafuu ili kuishi kwenye dunia au kwa upande wetu kuwa na Tanzania isiyo na njaa.

Takwimu zinazotolewa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) zinaonyesha kuwa watu wanakabiliwa na njaa, watoto mamilioni wasichana kwa wavulana wenye miaka mitano hadi 19 ni wanene wa kupindukia wakati mamilioni ya watoto chini ya miaka mitano ni wazito waliopitiliza, lakini wapo mamilioni wenye udumavu wa kutisha.

FAO inasema walaji, hususan wa mijini hawana muda wa kutosha kuandaa vyakula nyumbani wengi wanakula chakula kutoka madukani au barabarani na kwenye migahawa na kwa ujumla wengi hutegemea chakula chenye wanga, sukari, mafuta, chumvi kwa wingi jambo linalotishia afya na ustawi wetu. Kama ilivyo katika nchi kadhaa, Tanzania kwa upande mwingine nayo ina tatizo la watu kuwa na lishe duni inayosababishwa na milo ya watu kupungukiwa na viini lishe muhimu ambavyo vinahitajika na mwili kwa ajili ya afya njema au kusababishwa na ugonjwa, malezi na lishe mbovu ya utotoni, uchafu wa mazingira na ule wa mtu binafsi, kutofikia huduma za jamii na maji masafi.

Nchi hii kama yalivyo mataifa mengine yenye uchumi unaokua, kuna shida ya ulaji ovyo unaoleta maradhi. Kila wakati magonjwa kama kuhara damu, kuharisha, taifodi na hata kipindupindu yamekuwa changamoto kutokana na ulaji ambao hauzingatii usafi katika kutayarisha vyakula mbalimbali hasa vinavyoandaliwa mitaani na hata nyumbani.

Aidha, tunaona kuwa kuna watu ambao hawana vibali vya kuuza vyakula lakini nao ni wajasiriamali ambao huhudumia walaji bila kujali usafi wala afya za watayarishaji hao.

Kwa hiyo tuhamasishane kuwa kupata chakula chenye virutubisho muhimu na kilicho salama ndiyo ufunguo wa maisha na afya bora. Kwa sababu tunalijua hilo ni wakati wa kuwahimiza Watanzania kuacha kula vyakula visivyo salama vyenye bakteria na vimelea hatarishi na virusi pamoja na kemikali nyingine.


Watu waanze kujiambia kuwa ni lazima kuacha kula vyakula hivyo visivyo salama ambavyo ni hatari kwa kuwa magonjwa zaidi ya 200 kuanzia ya tumbo hadi kansa hutokana na ulaji huo, kwa mujibu wa FAO.

Tukumbuke kuwa ulaji wa vyakula vyenye kemikali si lazima mwandaaji atume 'sumu' lakini ni mambo kama kutumia mafuta ya kukaangia chips, samaki au mihogo kwa muda mrefu bila kuyabadilisha.

Mathalani, waandaaji wengi huchuja mafuta hayo kwa vitambaa na kuendelea kuyatumia muda wote au mwaka mzima bila kuyabadilisha. Hili ni jambo linaloweza kuwa na athari kubwa kwa afya za binadamu japo hakuna utafiti uliofanywa kuujua ukweli. Magonjwa yanayotokana na ulaji wa kemikali kama kulima na kumwagilia mboga majitaka ya viwandani nalo ni suala la kukemewa. Wapo wajasiriamali kwenye miji mingi ambao hulima na kuuza matunda na mboga yanayolimwa kwenye mazingira mabovu ambayo husambaza magonjwa kutokana na maji na ardhi inayotumiwa kwa kilimo kutokuwa salama.

Tukumbuke kuwa ulaji wa vyakula vyenye vimelea vya magonjwa, kama sambusa na mishikaki inayouzwa mitaani kutoka kwa 'wamachinga wauza nyama' vinavyouzwa sehemu mbalimbali kama shuleni na mitaani vinaweza pia kuwa chanzo cha magonjwa na vifo. Ni hatari kwa sababu huenda nyama hizo hazijapimwa, nyingine zina kimeta na magonjwa ya mifugo. Hivyo tunapoadhimisha Siku ya Chakula Duniani, tuhimize usafi wa vyakula kwa afya endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuchuja wanafunzi hakufai, wasiojiweza vyema wanolewe



Na Yasmine Protace

**NI** juzi tumesikia matokeo ya mtihani ya darasa la saba, mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiibuka kidedea kufanya vizuri kitaifa katika mitihani hiyo.

Pia, baadhi ya viongozi wa elimu katika mikoa hiyo wametoa ufafanuzi, kwamba ni matunda ya hatua kama kutoa vyakula shuleni, mitihani ya kila mara na mazingira bora ya elimu kwa jumla.Wanapaswa kupewa hongera.

Hiyo ni sura moja. Katika upande wa pili, kunaelezwa kuwapo shule hasa binafsi, ambazo katika kutafuta sifa kama zilizopatikana katika Kanda ya Ziwa mwaka huu, zina tabia ya kuwachuja baadhi ya wanafuzi, pindi wanaposhindwa kufikia wastani wa ufaulu walioupanga.

Kwa mtazamo wangu, kumuengua mwanafunzi asiyefanya vizuri katika mitihani au kumkwamisha, sio sababu ya kumaliza tatizo la ufaulu kwa wale wanaobaki.

Ikumbukwe, inawezekana hilo la kuenguliwa linaweza kuwakumba watoto waliokuwa na changamoto, hata alipofanya mitihani hawakuweza kufanya vizuri.

Kinachotakiwa hapo shuleni, ni kuhakikisha suala hilo wanalifanyia kazi, ili kuondoa malalamiko kwa wazazi.

Tunafahamu kuwa jukumu la mwalimu ni kuhakikisha wanawafundisha watoto waelewe na kufaulu zaidi madaraja walioko, wasonge kuelekea ngazi zaidi za juu kama vile vyuo vikuu.

Lakini kama walimu wataendelea kuwachuja watoto, wajue wao ndio watakuwa wamemfanya mtoto ashindwe kufikia malengo ya mbali na baadaye.

> **Hiyo ni sura moja. Katika upande wa pili, kunaelezwa kuwapo shule hasa binafsi, ambazo katika kutafuta sifa kama zilizopatikana katika Kanda ya Ziwa mwaka huu, zina tabia ya kuwachuja baadhi ya wananfuzi, pindi wanaposhindwa kufikia wastani wa ufaulu walioupanga.**

Hivi karibuni katika mahafali ya pamoja ya kidato cha nne katika shule za sekondari za Ujenzi,Victory, St.Mathew's na St. Mark's zilizoka Dar es Salaam na Mkuranga, Pwani, mmiliki wa shule hizo, Peter Mutembei, anasema mfumo wao ni kutochuja wanafunzi kwa mujibu wa uwezo wao.

Anasema watoto walio na uwezo mdogo wanawapatia masomo ya ziada ili kuwafikia wenzao wenye uwezo mkubwa darasani na kwamba watoto wameweza kuwasaidia uwezo mdogo darasani na sasa wanafanya vizuri katika masomo.

Mutembei anaziasa shule ambazo zinazowachuja watoto ziache kufanya hivyo kwa sababu ni madaraja wanakoanzia watoto hao.

Naibu Waziri Ofis ya Rais (Tamisemi), Mwita Waitara, anasema suala la kuwachuja watoto ni kosa kwa sababu hata wazazi wanakuwa wameandaa fedha za ada kwa ajili ya watoto wao ndani ya kipindi maalum.

Waitara anasema, kinachotakiwa ni kutolewa elimu itakayowezesha kufikia mbali kimasomo na pindi mtoto anapojua ni dhana inayomuweka mzazi katika hatua ngumu.'

Pia, Waitara anasema wanatambua mchango unaotolewa na shule binafsi katika utoaji elimu, kwani umewasaidia baadhi ya wanafunzi wanakosa nafasi katika shule za serikali, wanakwenda kusoma katika shule binafsi.

Waitara anazitaka shule binafsi kuwachukua watoto wasio na uwezo kabisa na kuwaingiza katika shule zao, ili wapate elimu na kuna baadhi ya watoto ambao maisha yao ni magumu na hawakubahatika kupata elimu.

MAKALA

## MIAKA 20 YA KUMKUMBUKA NYERERE

# Maadili ya Nyerere yalifika hatua iliyotukuka kimataifa

**Na Hilal Sued**

JUMATATU wiki hii ilitimia miaka 20 tangu kututoka muasisi wa taifa na Rais wa kwanza, Mwalimu Julius Nyerere.

Daima siishiwi kusukumwa na swali kwa nini Mungu Mwenyezi anakuwa 'mbahili' kwenye uzalishaji watu wazuri watakaokuwa viongozi waadilifu kitaifa na kimataifa, badala ya baadhi tunaowashudia wakipata nafasi wanaabudu kujilimbikizia, familia na maswahiba zao.

Nitamke Penye miti hukosa wajenzi.' Afrika tumepatiwa utajiri mkubwa wa madini na rasilimali nyinginezo, lakini wameambatana na katika baadhi ya maeneo ninaowaita 'wamafia.'

Kitu kikubwa Nyerere alichowapatia Watanzania mbali na ukombozi kutoka ukoloni, ni heshima ya nchi duniani. Sote tunakumbuka alivyochukia udhalilishaji wa wananchi wake.

Hakusita kuwatimua wageni waliofika nchini ama kufanya kazi au kibiashara, ilipobainika waliwatukana au kunyanyasa wazalendo. Wapo aliyowaamuru kuondoka ndani ya saa 24.

Alilinda heshima ya mwananchi kwa kuwaongoza wawe waadilifu na hakuwa na makuu ya kujilimbikizia mali. Alipenda awe mfano kwa viongozi wenzake.

KusisItiza hilo, alipitisha Azimio la Arusha mwaka 1967 lililojenga miiko ya viongozi. Alijua mamilioni ya Watanzania walikuwa masikini, hivyo viongozi wangejiingiza katika dhana ya kujilimbikizia mali, hivyo kuzaa uwezekano mkubwa kuwasahau wananchi.

Watanzania wanayafahamu yote hayo na hakuna aliyeweza kujinasibu kujilimbikizia mali kwa wazi. Yeye na familia yake waliishi maisha ya kawaida sana na ushahidi wake mio bayana.

**CHA KUSHANGAZA**

Binafsi nakumbuka kwa mara ya kwanza kabisa nilifika nyumbani kwa Mwalimu Msasani, jijini Dar ea Salam mwaka 1992, wakati nikiwa katika nafasi yangu ya uanahabari, katika moja ya magazeti ya Kiingereza baada ya tasnia ya habari iliporuhusiwa kuwa huria.

Nilikuwa katika kundi la waandishi wa habari aliyowaita kuzungumzia hoja ya kuwapo serikali ya Tanganyika, iliyoanzishwa na kikundi cha wabunge kilichoitwa G55.

Baada ya kusajiliwa getini, tulielekea kwenye jengo la ghorofa umbali wa mita 100. Lilikuwa jumba la kawaida sana ambalo mpita njia hana sababu ya kulitupia macho mara mbili.

Wengi tulishtushwa kukuta hadhi ya nyumba ile baadhi ya vioo vya madirisha (louvre) vimevunjika, nyavu za kuzuia mbu zimechanika, huku rangi za kuta zimepauka.

Binafsi nilidhani ni jengo la wasaidizi wake kama walinzi na wafanyakazi wake. Lakini, fikra hizo zilifutika muda mfupi baada ya kukaribishwa katika baraza iliyotazamana na Bahari ya Hindi kwa mbali.

Nikfanya marejeo ya picha nilizoziona magazetini zamani, hapo ni mahali alipokutana na kuongea na viongozi mashuhuri duniani katika zama za uongozi wake.

Baada ya kufahamishwa ujio wake, punde tukamuona anateremka ngazi kutoka ghorofani akifuatana na katibu muhtasi wake wa miaka mingi, Bi Joan Wickens, aliyekuwa na asili ya Uingereza na msaidizi mwingine wa kiume.

Akatupa mikono wote, nami ilikuwa ni mara yangu ya kwanza kupeana naye mkono na akatuashiria kuketi. Viti havikutosha na wengine kati yetu ilibidi tusimame. Aliketi katika kiti chake cha kubembea (rocking chair) akiipa mgongo Bahari ya Hindi.

Kuna baadhi yetu walipata nafasi ya kukaa katika viti vya sofa vitatu vilivyokuwapo, ambavyo pamoja na kile kiti chake cha bembea, vilikuwa vimechoka na hali ilionyesha kulipaswa kuwekwa samani mpya.

Nakumbuka picha za miaka ya nyuma, mahali hapo ndiko alikokutana na viongozi maarufu diniani kama Henry Kissinger, Kenneth Kaunda, Indira Gandhi na Fidel Castro. Wote walitumia sofa hizo.

Baada ya kuketi, mkutano ulianza, lakini mawazo yangu yalikuwa kwingine kabisa, - nikijaribu kuyatuliza akilini niliyoyaona. Ilikuwaje mtu huyu maarufu, shujaa wa ukombozi wa Bara la Afrika na ambaye hata baada ya kustaafu uongozi, aliendelea na umaarufu wake kwa kushikilia msimamo wake wa uongozi wa kimaadili na visheni yake ya Ujamaa, kuridhika kuishi katika mazingira duni kama hayo?

Bila shaka mazingira kama hayo ndiyo aliishi wakati katika zama za urais wake, tabia inayoeleza jinsi alivyowapiku viongozi wengi duniani katika uadilifu na kujinyima.

Kwa vipi alikataa maisha ya anasa, kitu ambacho angeweza kukipata wakati wowote kwa ishara ya vidole tu?

Wakati nikimsikiliza Mwalimu akitoa mashambulizi yake dhidi ya kikundi cha G55 ambao alisema walikuwa wanadhamiria kuuvunja Muungano, alitamka labda hiyo itokee juu ya kaburi lake.

Bado nilipandwa na hasira, kwa nini waliokabidhiwa dhamana ya kuisimamia waliamua kuyatelekeza makazi ya Mwalimu katika hali ile?

Siku ya pili yake habari kubwa katika magazeti mengi haikuwa kuhusu kile Mwalimu alichokieleza kuhusu hoja ya Tanganyika, bali hali mbaya ya makazi yake.

Mara moja, kukachukuliwa hatua ya ukarabati nyumba ya Mwalimu na baada ya wiki tatu nilifika nyubani hapo kumhoji Mama Wickens, iwapo Mwalimu anakubaliana na uamuzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuipa jina Barabara ya Pugu (Pugu Road) kuitwa Nyerere Road.'

Wakati huo Mwalimu alikuwa Butiama, lakini baada ya muda Mama Wickens (bila shaka baada ya kuwasiliana na Mwalimu kwa simu) akanijibu kwa kusema Rais mstaafu hataki jina lake lipewe barabara au kitu chochote kile wakati akiwa bado hai.

Hivyo, Halmashauri ya Jiji walioondoa jina 'Julius Kambarage' kwenye alama za barabara na kubakia Nyerere Road' kwani kina Nyerere walikuwa wengi duniani.

Leo hii baadhi ya wakuu wanaishi katika maisha hali ya juu, tofauti kabisa na hayo ya Mwalimu.


Mapema katika miaka ya 1970 nilipokuwa nafanya kazi mjini Arusha, kuna mtoto mmoja wa Mwalimu (simkumbuki) alikuwa katika Sekondari ya Arusha School, iliyokuwa ya bweni na Mkuu wa Mkoa alihisi mtoto huyo anapata adha shuleni.

Aliamua kumhamisha na kumuweka nyumbani kwake huku gari la serikali likimpeleka shuleni na kumrudisha kila siku. Mwalimu Nyerere alipopata habari alimjia juu sana Mkuu na kumuamrisha amrudishwe bwenini mara moja kijana huyo.

Ndivyo Mwalimu alivyokuwa, watoto wake wapate elimu nchini kama wengine. Leo hii, sababu inayotajwa elimu kuzorota ni watoto wengi hawasemi, kulingana na hadhi za wazazi wao. Hiyo, inapoteza umuhimu wa kuiboresha.

Mmoja wa wanafamilia wake, aliyewahi kuishi katika makazi yake, ana simulizi za kuishangaza kuhusu yalivyo maisha yake ya kawaida na alivyokuwa hapendi makuu, ikiwamo hata ilipotokea shida ya maji kupungua kwake, hakuchukua hatua kubwa zaidi ya kuendana na uhalisia, hata kudiriki kuchota binafsi inapobidi.

Sote tunaikumbuka hotuba moja ya Mwalimu Nyerere kuhusu Ikulu na biashara. Na katika kuzingatia hilo, ndiyo maana Mwalimu, kimaadili, ni vigumu kumlinganisha na kiongozi yoyote mwingine baada yake.



Julius Nyerere.**PICHA: MAKTABA.**

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# NMB yazindua malipo ya MasterCard QR kwa bodaboda

INATOKA UK. 3

wa huduma hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema huduma hii inaweka msingi wa kurasimisha sekta ndogo ya usafiri wa bodaboda. "Mnachokifanya leo kina baraka zote za serikali. Hiki kitawasaidia vijana kuongeza umakini kwenye shughuli zao na kuchangia uchumi wa Taifa," alisema Mhagama.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema huduma hiyo inatoa fursa kwa maelfu ya madereva wa bodaboda nchini kutumia huduma za benki hatua ambayo itaimarisha usalama wa fedha zao pamoja na wao wenyewe.

"Hii ni namna bora zaidi ya kurudisha uwajibikaji kwa shughuli za madereva wa bodaboda ambao mchango wao kwenye uchumi wa Taifa unatambulika. Tunazindua huduma hii jijini Dar es Salaam kisha tutaenda Mwanza, Arusha, Ruvuma, Dodoma na Mbeya wiki chache zijazo," alisema Zaipuna.

Mfumo huo wa malipo utawasaidia madereva bodaboda kukuza biashara zao kwa kuwapunguzia adha ya kuhifadhi fedha taslimu na kuwapa fursa ya kuepuka matumizi yasiyokuwa na mpangilio.

"Kwa kutumia MasterCard QR, tunatoa huduma ya uhakika wa malipo kwa madereva bodaboda kutoka kwa watoa huduma wote na benki za biashara wanaotumia huduma hii. Malipo yatafanywa kwa kutumia simu ya mkononi yenye programu ya MasterCard QR na kupunguza hatari za kumiliki fedha taslimu. Huduma hii kwa bodaboda ni sehemu ya mkakati wa benki kufikisha huduma zake kwa watu wengi zaidi," alisema Zaipuna.

Mwakilishi wa MasterCard Tanzania, Frank Molla, alisema mfumo huo wa malipo ya kidijiti unakusudia kuwapa uhuru dereva na abiria wake wakati wote wa safari huku ukimwepushia dereva uwezekano wa kuporwa au kupoteza fedha zake.

"MasterCard inakusudia kuhamasisha na kuwezesha malipo ya kidijiti nchini. Benki ya NMB inayo dira inayofanana nasi katika ujenzi wa miundombinu itakayoiwezesha jamii kufurahia ulimwengu wa malipo ya kimtandao kwa kutumia teknolojia ya kisasa," amesema.

Tayari Benki ya NMB imewajengea uwezo zaidi ya madereva 1,000 wa jinsi ya kutumia QR kufanikisha malipo kwa kutumia simu za mkononi. Mfumo huo unatarajiwa kuongeza usalama wa malipo ya kimtandao kwa sekta hiyo ndogo ya watoa huduma.

# Mil. 16.9 wajiandikisha uchaguzi wa S/Mitaa

INATOKA UK. 2

kujiandikisha kabla ya kuanza kwa kazi ya uandikishaji kwa sababu wananchi hawana uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi huo.

"Kwanza tunaishukuru serikali kwa kuongeza siku tatu ingawa bado wananchi hawana uelewa wa kutosha, ilitakiwa asasi za kiraia ziwezeshwe kutoa uelewa kwa siku 30 kuhusu umuhimu wa uchaguzi huo," alisema Henga.

Henga alisema kutokana na hali hiyo watendaji wa serikali wameamua kutumia mbinu mbadala za vitisho kinyume cha sheria na haki za binadamu.

"Kujiandikisha na kupiga kura ni suala la hiari na siyo sahihi kutumia nguvu kuhamasisha wananchi ingawa ni muhimu Watanzania kushiriki uchaguzi huo wa kuchagua viongozi wao wa mitaa," alisema Henga.

Naye Olengurumwa, alisema serikali inapaswa kuwashawishi wananchi kujitokeza kujiandikisha kwa wingi, lakini siyo kutumia vitisho.

Alisema kufanya hivyo ni kinyume cha Katiba ya Tanzania ambayo inasema ni haki ya kila Mtanzania kujiandikisha na kushiriki katika uchaguzi kwa hiari na siyo lazima.

Alisema watu wameshindwa kujitokeza kujiandikisha kutokana na sababu kadhaa ikiwamo kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi huo na kuwapo kwa shaka kutokana na kukosekana kwa uhuru katika chaguzi zilizopita.

"Huenda wananchi wanashindwa kujitokeza kujiandikisha kutokana na kukosekana kwa haki na kukatishwa tamaa na uchaguzi uliopita.

**Imeandikwa na Augusta Njoji, DODOMA Mary Geofrey, DAR**

# Wakurugenzi ruksa kusimamia uchaguzi

INATOKA UK. 2

kwamba wakurugenzi hao kabla ya kuwa wasimamizi, wanapaswa kula kiapo.

Katika kuwasilisha hoja zake, Dk. Mashamba alidai kuwa katika kutekeleza majukumu yao kama wasimamizi, wanawajibika kwa NEC ambayo ina mamlaka ya kuwaondoa iwapo watashindwa kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa kiapo.

Pia Dk. Mashamba alidai kuwa katika kiapo chao, wakurugenzi hao wanatoa tamko la kutokuwa na uhusiano na chama chochote cha siasa wanapotekeleza wajibu wao au wanajitoa uanachama wa vyama vya siasa.

Katika uamuzi wake, jopo la majaji lilikubaliana na hoja hizo kwamba kiapo cha wakurugenzi hao na watumishi wengine wa umma kuwa wasimamizi wa uchaguzi, kinawaondoa kuwa na uhusiano au ufuasi wa chama chochote cha siasa.

"Wakurugenzi wanaweza kuwa walikuwa wanashiriki masuala ya kisiasa kabla ya kuteuliwa kushika nyadhifa hizo, lakini wanapoteuliwa na baadaye kuwa wasimamizi wa uchaguzi, moja kwa moja wanazuiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa," ilieleza sehemu ya hukumu hiyo.

# RC, DED wawekwa kikaangoni mbele ya Rais

INATOKA UK. 3

ambayo hayajaisha," aliongeza. Alisema walitumia Sh. milioni 81 kujenga mabanda 26 hadi ngazi ya boma na choo pamoja na kufungua kituo ili ianze kuanza kutumika maana ni kubwa kuliko nyingine na kwamba kuna maeneo ya wajasiriamali ambayo waliahidi kuwapimia na kuwaelekeza namna ya kujenga.

Kuhusu soko, mkurugenzi huyo alisema ni la zamani ambalo lilianza ukarabati zaidi ya miaka mitano ambalo limetumia Sh. milioni 71 na kuhusu redio ya halmashauri, alisema mpango huo ulikuwapo kwa kipindi kirefu.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli alishuka kwenye gari lake na kutembea kwa miguu mpaka kwenye soko hilo kujionea yanayoendelea.

Rais Magufuli, baada ya kushuhudia hali hiyo, aliwashukuru wananchi kwa kumwelezea ukweli na kuliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha wanamlinda Mkanjaluka ili asidhurike kwa kueleza ukweli. "Nimeona kuna tatizo hapa. Lile jengo limeanza kukarabatiwa tangu mwaka jana lakini halijakamilika na Sh.milioni 71 zimetumika pale. Kulikuwa na stendi lakini matumizi yake hayajapangwa mpaka leo.

"Hapa kuna tatizo kwa sababu palitakiwa baada ya kuwatoa wananchi kwa ajili ya matumzi ya stendi, pangepangiwa matumizi mengine lakini limeachwa hivyo hivyo," alisema.

Baada ya hapo Rais Magufuli alimwita Mkurugenzi kujibu sababu za kuwahamisha wananchi kabla stendi hiyo haijakamilika ambaye alisema alifanya hivyo kutokana na maelekezo ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. Alipoitwa Mkuu wa Mkoa kueleza sababu za kuwahamisha wananchi hao, alisema aliiagiza halmshauri kuweka mazingira mazuri na kutafuta eneo la muda la wafanyabiashara wakati ukarabati unafanyika.

"Tuliagiza halmashauri itafute eneo la muda ili likarabatiwe kwa sababu mazingira hayakuwa mazuri sana. Tatizo lililojitokeza ni 'speed' (kasi) ndogo ya ukarabati," alisema Zambi.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli alihoji fedha zinazotengewa halmashauri hiyo na mkurugenzi alijibu wanatengewa Sh. bilioni 27.

Alipoulizwa pesa hizo zinavyotumika na kwa nini zisingetumika kumalizia stendi, alisema baadhi ya fedha hizo zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi, kulipa mishahara na matumizi mengine ya uendeshaji wa halmashauri.

Hata hivyo, Rais Magufuli alionyesha kutoridhishwa na maelezo hayo na kumwita Mkuu wa Wilaya ili aeleze sababu za ujenzi huo kusuasua. Naye alisema sababu za kuchelewa kukamilika miradi hiyo ni mabishano kutoka halmashauri na kamati ya usalama.

**AMWAGIZA MBARAWA**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli alimtaka Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, kuwawajibisha watendaji wake ambao ni wazembe wakiwamo makandarasi ambao wanakwamisha miradi ya maji huku akionya kuwa endapo atashindwa, atatumbuliwa mwenyewe.

Alisema hayo wilayani Masasi mkoani Mtwara baada ya wananchi kulalamikia kukosa maji huku makandarasi wakitoa sababu kwamba bado wanafanya upembuzi yakinifu mwezi wa sita sasa.

"Una watu wa ajabu, nataka nikueleze ukweli Waziri. Hao ndio wanaokuchelewesha, huwezi kufanya upembuzi yakinifu miezi sita eneo moja... Waziri nataka ndani ya wiki mbili wamalize huo upembuzi yakinifu," alisema.

# Kanda ya Ziwa yataja siri kung'ara matokeo la saba

INATOKA UK. 2

walimu na serikali kuhakikisha ufaulu umeongezeka na kumefika asilimia 81.5.

"Wakati tukipongeza bado kuna changamoto baadhi ya maeneo ambayo wanafunzi, wadau na serikali wanapaswa kuyafanyia kazi, tunapozungumza ufaulu wa asilimia 81.5 tuikumbuke asilimia 19 iliyobaki.

"Tusiangalie kwa asilimia tuangalie kwa namba yao, ukiangalia idadi waliofanya mitihani asilimia 19 ni jumla ya watoto 173,632 ambao baada ya matokeo hayo hawawezi kwenda sekondari. Idadi hii ni sawa na kuchukua uwanja wa taifa katika mechi ya Simba na Yanga, uujaze mara tatu, tunatakiwa kutafuta kiini kwa nini wamefeli," alisema.

Alitaja jambo la pili kuwa katika matokeo hayo idadi ya watoto waliofeli zaidi ni wanafunzi wa kike ambao ni 94,228 sawa na asilimia 54, huku wavulana wakiwa ni 79,404 sawa na asilimia 46.

"Utaona kwamba kati ya waliofeli watoto wa kike ndiyo wengi, tafsiri ya hapo, bado kuna mazingira magumu ya kumwezesha mtoto wa kike kujifunza, yawezekana changamoto zikawa ni mazingira ya kujifunzia, usafi wa vyoo.

Bado mwongozo wa elimu unambeba mtoto wa kiume," alisema.

Alitaja eneo la tatu kuwa ni ufaulu wa somo la Kiingereza bado upo chini, huku karibu nusu ya wanafunzi wamefaulu na nusu wamefeli.

"Takribani asilimia 47 wamefeli ambao wanakwenda kidato cha kwanza na lugha ya kujifunzia ni Kiingereza, wadau lazima suala hili tulifanyie kazi ili kutafuta ufumbuzi," alisema.

Boniventura alitaja jambo la nne kuwa ni idadi ya waliosajiliwa kuufanya mtihani huo walikuwa ni 947,077, lakini walioufanya ni 933,369.

"Changamoto ni kwamba wanafunzi wanasajiliwa, lakini hawafanyi mtihani, lazima tutafute tatizo ni nini.

"Jambo la tano, bado kuna wizi wa mitihani, kitu gani kinasababisha. Baraza waliahidi mwaka jana kudhibiti, lakini tumeona katika matokeo haya watahiniwa 909 wamefutiwa baada ya kubainika kufanya udanganyifu, maswali kwa nini udanganyifu, je, watoto hawajifunzi ipasavyo, shule zimelenga ufaulu zaidi," alihoji.

HABARI KITAIFA

# Polisi Jamii waliojeruhiwa Dar sasa wasubiri hatima

**Na Mwandishi Wetu**

SAKATA la kushambuliwa na kujeruhiwa kwa Polisi Jamii (PJ) Mtaa wa Saranga kijini Dar es Salaam, wakati wakikamata wanaochimba mchanga mtoni linafuatiliwa na Jeshi la Polisi kwa hatua za kisheria.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kamanda wa Mkoa wa Polisi Kinondoni, Mussa Taibu, alieleza kuwa jambo hilo analifuatilia, na kuahidi kuwasiliana na Mkuu wa Kituo cha Polisi Gogoni.

Polisi Jamii wanne wa kikundi cha ulinzi shirikishi Mtaa wa Saranga katika Kata ya Saranga wilayani Ubungo, walishambuliwa kwa mapanga na chepe wakati wakiwakamata watu waliodai kuwakuta mtoni wakichimba mchanga.

Walieleza kushtushwa kufika kwa polisi mmoja aliyekuwa amevaa kiraia akamvua pingu mtuhumiwa waliyemkamata kisha kuwafunga Polisi Jamii wawili na kuwapeleka katika Kituo cha Polisi Stakishari.

Tukio hilo lilitokea Oktoba Mosi saa 8 mchana kwenye mto huo katika eneo la Nguogani mpakani kati ya Mtaa wa Saranga na Msingwa wilayani Ilala.

Kamanda Mkuu wa Kikundi hicho, Mdoe Kissu, alisema baada ya tukio hilo walitoa taarifa polisi na kupewa RB mbili tofauti moja namba KMR/RB/ 10351/019 iliyofunguliwa Oktoba 2, mwaka huu.

"Katika tukio hilo licha ya kwamba tulikuwa wanne, tulijeruhiwa wawili pamoja na PJ Miho kuibiwa simu yake," alisema.

Kissu alibainisha amewasiliana na mpelelezi anayefuatilia kesi hiyo, na amemwahidi kuwa suala lake linashughulikiwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Awali Kissu alisema siku hiyo aliongozana na wenzake Karim Tarimo, Thadei Simba na Alfani Miho baada ya kupata taarifa kuna watu wanachimba mchanga, walipofika kule walikuta watu kadhaa wakiwa na chepe wakikusanya mchanga.

"Tulifanikiwa kumnasa mmoja na kumfunga pingu, lakini walitana wakajikusanya na kuzusha purukushani tulipoanza kuondoka, mtuhumiwa akakimbia na pingu kuelekea Mtaa wa Msingwa ambapo tulianza kumkimbiza," alisema.

Kissu alisema kutokana na mazingira ya taharuki, walijikuta wamevuka mto ambao ndiyo mpaka.

Alisema ghafla Miho alivamiwa na watu wenye mapanga na chembe na kuanza kumshambulia, ndipo akamfuata ili kumnusuru lakini akajikuta naye anashambuliwa na kujeruhiwa.

"Hapo ndipo tukagutuka kuwa tumeingia kwenye hatari, maana tulijikuta tunashambuliwa, mara polisi mmoja aliyevalia kiraia alifika, akawaamuru waache, kisha akataka tumwonyeshe vitambulisho vyetu, tukamwonesha, lakini katika hali ya kushangaza akaanza kutufokea," alisema Kissu.

"Alituambia sisi tunavunja amani, tukamjulisha kilichotokea, mtuhumiwa wetu akaletwa tukaamliwa tumfungue zile pingu kisha polisi yule akachukua na kuwafunga wenzetu wawili, huku akimwachia mtuhumiwa, jambo hilo lilitufedhehesha," alisema.

Alibainisha wakati huo alikuwa anavuja damu kutokana na jeraha usoni mwake, polisi hiyo aliwachukua na kuwapeleka Kituo cha Polisi Stakshari, ambako mkuu wa upelelezi aliwasikiliza kisha kuwaruhusu kuondoka.

"Kutokana na tukio hilo tumebaini kwamba kuna mtandao wa aina yake wa uharibifu wa mazingira kwa uchimbaji wa mchanga ambao unahusisha baadhi ya polisi wasio waaminifu, tunaomba Takukuru wamulike ili kusaidia kujua ukweli," alisema Kissu.



Mafundi wakijiandaa kuzibua mfumo wa maji taka ulioziba katika Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JOHN BADI**

# Nchi za SADC zaipandisha chati MSD

**Na Yasmine Protace**

NCHI za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), zimeichagua Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kuwa ni chombo ambacho kitakuwa kinasimamia mnyororo wa ugavi katika nchi hizo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, katika mkutano wa pili wa mnyororo wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

"Wataalamu kutoka maeneo mbalimbali wamekuwa wakijadiliana na kuangalia mafanikio na changamoto mbalimbali za mnyororo huo," alisema.

Alisema Tanzania imepiga hatua kwa kuangalia mnyororo wa dawa unavyopatikana ikiwamo na upatikanaji wa dawa katika vituo vya afya. Alisema bajeti imeongezwa, ambapo MSD imepatiwa magari 180.

Dk. Ndugulile aliongeza kuwa dawa zote zinapatikana katika vituo vyote vya afya na kwamba mnyororo huo umezaa matunda ambapo dawa zinatolewa kwa kipindi cha miezi miwili badala ya miezi mitatu kama ilivyokuwa awali. Aliongeza kuwa pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, kuna haja ya kuwapo na mfumo kwa ajili ya kusaidia kuonyesha matumizi ya dawa yanavyofanyika katika vituo vya afya.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, kuwapo mfumo kuwasaidia hata mahesabu ya fedha za serikali kwenda vizuri.

Akizungumzia tishio la ugonjwa wa ebola, alisema serikali imejipanga kukabiliana na ugonjwa huo kwa kuweka wataalamu mipakani wakiwa na vifaa vya kuwapima watu wanaoingia nchini.

Hata hivyo, alisema hakuna mtu yeyote aliyegundulika kuwa na ugonjwa huo nchini.

## Siku ya Bidhaa Tanzania, China

**Na Enock Charles**

KITUO cha kibiashara cha Afrika Mashariki, kimeandaa sikukuu ya bidhaa za jumla za nguo ili kutekeleza malengo yaliyowekwa kati ya China na Tanzania kwenye mkutano wa ushirikiano wa kibiashara.

Mkutano huo uliofanyika mwezi uliopita ulilenga kuwa na ushirikiano mzuri katika sekta ya biashara.

Sikukuu hiyo imepangwa kufanyika Novemba 11 mwaka huu, ikiwa ni mwendelezo wa mkutano wa kwanza uliofanyika kati ya Jimbo la Shandong la nchini China na Tanzania Septemba 5, mwaka huu, jijini Dar es Salaam ambao uliweka malengo kadhaa ya ushirikiano huo.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mwenyekiti wa Kituo hicho, Cathy Wang, imeeleza kuwa sikukuu hiyo itawezesha kuwaunganisha wanunuzi wa bidhaa hizo za nguo kutoka China na watengenezaji wa bidhaa hizo na hivyo kuwarahisishia mahitaji wafanyabiashara wa Tanzania wanaohitaji bidhaa hizo.

"Ni dhamira ya kituo hiki cha kibiashara kuondoa urasimu wa kibiashara kwa kuwaunganisha moja kwa moja wanunuzi pamoja na watengenezaji wa bidhaa mbalimbali za nguo," ilisema sehemu ya taarifa hiyo. Katika kongamano lililofanyika mwezi uliopita jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu na Uwekezaji, Angela Kairuki, aliwaomba wafanyabiashara na wawekezaji kutoka China kuwekeza kwa wingi nchini kwa kuwa kuna mazingira mazuri na rafiki ya uwekezaji.

Naye, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Biashara katika Jimbo la Shandong nchini humo, Lyu Wei, alisema wakazi kutoka Jimbo la Shandong lenye wakazi zaidi ya milioni 99, alisema wamekuja Tanzania kuangalia fursa za uwekezaji kutokana na urafiki wa muda mrefu uliopo kati ya China na Tanzania.

## Makonda aeleza umuhimu uongozi serikali za mitaa

**Na Futuna Seleman**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewataka wananchi kutumia siku mbili zilizosalia kujiandikisha kwa wingi kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji.

Aidha, amesema muundo wa kutengeneza bajeti na kujadili changamoto mbalimblai zinazowakabili wananchi, unaanzia ngazi ya mtaa hivyo ni lazima uongozi upatikane ili ziweze kushughulikiwa. Aliyasema hayo Dar es Salaam jana wakati akifuatilia uandikishaji katika baadhi ya vituo kikiwamo kituo kipya cha uandikishaji cha Mengo ambalo ni eneo la wazi huko Masaki. "Viongozi watakaochaguliwa wana majukumu makubwa na muundo wa kutengeneza bajeti unaanzia serikali ya mtaa. Ni kwenye mkutano mkuu wa mtaa unaojadili changamoto kwa mujibu wa sheria kuanzia kamati tatu za mipango uchumi na fedha, maendeleo ya kijamii ulinzi na usalama," alisema.

"Pia mkutano mkuu na mamlaka ya mwenyekiti wa mtaa ni kuishauri kamati ya maendeleo ya kata inayompeleka diwani mapendekezo. Naye akiyapata anayapeleka manispaa ili kuandaa bajeti." Aliendelea kusema kwa kuanzia hapo wanaikamilisha na kufikisha kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambayo mwenyekiti ni Mkuu wa Mkoa na inahusisha wadau wa vyama vya siasa na bajeti inapelekwa bungeni Dodoma.

Makonda alisema mlolongo huo unakwenda hadi kwenye Kamati ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ambayo Waziri wa Tamisemi anaingia nayo bungeni na ndiyo huwa bajeti kamili.

Alihoji: "Sasa msipochagua viongozi bora katika mitaa yenu barabara, uhalifu, kuzoa taka na vitu vinavyohusu maendeleo vitatoka wapi? Mtavikosa."

Aidha, pia aliwakumbusha wananchi faida ya kujiandikisha kuwa ni pamoja na kuwapo kwenye orodha ya daftari la mtaa kuwa endapo mtu anapata shida ni rahisi kumsaidia na akikosekana huhesabika kama mhalifu.

"Kwa mujibu wa sheria moja ya jukumu la uongozi wa serikali ya mtaa kutumia rejista ya wananchi wanaoishi katika mtaa husika jiandikisheni orodha itatumika kama kitambulisho cha mkazi halali ndani ya mtaa," alisema Makonda. Pia alipongeza jitihada zinazofanywa na wabunge Mussa Azzan Zungu wa Ilala na Bonna Kamole wa Segerea kwa kufanya kazi ya uhamasishaji wananchi ambao wamewezesha watu wengi kujiandikisha. Aliwakemea baadhi ya viongozi wa Kinondoni na Ubungo wanaopita mitaani na kuwakataza wananchi kujiandikisha.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James (kushoto) na Kaimu Balozi wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Jorg Herrera, wakionyesha nakala za mikataba baada ya kutiliana saini, jijini Dar es Salaam jana, ambapo shirikisho hilo, limetoa msaada wa Sh. bilioni 20 kwa serikali, kwa ajili ya kuboresha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), katika mfuko wa Bima ya Afya nchini NHIF. **PICHA: MAELEZO**

# Mkuu wa polisi apewa siku tatu

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evaristo Ndikilo, ametoa siku tatu kwa Mkuu wa Polisi Kibiti, kueleza sababu za kutokamatwa mtuhumiwa ambaye ni mfugaji, aliyedaiwa kuwajeruhi mke na mume wakulima wa kijiji cha Mtawanya.

Ndikilo ametaka kupata maelezo hayo kutoka kwa mkuu huyo, akieleza kuwa mtuhumiwa hajakamatwa licha ya kutoa taarifa kituoni Bunge kwa zaidi ya mara mbili.

Aidha, alimtaka kuachia ngazi endapo atashindwa kulifuatilia suala hilo ambalo linaichafua serikali na Jeshi la Polisi, kwani inaonekana kuwa, wafugaji wamewatia mfukoni kwa kutumia nguvu ya fedha.

Alitoa maelekezo hayo katika Kijiji cha Mtawanya, alipokwenda kuhamasisha wananchi kujiandikisha katika daftari la wapigakura. Alifika hapo baada ya kupitia kituo kimoja kilichopo kijijini hapo na kuzungumza na wananchi.

Katika mkutano huo wananchi licha ya kumhakikishia mkuu huyo kuwa watajiandikisha, walitaja kero kubwa ya wafugaji kuwaonea, kuwapiga, kuwajeruhi kisha kuachia mifugo yao kula mazao yao.

Walilalamika kuwa licha ya kwenda kuripoti polisi hakuna hatua zinazochukuliwa na watuhumiwa kuendelea kuwatambia.

Akitoa maagizo Ndikilo alisema: "Hili halikubaliki kama kweli mkulima ameonewa amepigwa na mazao yake yanaliwa. Ameripoti polisi kwa maana ya chombo cha serikali lazima atasaidiwa kupata haki yake hivyo, hili halikubaliki". Aliongeza kuwa uzembe huo unalichafua Jeshi la Polisi na serikali yake iliyopewa dhamana ya kulinda raia na mali zao, polisi inaonekana ina matatizo kumbe ni baadhi ya maofisa wachache na mapungufu yao kwa kutokuwa waadilfu.

Alisema haiwezekani mtu yeyote apige mke na mume halafu polisi ishindwe kumkamata mtuhumiwa, hivyo lazima apatiwe maelezo ya jambo hilo ndani ya siku tatu na taarifa kama mtuhumiwa aliyewajeruhi walalamikaji hao amekamatwa.

Alitaka hatua zichukuliwe mara moja mtuhumiwa akamatwe na kuhojiwa kwa nini amefanya kitendo hicho kinyume chake, Mkuu wa Kituo Bungu achukuliwe hatua, ama ajihesabie kazi imemshinda.

Alisema wananchi wakilalamikia tuhuma hizo mbele ya viongozi wa kitaifa ni aibu kwa serikali nzima ya mkoa wa Pwani na

hivyo hatokubali mkoa huo kuchafuliwa kwa maslahi ya watu wachache.

Aliongeza kuwa wananchi wengi wamezungumzia matatizo ya wafugaji, lakini aliwataka kuacha kubaguana na sheria zifutwe ili kila upande utende haki kwa mwenzie.

Mkulima aliyejeruhiwa alilalamika mfugaji kumjeruhi usoni na mkononi pamoja na mkewe ambaye yuko hospitalini naye akipatiwa matibabu.

Alisema si mara ya kwanza kufanyiwa hivyo licha ya kupeleka taarifa hizo Kituo cha Polisi Bungu hakuna hatua zinazochukuliwa.

Baadhi ya kinamama nao waliangusha vilio wakilalamika kuwa wafugaji hulisha mazao yote na kibaya hawana uwezo wa kupambana nao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Onesmo Lyanga, aliahidi kulifuatilia suala hili na kuwataka wananchi kupiga simu wanapoona changamoto zao zimeshindikana kutatuliwa.

"Nilisambaza vipeperushi, namba zangu niliwapa na leo nawapa tena toeni taarifa tutazishughulikia kwa kutenda haki kila upande," alisema Lyanga.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti Gullam Hussein Kiffu, aliwataka wananchi wanapokuwa na kero kufika ofisini kwake moja kwa moja ili zitatuliwa mapema akiwaambia milango iko wazi saa zote.

# Inahitajika sheria ya matumizi mbegu bora

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WIZARA ya Kilimo, imeshauriwa kutunga sheria itakayomtaka kila mkulima kutumia mbegu bora pekee na kuachana na mbegu za kuokoteza mitaani.

Aidha, sheria hiyo iainishe kuwa ni kinyume kutumia mbegu duni na iwapo muhusika akibainika achukuliwe hatua kisheria, jambo litakalowalazimisha wakulima kutumia mbegu za kisasa na kujikita kwenye kilimo cha kitaalamu na chenye tija kama ilivyo kwa Kenya na Ufaransa. Hayo yalibainishwa jana na Mtafiti Msaidizi wa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Matengia Swai, alipozungumza na wanahabari. Alikuwa anazungumzia uzalishaji wa mbegu za muhogo na kusema iwapo itungwe sheria itakayombana mkulima asipolima kilimo cha kitaalamu kwa kutumia mbegu zilizothibitishwa, achukuliwe hatua kama zilivyo nchi za Ufaransa na Kenya. Alisema, Ufaransa wamekuwa na sheria inayomtaka mkulima kutumia mbegu bora pekee na si vinginevyo na ikibainika kwenda kinyume huchukuliwa hatua.

Alisema, changamoto ya wakulima kutofuata maelekezo ya wataalamu ikiwamo matumizi ya mbegu zilizothibitishwa ubora na mbolea inaendelea kuleta matatizo kwenye suala la kilimo siku hadi siku.

Swai alisema wakulima hawana utaalamu wa kilimo kwenye mazao mbalimbali na kwamba hawazingatii wala kufahamu kanuni za kilimo zinazoshauriwa na wataalamu.

Hivyo, alisema, Wizara ya Kilimo haina budi kutumia wataalamu waliopo kuhamasisha wakulima kulima kisasa na kwa manufaa.

"Wengi wamekuwa na visingizio mbalimbali, muhimu ni kwamba wapite kwa wataalamu kupata ushauri, mtu anaweza akalima kwa mwaka wa kwanza kwa mbegu hiyo na mwaka unaofuata akairudia na akikosa, anaanza kulalamika, kumbe hakufuata ushauri," alisema Swai.

Mkulima wa muhogo kutoka wilayani Mvomero, Erasmo Komba, alisema suala la kulima kwa kufuata ushauri wa kitaalamu ni jema lakini linahitaji mtaji mkubwa kufuatia mbegu na mbolea kuwa na gharama kubwa tofauti na hali ya uchumi wa wakulima.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akiwahoji baadhi ya watuhumiwa wa wizi wa vifaa vya mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520, unaopita katika baadhi ya vijiji vya wilaya hiyo, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mbaroni tuhuma za wizi vifaa vya maji

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WATU saba wakiwamo wenyeviti wawili wa vitongoji, wametiwa mbaroni kwa tuhuma za wizi wa vifaa vya mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520.

Tukio hilo la wizi lilitokea juzi katika eneo la ujenzi wa moja ya visima 53 vilivyoko Kata ya Kikwe Kijiji cha Maweni wilayani Arumeru.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watu hao wamekamatwa lakini majina yao yamehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi. Alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao, waliwawekea mtego baada ya kupata taarifa kutoka kwa baadhi ya wananchi wanaoshirikiana na wafanyakazi na walinzi wa eneo la mradi kuiba vifaa vya ujenzi vikiwamo nondo, mabomba na mabati.

Alisema kutokana na taarifa hizo, walifanya msako wa ghafla na wa kushtukiza katika nyumba za baadhi ya wafanyakazi wa mradi huo waliodaiwa kuiba vifaa hivyo na kukuta zaidi ya nondo 40 zikiwa zimetelekezwa nje ya nyumba ya mwananchi mmoja ambaye awali alikuwa akifanya kazi katika mradi huo.

"Hizi nondo zilizotelekezwa hapa inaonekana wezi hawa walishtukia na kuhisi kuwa tunawafuatilia, hivyo wamekimbia na kuzitelekeza hapo," alisema Muro.

Muro alisema msako huo aliufanya alfajiri mpaka mchana wa juzi na baada ya kuwakamata, alitoa onyo kwa watu wote wanaotaka kuhujumu miradi ya maji, kuacha tabia hiyo mara moja kwa kuwa atakayekamatwa angemchukulia hatua kali za kisheria.

"Watu wote watakaobainika kuiba na kuficha vifaa vya ujenzi katika miradi hii tutawachukulia hatua kali ili iwe fundisho kwa wengine," alisema.

Diwani wa Kikwe, Paul Shango, alipongeza jitihada zinazofanywa na Mkuu wa Wilaya kwa kusimamia miradi hiyo kikamilifu, huku akiwataka wananchi kutothubutu kuhujumu miradi hiyo kwa kuwa ina manufaa makubwa kwa wananchi hasa upatikanaji wa uhakika wa majisafi na salama.

Katika hatua nyingine, Muro ametoa mwezi mmoja kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Arumeru, kuwahamisha askari polisi ambao si waaminifu wanaofanya kazi katika Kituo cha Polisi Mbuguni.

Muro ametoa amri hiyo baada ya kupokea malalamiko kuwa baadhi ya polisi wanatuhumiwa kuwalea wezi wanaoiba vifaa katika miradi hiyo.

## NMB yaja na mkopo rahisi kwa wateja

**Na Allan Isack,** MIRERANI

WAFANYAKAZI wa Benki ya NMB Tawi la Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wamezindua Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa kutangaza mpango mpya wa mikopo rahisi kwa wateja uitwao 'Afya Loan'.

Meneja wa NMB Tawi la Mirerani, Allan Kombe, akizungumza juzi na wadau na wafanyakazi wa benki hiyo, alisema mkopo huo ni huduma mpya maalum ya watu au taasisi binafsi.

Kombe alisema lengo la kuzinduliwa kwa mkopo huo ni kufungua milango ya kuwakopesha watu binafsi wenye maduka ya dawa, mashirika, taasisi binafsi, maabara, zahanati na vituo vya afya vya watu binafsi.

Alisema 'Afya Loan' pia itaimarisha na kutoa huduma za afya zinazotolewa na watu binafsi au mashirika na taasisi binafsi.

"Mpango huu utakuwa endelevu kwa wiki hii ya huduma kwa wateja itaendelea kwa muda wa mwezi mzima wa Oktoba," alisema Kombe. Ofisa Tarafa ya Moipo, Joseph Mtataiko, aliwapongeza wafanyakazi wa NMB Tawi la Mirerani, kwa kutoa huduma vizuri kwa wateja pindi wanapofika kwenye benki hiyo.

Mtataiko alisema watumishi wa serikali, wafanyabiashara, wakulima, wafugaji, wachimbaji madini na watu wa kada mbalimbali za Mirerani wanaopata huduma kwenye benki hiyo, kutokana na huduma nzuri zinazotolewa kwenye benki hiyo.

Meneja wa Huduma kwa Wateja wa benki hiyo, Bahati Nelson, alitumia fursa hiyo kuwakaribisha wadau mbalimbali kufika kwenye ofisi za NMB kwa ajili kupatiwa huduma bora na za uhakika.

# Waandishi watakiwa kuwafichua watoa rushwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Arusha, Frida Wikesi, amewataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao kufichua rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akifungua semina ya siku ya waandishi wa habari na uongozi iliyoandaliwa na Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Wikesi alisema viongozi wanaopenda kutoa rushwa ili wachaguliwe si viongozi bora kwa manufaa ya nchi.

"Hawa watu wanaotoa fedha au kanga na vitu vingine ili wachaguliwe, lazima watakapochaguliwa watajijali binafsi badala ya kuwahudumia wananchi. Lakini watu pekee wakutusaidia kuwafichua watu hao ni wanahabari kwa kutumia kalamu zao," alisema.

Wikesi alisema Mkoa wa Arusha umeelimika katika utoaji taarifa wanapoona viashiria vya watu wanaotoa rushwa na wamekuwa wakishirikiana na Takukuru katika kuwanasa kulinganisha na baadhi ya mikoa.

Pia aliwaomba wanahabari kuwafichua na kuwalaani watu wote wanaojihusisha na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema ukatili upo wa aina nyingi kama wa kukatiza masomo wanafunzi kwa kuwapa mimba na kusababisha kukatiza ndoto zao na mauaji ya wazee kwa imani za kishirikina.


"Lakini mtumie kalamu zenu kupigia kelele mambo haya mtayakomesha kikubwa msitangulize maslahi mbele ya jamii, maana baadhi yenu hamtaki kuandika habari bila kulipwa kwa kufanya hivyo hamtalisaidia taifa," alisema.

Aliwahimiza wanahabari wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi hasa kuelekea katika uchaguzi ujao kwa sababu wanaweza na hakuna sababu ya kuogopa au kusubiri nafasi za kuteuliwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTPC, Abubakar Karsan, aliwataka waandishi wa habari nchini kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kwenye vyama vya wanahabari, siasa, taasisi za dini na jamii kwa kuwa wanaweza kuleta mabadiliko ya kiuongozi.

"Acheni kuachia wanaume kugombea nafasi zote za kiongozi. Mfano ukiangalia katika klabu nyingi za wanahabari nchini, viongozi ni wanaume. Ukikuta mwanahabari mwanamke ni kiongozi basi nafasi yake itakuwa ya mtunza hazina na si katibu au mwenyekiti," alisema Karsan.

Alisema anaamini baada ya mafunzo hayo wengi watajitokeza kugombea nafasi mbalimbali kwenye klabu na hata kwenye uchaguzi wa serikali za



# Meneja wa benki atinga kortini na mashtaka 32

**Na Paul William,** MOSHI

ALIYEKUWA Meneja wa Benki ya Ushirika ya Mkoa Kilimanjaro (KCBL), Joseph Kingazi (39), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, akikabiliwa na mashtaka 32.

Katika makosa hayo yamo ya ufisadi, wizi na utakatishaji wa fedha zaidi ya shilingi bilioni nne.

Kingazi anashtakiwa kutenda makosa hayo kati ya Januari na Desemba 2013 hadi mwaka 2017, akitumia nafasi yake ya Meneja wa Benki kufisidi mabilioni hayo ya fedha zikiwamo programu ya miundombinu ya masoko, uongezaji thamani na huduma za kifedha vijijini uliopo katika Ofisi ya Waziri Mkuu (MIVARF).

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi, Namba 10 ya mwaka 2019, ilisomwa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Pamela Mazengo.

Hati ya mashtaka ilisomwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Lucy Kyusa, akisaidiwa na Rehema Mteta, wakati upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Ephraim Kowesenge.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka anakabiliwa na makosa 32, tisa ni ya kutakatisha fedha, nane ni ya kughushi, saba ni ya wizi na nane ni ya kutumia nyaraka za uongo.

Katika kosa la kwanza hadi la nne, meneja huyo anashtakiwa kughushi, kutumia nyaraka za uongo pamoja na kutakatisha fedha na wizi wa Sh. milioni 113.2 fedha ambazo ni za mradi wa MIVARF.

Katika kosa la tano hadi la nane, Kingazi anatuhumiwa kutakatisha fedha na wizi wa Sh. 138,220,000 huku katika kosa la tisa hadi la 12 akishtakiwa kwa kutakatisha na kufanya wizi wa zaidi ya Sh. milioni 420.

Makosa ya 13 hadi 16 anashtakiwa kutakatisha na kufanya wizi wa Sh. 371,445,000 na kosa la 17 hadi 28 ni kutakatisha na wizi wa Sh. milioni 816.3.

Katika kosa la 25 hadi 28 anashtakiwa kutakatisha fedha na wizi wa Sh. 111,955,000 huku katika kosa la ishirini na tisa hadi thelathini na mbili anashtakiwa kutakatisha fedha na wizi wa Sh. 252,700,000 zote zikiwa za MIVARF.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Mkazi Pamela alisema, mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi na kwamba Mahakama Kuu ndiyo yenye mamlaka hayo, hivyo mshtakiwa hakutakiwa kujibu lolote na kupelekwa rumande hadi kesi hiyo itakapotajwa tena Oktoba 29 mwaka huu.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, akizungumza na wananchi wa Matadi, Kata ya Endumeti, Wilaya ya Siha jana, kuhusu zoezi la uandikishaji. Kilimanjaro inashika nafasi ya mwisho katika uandikishaji wa wapigakura katika uchaguzi wa vijiji, mitaa na vitongoji 2019. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Waanza kuvurugana uchaguzi wa S/Mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MAJERAHA ya kukatwa mapanga pamoja na tuhuma kuhusu viongozi wa CCM kutaka kupitisha jina la mtu ambaye wananchi hawamkubali kugombea uenyekiti wa mtaa wa Shabaha, Wilaya ya Hai, yanadaiwa kuwagawa wananchi wa eneo hilo.

Kuna madai kuwa umeibuka mgogoro wa kiuongozi unaofukuta chini kwa chini.

Anayedaiwa kufanyiwa mizengwe ni mwenyekiti wa sasa wa mtaa huo, Emanuel Laizer.

Kutokana na mgogoro huo, wakazi wa mtaa huo wamemwangukia Mkuu wa Wilaya, Lengai Ole Sabaya, kuingilia kati mgogoro wa uongozi CCM.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, jana walisema mchakato wa kura za maoni wa kumpata mgombea uenyekiti wa mtaa huo hazikufanyika kwa haki, hivyo kuomba urudiwe.

Mtaa wa Shabaha una vitongoji vitatu, na kwamba wananchi hao walisema vitongoji viwili vya Miembeni na Ngungu vilimpigia kura aliyekuwa mwenyekiti wa kijiji hicho, Emanuel Laizer na si mpinzani wake Mosoka Singo, aliyepitishwa.

Wananchi wa vitongoji hivyo walidai katika mchakato wa kumchagua mgombea wa CCM mtaa huo, haukufanywa kwa haki. Mmoja wa wananchi hao Mkindi Molel, alisema wagombea wawili waliosimamishwa na CCM Moseka Singo na Emanuel Laizer, lakini upigaji wa kura haukufuata taratibu na haki za uchaguzi. Alisema wakala wa Emanuel Laizer, walifukuzwa kituoni na kuiba kura kwa kutumia mwanya wa watu ambao hawajui kusoma na kuandika ambao walikuwa wengi katika mtaa huo. Mery Nkya, alisema hatua ya viongozi wa siasa kata kuwafukuza mawakala wa Laizer ni kiashiria tosha kuwa kura ziliibwa na kwamba wananchi wa vitongoji viwili vya Miembeni na Ndungu walimchagua Laizer na si mpinzani wake.

Komotoi Saitoti, alidai hujuma hizo zilifanywa msimamizi wa uchaguzi huo ambaye ni Katibu wa CCM Wazazi Wilaya ambaye anadaiwa badala ya kuwa msimamizi wa uchaguzi alijigeuza wakala wa kuiba kura za Laizer na kumpa Sengo.

"Sisi tunachokitaka ni uchaguzi urudiwe na ufanyike kwa haki, na kwamba yoyote atakeshinda kwa kuzingatia haki tutamuunga mkono maana sisi tunataka haki itendeke na si kupendelea mtu mmoja," alisema.

Alisema endapo uchaguzi huo hautarudiwa wako tayari kuhama chama na kumuunga mkono mgombea yoyote wa upinzani ambaye atakayesimama kugombea katika mtaa huo.

Alisema Laizer, alikuwa Chadema na kuondoka kwa kuunga mkono juhudi za serikali na kwamba wao walihama naye lakini sasa wamemwibia kura na kumpa mtu ambaye hajashinda.

Wapigakura waliojiandikisha kwenye mtaa ni 448, lakini kura zilizopigwa ni 507, hapo ndipo utaka uliopo, Laizer alipata kura 251 huku mpinzani wake Moseka Sengo, akipata kura 256.

## RC ajitosa mitaani uandikishaji kura

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATIKA juhudi za kuwahamasisha wananchi kujiandikisha kupiga kura Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amefika katika magulio kuwataka wananchi kujiandikisha.

Aidha, alifika kwenye maeneo yenye watu wengi, akiagiza maofisa waandikishaji wa daftari la wapiga kura za uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji, kuhamisha vituo vyao kwa dharura na kuwafuata wafanyabiashara walioshindwa kujiandikisha.

Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Dar es Salaam, mapema wiki hii ilitajwa kuwa ndiyo iliyokuwa chini kwa uandikishaji, ikilinganishwa na mikoa mingine.

Kwa mujibu wa Dk. Mghwira, uandikishaji katika mkoa huo ulikuwa asilimia 48, wakati halmashauri za mkoa huo zilizo chini ya kiwango cha uandikishaji ni Manispaa ya Moshi yenye asilimia 27, Moshi Vijijini asilimia 38 na Rombo asilimia 39.

Nyingine ni Siha asilimia 41, Same asilimia 45, Hai asilimia 45 na Mwanga ambayo ndiyo kinara ikiwa iliyokuwa imeongoza kuandikisha kwa asilimia 54.

Kiwango cha chini cha uandikishaji katika mkoa huo kinawaumiza vichwa viongozi, na sasa kila wilaya na hata ngazi ya mkoa, wamekuwa wakipita huko na huko hasa maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi na mwingiliano wa watu kuwahamasisha wananchi kujiandikisha.

Alipokwenda katika soko la kimataifa la Kumbukumbu ya King George maarufu kama 'Maimoria' Mkuu wa Mkoa alisema: "Manispaa ya Moshi, Mkurugenzi uko hapa, waandikishaji watoke kule waje wawafuate wananchi na waandikishwe wakiwa kwenye eneo lake la kazi.

"Na sehemu nyingine, naagiza waandikishaji watoke na kuja kwenye maeneo yenye mwingiliano mkubwa wa watu na kuandikisha. Lakini nawaomba kila mfanyabiashara na hata wanunuzi mjiandikishe, tuko na maofisa ambao nimefuatana nao."

Lakini Dk. Mghwira alisisitiza wanaoandikishwa ni lazima wafahamu kwamba watakwenda kupiga kura katika maeneo yao na si katika soko la Maimoria.

"Sisi tunategemea taarifa kutoka kwa viongozi hawa wa vijiji na mitaa, hatutaki shughuli zikwame au zisimame, ndiyo maana nimeagiza mje muandikishwe hapa hapa sokoni na utafuatwa kila mmoja,"alieleza Mghwira

ama
ALHAMISI OKTOBA 17, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



## Madhara matatu anayopata mtoto pindi inapotokea ajali

Ukurasa 19




## Fahamu tofauti za maumbile katika kumudu shinikizo damu

Ukurasa 20



Ukurasa 14

## Msimamo wa Manyara kuhusu dira ya unyoyeshaji kimataifa




# Mkunga asiyesomea: Nje ya wodi nimesaidia 1900; wodini 700

Ukurasa 16



Mnyama sokwe. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Malaria mpya kutoka kwa sokwe

**Na Mwandishi Wetu**

WANASAYANSI wanasema kuna msururu usio wa kawaida wa matukio umeibua aina hatari ya malaria kutoka kwa wanyama sokwe, ukahama na kuanza kushambulia binadamu.

Maelfu ya watu wanatajwa kufariki kutokana na malaria kila mwaka, kwa sababu ya vimelea vya Plasmodium falciparum, iliyofanyiwa uchunguzi na watafiti.

Wataalamu wamegundua, sokwe ndio wanaobeba vimelea hiyo, lakini mabadiliko yaliyotokana na maumbile, miaka 50,000 iliyopita iligeuka kuwa tishio kwa wanadamu.

Matokeo ya utafiti uliochapishwa katika jarida la PLoS Biology, ni kwamba huenda ikavumbua njia mpya ya kukabiliana na malaria, ugonjwa unaosababishwa na vijidudu vya Plasmodium

Inafafanuliwa, kuna aina tofauti ya vijidudu, vinavyowaathiri binadamu peke yake ni Plasmodium falciparum.

Ilihama kutoka kwa sokwe mtu na wakati sawa na ule ambao binadamu walihama kutoka Afrika, miaka kati ya 40,000 hadi 60,000 iliyopita, watafiti wanasema.

Vijidudu hivyo huathiri chembehai kwenye ini na chembe nyekundu za damu na kusababisha dalili nyingine, ikiwamo upungufu wa damu.

Ni ugonjwa unaoathiri mwili mzima, ikiwamo ubongo na unaweza kuua. Takriban watu 435,000, wengi wao watoto wanakufa kutokana na malaria ya kila mwaka.

MAMA & MTOTO...

# Msimamo wa Manyara kuhusu dira ya unyoyeshaji kimataifa

**Na Jaliwason Jasson, Babati**

UTAMADUNI wa sehemu nyingi za Kiafrika, wanawake wanapojifungua huanza kuwanyonyesha watoto wao kama sehemu ya kuwapatia mlo wa kila siku.

Zipo jamii zinazoendelea zikiwa na mtazamo hasi dhidi ya kanuni za unyonyeshaji, kwa mitazamo tofauti kuhusu wakati mtoto anaotakiwa apate haki hiyo ua kunyonya .

Wapo wanaoamini mtoto baada ya kuzaliwa anapaswa kunyonya maziwa ya mama ambayo yana virutubisho vya msingi na wengine ambao kwa mujibu wa mila na desturi zao, wanaamini maziwa ya mama kwa wakati huo hayafai, kwa sababu ni machafu na wanawapatia watoto mbadala wa maji ya moto.

Ni kitendawili ambacho jamii bado inaumiza akili za wazazi na kitatenguliwa kupitia elimu juu ya unyonyeshaji, badala ya kubaki na imani, mila na desturi.

**DAKTARI ASEMA**

Katika kujua ukweli huo, Nipashe imekutana na Daktari Anna Akaro kutoka Kitengo cha Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Manyara, anayetetea dhana ya kunyonyesha kuwa kitu ambacho ni muhimu sana kwa mama na mtoto maana kunyonyesha kwa mama kunajenga uhusiano mkubwa kati ya mama na mtoto.

"Maziwa ya mama yana virutubisho vyote na kunyonyesha vizuri bila ya kumchanganyia mtoto kitu chochote, ni njia mojawapo ya uzazi wa mpango, maana mama hawezi kupata mimba. Hivyo, kinamama wananyonyesha vizuri, inawasaidia sana," anaeleza Dk. Akaro

Kwanini wanaojifungua hawataki kunyonyesha muda unaoshauriwa kitaalamu? Dk. Akaro anasema suala hilo kwa wanaogoma kunyonyesha yanaweza yakawa mambo yao binafsi, kukosa elimu na wengine kuharibiwa na utandawazi.

Aidha, Dk. Akaro anasema, mama anapomnyonyesha vizuri mtoto, inasaidia kupunguza majipu yanayoshika maziwa na kuyazuia yasitoke, pia inasaidia kutoa lishe kwa mtoto na kadri mama anavyonyonyesha maziwa yanazidi kutoka .

Mtaalamu wa watoto, anasema mama anapojifungua, anatakiwa kuanza kumnyonyesha mtoto maziwa yake mfululizo kwa miezi sita, bila ya kumpatia kingine chenye virutubisho vinavyoweza kupatikna kwenye chakula.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika uzunduzi wa Wiki ya Unyoyeshaji mwaka huu.

> **Unajua ukizembea hapo chini, watoto watapata matatizo. Wanaofanya kazi wanyonyeshe, wasiwe na visingizio, wakiweza asubuhi kukamua maziwa kwa ajili ya kuwapa watoto, ila usafi uzingatiwe kwa kiwango cha hali ya juu. Wanapewa muda...**

Dk. Akaro anaelimisha zaidi, hata maji yanayohitajika katika mwili wa binadamu kwa kiwango kikubwa yanapatikana ndani ya maziwa ya mama. Anaeleza agalizo: "Kinamama ambao hawawanyonyeshi watoto wao wanawanyima haki yao ya msingi."

Anaendelea: "Ingekuwa kuna sheria ya kuwabana, wangestahili kubanwa na kama watu wa haki za binadamu wangeweza kuwapata wanawake ambao hawataki kunyonyesha, wakawaadhibu, maana kuacha kumnyonyesha mtoto tukiacha ile haki ya kuzaliwa na kuishi na kunyonya ni haki ya mtoto."

Mtazamo wake wa kitaalamu, ni kwamba mtu naapokuwa mzazi anakuwa na wajibu rasmi wa kumpa mtoto chakula, hivyo kinamama wanatakiwa kujitambua na kuwanyonyesha mara nyingi kadri wawezavyo.

"Unajua ukizembea hapo chini, watoto watapata matatizo. Wanaofanya kazi wanyonyeshe, wasiwe na visingizio, wakiweza asubuhi kukamua maziwa kwa ajili ya kuwapa watoto, ila usafi uzingatiwe kwa kiwango cha hali ya juu. Wanapewa muda wa kunyonyesha waruhusiwe na wahutumie vizuri,"anaeleza.

**BOSI LISHE**

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Babati Bernadetha Tembo, anasema wanawake wanapojifungua, ni lazima waanze kunyonyesha watoto wao kwa mfululizo kipindi cha miezi sita bila ya kuwapa chochote, maana maziwa ya mama yana virutubisho na kinga, kwani katika umri huo, uwezo wa utumbo kumeng'enya chakula bado ni mdogo.

Pia, anataja madhara yanayoweza kupata akianza kula vyakula vingine, badala ya maziwa ya mama, ni kuchubuka utumbo na kupata magonjwa ya kuhara.

Inaendelea Uk. 15

AFYA

Inatoka Uk. 14

MAMA & MTOTO...

# Msimamo wa Manyara kuhusu dira ya unyoyeshaji kimataifa



Mtoto aliye katika mikono ya malezi salama. Lishe ni kiungo muhimu.



Mama akimnyoyesha mwanawe. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**KIMATAIFA**

Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema takribani asilimia 40 ya watoto chini ya umri miezi sita ndio wanaoishi kwa kunyonyeshwa tu, pasipo kuchanganya milo kama inavyotakiwa.

Pia, WHO ina mtazamo zaidi ya watoto 820,000 wenye umri chini ya miaka mitano wanaweza kunusurika kila mwaka, ikiwa hadi umri wa miezi 23 wangenyonyeshwa kikamilifu.

Shirika hilo linaeleza umuhimu wa unyonyeshaji, kwamba ni nia sahihi ya kuhakikisha mtoto anakuwa na afya njema na anaendelea kuishi.

Unyonyeshaji mtoto unamsaidia kuboresha uwezo wa kutambua akili(IQ), mahudhurio shuleni, pia anahusishwa na mapato ya juu katika maisha yake ya utu uzima.

"Kunyonyesha kwa muda mrefu, pia kunachangia afya na maisha bora ya mama, kwani humpunguzia hatari ya kupata saratani ya mfuko wa mayai ya uzazi na matiti, na watoto na vijana wadogo walionyonyeshwa wakiwa wachanga, wana uwezekano mdogo wa kua na uzito wa mwili wa kupindukia," ilifafanua taarifa ya shirika hilo

WHO inatafsiri maziwa ya mama ni zaidi ya chakula kwa mtoto. Pia, ni dawa ya magonjwa na vifo vya wazazi wanaotakiwa kuhakikisha wanawanyonyesha inavyotakiwa.

Kwa mujibu wa Save The Children, utapiamlo unachangiwa na kutonyonyeshwa ipasavyo na unakadiriwa kusababisha vifo vya watoto milioni 2.7 kila mwaka.

Pia, inaelimisha mguso wa mwili na kunyonya, kunavyosaidia kuchochea uzalishaji maziwa ya mwanzo baada ya kujifungua na kunatambuliwa kama "chanjo ya kwanza" yenye virutubisho na kinga ya mwili.

Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef), katika wiki ya unyonyeshaji iliyoanza tarehe Mosi ya Agosti, ina asilimia 60 ya watoto wachanga wasionyonyesha, kwa sababu ya sera za kazi.

Shirika linataja faida za unyonyeshaji mama na mtoto, kwamba kunaimarisha afya ya akili katika maendeleo ya mtoto, kuwalinda dhidi ya magonjwa, hatari, unene, kupunguza gharama za huduma za watoto kuwalinda kinamama wanaonyonyesha, dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na matiti.

Unicef inasema, sera za kuunga mkono unyonyeshaji kama likizo yenye malipo kwa wazazi na malimbikizo ya kunyonyesha, hazipo kwa kinamama wengi duniani.

Mwaka jana, Unicef inasema wastani wa watoto wanne kati ya 10, walionyonyeshwa maziwa ya mama katika miezi sita ya mwanzo ya maisha yao, ni asilimia 41 ya watoto wote.

> "Kunyonyesha kwa muda mrefu, pia kunachangia afya na maisha bora ya mama, kwani humpunguzia hatari ya kupata saratani ya mfuko wa mayai ya uzazi na matiti, na watoto na vijana wadogo walionyonyeshwa wakiwa wachanga, wana uwezekano mdogo wa kua na uzito wa mwili wa kupindukia," ilifafanua taarifa ya shirika hilo

**KUNAKOONGOZA**

Nchi zinazoongoza kwa unyonyeshaji huo ni Rwanda, inaongoza asilimia 86.9; Burundi inafuatia kwa asilimia 82.3; Sri Lanka asilimia 82;Visiwa vya Solomoni, asilimia 76.2 na taifa la Vanuatu asilimia 72.6, pia inaonyesha watoto vijijini wana kiwango kikubwa cha kunyonyesha kuliko mjini.

Unicef inasema unyonyeshaji ni uwekezaji kuwa endapo kiwango cha juu cha unyonyeshaji kitafikiwa duniani kitapunguza gharama za huduma za afya duniani kwa Dola za Marekani Sh.bilioni 300, fedha ambazo zingetumika kwa mengine ya maendeleo.

Takwimu mpya za Unicef mwaka jana, inasema chini ya nusu ya watoto wote duniani, asilimia 43 ndio walionyonyeshwa katika saa ya kwanza ya uhai, baada ya kuzaliwa. Sera mpya ya Unicef iliyotangazwa mwaka huu kuhusu likizo ya uzazi, inapendekeza miezi sita ya likizo yenye malipo kwa wazazi, kati ya miezi 18 zinapaswa kutengewa kinamama.

Hivi sasa inapendekeza serikali na kampuni za biashara kutoa walau miezi tisa ya likizo kwa wazazi na katika utafiti wa karibuni, Unicef imebaini wanawake wanaopata likizo ya uzazi ya miezi sita au zaidi, ni takribani asilimia 30, wanaendelea na kunyonyesha maziwa ya mama pekee.

Shirika la Kazi Duniani (ILO), linasema angalau kuwapo likizo ya wiki 14 yenye malipo, huku nchi zikihimizwa kutoa wiki 18 pamoja na msaada kazini. Hadi sasa inasema, hadi sasa ni asilimia 12 ya nchi zote duniani zinazotoa likizo hiyo yenye malipo.

**WAZAZI**

Mkazi wa eneo la Qash, Juma Athuman, anashauri suala la wanawake kuwanyonyesha watoto wachanga iangaliwe, pia wanaume kupewa msukumo.

Ester Mkumbi, mkazi wa Babati, anasema wanaokataa kunyonyesha ni mabinti kwa dai 'chuchu zao zisianguke.'

Mratibu wa shirika la Bapace, Said Mnyaruge, anasema kinamama wanaoacha kunyonyesha watoto kwa kipindi kinachoshauriwa kitaalamu, wanawanyima watoto haki zao.

Mnyaruge anashauri wataalamu wa afya na lishe wawapatie elimu kinamama, warejee haja ya kunyonyesha watoto kwa kipindi kinachoshauriwa kitaalamu.

Mkazi wa Bashnet, Janeth Sanka, anasema wanawake wanaosuasua kunyonyesha, wengi wao ni wasiojipanga kuzaa, hivyo wanaona kunyonyesha ni kaa la moto kwao.

AFYA

# Mkunga asiyesomea: Nje ya wodi nimesaidia 1900; wodini 700

- Makubwa ya kumuokoa abiria daladala
- Aliposubiri kujifungua, alianzia kusaidia
- Katika ajira yupo, mtaani pia hajastaafu
- Aonyesha maajabu ya kunusuru mbuzi



Kundi la wanafunzi wa shule ya msingi, ambao Mkunga aliyewezesha kuzaliwa kwao ni Ziada Ngwere.

**Na Anthony Gervas**

"SIJAUSOMEA ukunga darasani, lakini nimeokoa maisha ya maelfu ya kinamama wajawazito kujifungua salama," anatamka Ziada Ngwere, mkunga mjuzi aina yake mwenye sifa ya kujituma, ingawa hana historia ya mafunzo rasmi, alipodokeza katika mazungumzo yake na Nipashe.

Anaendelea: "Taaluma hiyo nimeirithi kutoka kwa bibi yangu Mwasiti Titimo, niliyekuwa naishi naye kijiji cha Bolisa mkoani Dodoma, enzi hizo...."

"Nilikuwa napenda sana kuona watoto wachanga waliozaliwa. Nilikuwa nafurahia kumuona bibi yangu akiwazalisha kinamama nyumbani hapo. Mimi nilikuwa natamani kuwa mkunga, baadaye nikikua, ili niwasaidie kinamama kuwazalisha kama alivyokuwa akifanya bibi yangu," anasema Ziada.

Huyu ni mzaliwa wa mwaka 1969 mkoani Iringa katika mtaa wa Ilala, anayesema kuwa kazi ya ukunga amejifunza kutoka kwa bibi yake wakati akiishi naye Kondoa,Dodoma, lakini anasema anaipenda kazi hiyo tangu mdogo hajaanza hata shule akiwa na miaka sita.

> **"Nilikuwa napenda sana kuona watoto wachanga waliozaliwa. Nilikuwa nafurahia kumuona bibi yangu akiwazalisha kinamama nyumbani hapo. Mimi nilikuwa natamani kuwa mkunga, baadaye nikikua, ili niwasaidie kinamama kuwazalisha kama alivyokuwa akifanya bibi yangu," anasema Ziada.**

Anasema baadaye alihamia Dodoma na wakati akiishi na bibi yake, mwaka 1975 alichukuliwa na mama mzazi, Mariamu Hussein, wakaenda kuishi Masiwani mkoani Tanga, alikoanza darasa la kwanza mwaka 1976 katika Shule ya Msingi Kana. Wakati huo, mama yake aliafanya kazi katika Shirika la Uuzaji Mazao Nchi za Nje (Gapex)

Anasimulia mwaka 1980, mama yake alihamishiwa mkoani Iringa alikozaliwa, alikoendelea na masomo katika Shule ya Msingi Ilala, wakati huo akiwa darasa la tano na mwaka 1983 alihitimu darasa la saba shuleni hapo.

Ziada anasema alibahatika kufaulu na alijiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Lugalo mjini hapo, ambako alisoma hadi kidato cha nne.

**UKUNGA ULIPONOGA**


Anasimulia kwamba, wakati akisoma sekondari aliupenda sana ukunga, akajenga tabia na rafiki yake anayemtaja kwa jina la Emmanuela Lusinde, kila walipotoka shuleni jioni, walipitia ziliko wodini ya wazazi katika Hospitali ya Mkoa Iringa 'kuwasalimia' na kuwaona watoto wachanga waliozaliwa.

"Ilifikia hatua tukiingia wodini tukiwa na sare za shule, wauguzi wanatuuliza 'kila mara huwa mnakuja wodini kufuata nini?' Tukawaambia tunapenda kuja kuwasalimia wazazi na kuona watoto wachanga waliozaliwa, ndipo walipotuzoea tukaendelea kama kawaida. Ila mimi moyo wangu ulikuwa ukitamani baadaye niwe mkunga niwasaidie akinamama," anaeleza Ziada.

"Kazi ya ukunga mimi iko kwenye damu na sasa niliamua kuirithi kutoka kwa bibi yangu aliyefariki dunia mwaka 1978 akiwa nyumbani kwake wilayani Kondoa mkoani Dodoma. Lakini, wakati anafariki dunia, tayari nilikuwa nimeshajifunza kuzalisha kutoka kwake," anasimulia.

Ziada anaendelea kusema kuwa mwaka 1989 aliolewa na Abdallah Ibrahim, aliyekuwa mfanyakazi wa Shirika la Mbegu Tan Seed mkoani Arusha na baadaye mwaka 1993, walihamia mkoani Mwanza.

"Mwaka 1995 tukiwa Mwanza, nilianza shughuli za kijasiriamali za biashara ya kuuza nafaka za mazao, mchele, sukari na 'mama ntilie' katika soko la Pasiansi na baadaye 1997 ndipo nikaanza rasmi kazi ya ukunga," anasema.




Ziada Ngware, akiwa kazini.

Anasema, wakati huo anaanza ukunga, kilikuwa bado ni kijiji cha Nyamwilolelwa katika kata ya Bugogwa, Wilaya ya Nyamagana, kabla haijagawanywa ilivyo sasa na kuzaliwa Wilaya ya Ilemela.

Mahali hapo anakosimulia mwanzo wake, hivi sasa ni Kata ya Shibula, Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza.

Anasema, wakati anaanza kazi ya ukunga umeme haukuwapo na alifanya kazi ya uzalishaji wajawazito akitumia taa za koroboi na chemli.

KULIKONI MAARUFU?

Umaarufu huo hauna siri, pindi unapopita maeneo tofauti ya Mwanza na hususani Manispaa ya Ilemela, jina Mama Ibra, liko juu zaidi hata kufunika jina la Ziada Ngwere, katika kila kona; iwe kazini na mtaani kwake. Hilo liko bayana.

Wapo wanaodiriki kumtafsiri kwamba historia yake inatosha kumbebesha sifa ya kuupata uongozi wa kura za kishindo asubuhi tu, tena kwa kampeni ya kupunga mkono tu, japo mwenye anakiri kwa sasa hana nia ya kuwania nafasi yoyote.

Kwanini hivyo? Ziada ana majibu yake yatokanayo na simulizi mkasa wa aina yake. Anakumbuka mwaka 1997, akiwa katika kata hiyo - Shibula mama mjamzito mtaani kwake, alikabiliwa na uchungu wa uzazi usiku wa manane na hakuwa na uwezo wa kwenda kujifungua katika Hospitali ya Mkoa ya Sekou Toure.

Wakati huo, kutokana umbali uliopo wa kilomita tano na ukosefu wa usafiri, watu wakitumia baiskeli ndani ya miundombinu yenye hali mbaya, ulikuwa mtihani mkubwa kufika hospitalini hapo, tena katika mazingira ya dharura kama hayo.

Anasimulia mkasa ulivyokuwa, ndugu na viongozi wa serikali akiwamo Diwani, Bwana Afya na Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Nyamwilolelwa, walimfuata kumsihi mkunga huyo wa jadi awasaidie kumzalisha mama huyo ikiwa jitihada za kunusuru maisha ya mama na mtoto. Alikubali na kufanikisha lengo. Ziada anaendeleza simulizi ya mafunzo ya msingi, kwamba hatolisahau shirika lisilo la kiserikali la Hesawa lililojishughulisha na miradi ya afya, mazingira na maji, mwaka 2000 lilimuwezesha kupata mafunzo ya uzazi kwa mama na mtoto.

Pia, anaitaja Plan International, iliyomuwezesha kupata mafunzo ya matunzo ya mama na mtoto majumbani

Nini alilolivuna kitaaluma? Hapo tena ana majibu kwamba, tangu aanze ukunga mwaka 1997, ameshawasaidia kinamama 1940 waliojifungulia mtaani na wale wa hospitali ambako aliajiriwa tangu mwaka 2011, jumla yao 700.

Kwa mujibu wa Ziada, hata baada ya kuajiriwa ameendelea kutoa huduma zake kwa wajawazito wahitaji wa mtaani hadi sasa.

Ziada anasema, katika jitihada zake za ukunga, alimhuhudumia mjamzito kujifungua mtaani kwake, ambaye alipewa rufani kutoka Kituo cha Afya Karume, akielekea Hospitali ya Sekou Toure jijini Mwanza.

Anakumbuka akiwa Mtaa wa Buganda mwaka 2010, mjamzito alishushwa kwenye daladala baada ya kuzidiwa na uchungu umma ulifika, wakiwamo kinamama waliomzingira kuhudumia kando ya barabara.

Miongoni mwao alikuwa Ziada, ambaye alifuatwa nyumbani na kubeba jukumu mara moja lililomuwezesha mzazi huyo kujifungua salama na baada ya hapo alimchukua kwenda naye kumpumzisha nyumbani, kisha alimrushu aondoke.

Mbali tu na kupaisha umaarufu wake kupita kiasi, ikiwamo kutangazwa katika vyombo vya habari, Ziada anasema ni tendo lililowashtua viongozi wa kiserikali wa mtaani kwake na Manispaa ya Ilemela, waliomvamia ghafla nyumbani kwake siku iliyofuata, wakitaka kujua kulikoni hilo la kumsaidia mtu kujifungua barabarani kinyume na sheria na taratibu?

Ziada anasema, baada ya ufafanuzi wake uliowashangaza na kugueza udadisi wao wa kisheria, walimshukuru na kumpongeza, kulikoendana na walichomuahidi kwa kauli "Ahsante mama! Utaona shukrani yetu..."

Anaendelea kusimulia, mwaka uliofuata, mwezi Januari, alipatiwa barua ya ajira na muda mfupi baadaye aliripoti mahali aliko sasa.

Leo hii, Ziada Ngwere ni mkazi wa mtaa wa Buganda-Igombe katika Kata ya Shibula, wilayani Ilemela akitumikia katika Kituo cha Afya Karume, ambako makali ya uchapa kazi wake yako bayana.

INAENDELEA UK.18

## Namna CCBRT inavyokabili tatizo la mdomo sungura




Hali halisi ya matibabu ya mdomo sungura, kupitia Hospitali ya CCBRT. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

**Na Yasmine Protace**

DAKTARI bingwa wa mifupa kutoka hospitali ya CCBRT, Zainabu Ilongo, anasema ni Siku ya Tabasamu inayofanyika katika nchi 90 ikiwamo Tanzania, inanafasi yake maalum kiafya.

Hapo anaitafsiri vita rasmi ya kukabili maradhi ya mdomo wazi au kwa jina lingine mdomo sungura, katika vyanzo vyake kuna baadhi ya yanayohisiwa kuwa ni mama kuvuta sigara, ugonjwa wa kisukari na unene wakati wa ujauzito, vinahisiwa kusababisha mtoto kuzaliwa mdomo wazi.

Dk. Ilongo anasema, tafiti zilizofanyika hazijaweza kueleza tatizo gani linachangia mtoto kuwapo mdomo wazi na anafafanua mtoto aliyezaliwa mdomo wazi, ukuaji wake ni dhoofu na hawezi kunyonya vizuri.

Pia, anafafanua watoto wenye tatizo hilo, ni muhimu kufanyiwa upasuaji wakiwa na umri wa miezi sita au zaidi na kuendelea.

Anasema, kwa kushirikiana na shirika la Smile Train, wanatoa huduma isiyo na malipo kwa ajili ya kuwezesha kufanya kwa huduma za Mdomo Sungura.

Daktari huyo anasema mwaka 1998, walianza kuwahudumia watoto zaidi ya milioni moja mpaka sasa, ambao walikuwa na tatizo la mdomo sungura.

"Tabasamu ni kitu muhimu sana kama kutakuwa na hitilafu katika mdomo, watoto wanapata shida katika kula, kupumua na wengine kukosa marafiki," anasema.

Anafafanua kwamba, kati ya watoto milioni saba wanaozaliwa duniani kila mwaka, watoto 700,000 wanaozaliwa duniani wana shida ya mdomo wazi.

Daktari Ilongo anasema tatizo la mdomo wazi au mdomo sungura kwa mtoto au mtu mzima, matibabu yake yanapatikana vizuri na kurudi katika hali yao.

Anasema, tafiti zilizofanyika hazijaweza kueleza tatizo gani linachangia mtoto kuwapo mdomo wazi na kuingeza kuwa CCBRT ina mabalozi zaidi ya 500 nchini, wanafuatilia na kuwatafuta watoto ili wakafanyiwe vipimo.

Katika hatua hiyo, anawaasa wazazi wawapeleke watoto na watu wazima CCBRT, ili wapatiwe matibabu bure.

Neema Ally, ni mama wa mtoto Selemani Abdully, anayesimulia mdomo wazi kwa mtoto wake, ilianza baada ya kujifungua siku nne ndipo alipogundua kuwa mtoto wake ana tatizo mdomo wazi.

Anasema baadhi ya watu walimwelekeza kwenda CCBRT na alifanya hivyo, sasa ameshafanyiwa upasuaji.

Pia, mkazi mwananchi mwigine anayejitambulisha, Mama Evelyn Christopher, aliyekuwa na mtoto aliyezaliwa akiwa mdomo wazi na alipopata taarifa za CCBRT, alimfikisha huko na anakiri sasa mtoto anaendelea vizuri.

Anaitamkia jamii iache kuwanyanyapaa watoto wakiwa na changamoto za kiafya na kinachotakiwa ni kuwasaidia warudi katika hali nzuri.

Mwingine ni Mama Amina Juma, wa jijini Dar es Salaam, anayesema watoto wasitengwe na ndugu kutokana na matatizo ya mdomo, bali waende CCBRT ambako yanatolewa bure na yamewsaidia watoto wengi.

Mwisho

caption

AFYA

INATOKA UK.17

# Mkunga asiyesomea: Nje ya wodi nimesaidia 1900; wodini 700

Pia, katika mazungumzo yake hafichi hisia zake kuipongeza serikali katika namna inavyojituma katika kuboresha utitiri wa huduma za hospitali, vituo vya afya na zahanati kila mahali nchini.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Karume, Dk. Samiah Nuru, anasema Mkunga Ziada ni mahiri katika kazi yake kwa kushirikiana na wauguzi na madaktari akiwa mhudumu wa afya kituoni hapo.

"Ukweli, Ziada Ngwere ni mchapa kazi anayeshirikiana na wauguzi na madaktari, hana kinyongo, ni mtu asiye na makuu katika kufanya kazi," anakiri Dk. Nuru.

Ifuautayo ni mazungumzo ya maswali na majibu kati ya Mkunga Ziada na mwandishi wa makala hii, walipokuwa katika Manispaa ya Ilemela siku chache zilizopita. Fuatilia maswali na majibu:

***Swali: Nini umahiri wako katika kazi ya ukunga?***

**Jibu:** Umahiri wangu katika kazi ya ukunga ni kwamba naipenda sana na kuithamini, iko kwenye damu. Ndiyo maana imanipa umaarufu mkubwa hadi serikali ikanitambua na kuniajiri katika Kituo cha afya cha Karume Kata ya Shibula Wilaya ya Ilemela, baada ya kuona kazi zangu nzuri za kuwasaidia kinamama wajawazito kuokoa maisha yao, ukunga ndiyo umenifikisha hapa.

***Swali: Je? Kwa vile umeajiriwa na serikali, kazi ya ukunga mtaani umeiacha?***

**Jibu:** Hapana. Pamoja na kuajiriwa na serikali, lakini bado naendelea kutoa huduma hiyo nyumbani kama kawaida. Nikiwa siko kazini au ikitokea usiku mtu hajiwezi kufika kwenye kituo cha afya, kwa sababu kazi ya ukunga iko kwenye damu, namsaidia.

Nitaacha baada ya kustaafu serikalini, nitapumzika. Nahudumia bure bila malipo na wengine huniletea wenyewe zawadi kama ahsante.

***Swali: Tofauti ya ukunga kabla na baada ya kuajiriwa ni nini?***

**Jibu:** Kinamama kwa sasa wamekuwa wakilazimika kunifuata katika Kituo cha afya Karume. Wakati nikiwa kazini wakati wa kujifungua wanaohitaji kuwasaidia, lakini licha ya hivyo, wauguzi wenzangu na madaktari wanatoa huduma vizuri kwa kinamama wajawazito na wagonjwa wengine na tunashirikiana pamoja wakati wa kutoa huduma.

Pia, baada ya kuajiriwa nimejifunza mengi na kupata ujuzi zaidi juu ya kutoa huduma za afya kwa kinamama wajawazito na kufanya usafi wa mazingira na maisha yangu kwa sasa yamebadilika baada ya kupata ajira, angalau yamekuwa mazuri ukilinganisha na zamani na umaarufu wangu kwa sasa umeongezeka zaidi .

Kutokana na mabadiliko ya maisha yangu, hivi sasa naishi na watoto wenye maisha duni waliokuwa wakiishi chini ya uangalizi wa msikiti waliokuwa mkoani Kagera, ambao ninawasomesha. Ni Shakra Athuman (miaka saba) anayesoma darasa la kwanza na Mwanaidi Jamal(14) , anayesoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Mhonze.



Mwanafunzi aliyezaliwa kwa msaada wa Ziada Ngwere, katika mahafali ya kidato cha nne, anayenuia kuwa mwanajeshi.

> "Mwaka 1995 tukiwa Mwanza, nilianza shughuli za kijasiriamali za biashara ya kuuza nafaka za mazao, mchele, sukari na 'mama ntilie' katika soko la Pasiansi na baadaye 1997 ndipo nikaanza rasmi kazi ya ukunga," anasema.

***Swali: Unajua kilichosababisha zaidi kupata ajira serikalini?***

**Jibu:** Kwanza, niseme kwamba Mungu hufanya njia pasipo na njia, nakumbuka ilikuwa mwaka 2010 alitokea mama mmoja mjamzito akiumwa uchungu kabla sijaajiriwa serikalini, ambaye alikuwa akitokea katika Kituo cha Afya Karume, ambacho sasa nafanyia kazi, aliyekuwa amepewa rufani ya kwenda kujifungua Sekou Toure.

Wakati akiwa njiani kwenye daladala kuelekea hospitali, alizidiwa uchungu na abiria kulazimika kumsaidia kumshusha chini pembeni mwa barabarani, ili apate msaada zaidi.

Ilikuwa karibu na mtaa ninaoishi na wasamaria mwema wakanifuata kuniomba msaada wa kumsaidia na nilimsaidia akajifungua salama pembeni mwa barabara, wakinisaidia wanawake wenzangu.

Sasa 'Mungu si Athumani' walitokea waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali, ambao walifika na kushuhudia tukio hilo wakiwa na viongozi wa serikali, baada ya kumaliza kutoa huduma hiyo kwa mama huyo, walinihoji wakachukua habari zangu na kwenda kuzitangaza.

Hivyo, viongozi wa serikali (siku iliyofuata) walifika nyumbani kwangu baadaye waliniambia wakati wa kuondoka kwamba 'nitaiona shukrani yao' kisha wakaondoka.

Siku moja nikiwa nyumbani kwangu majira ya saa tatu usiku, alikuja mwalimu mmoja akanipa barua ya ajira yangu iliyokuwa imetokea wizarani. Hivyo kesho yake, nilienda kwa Ofisa Utumishi wa Jiji, ambako pia nilikutana na barua nyingine ya ajira iliyokuwa imetolewa niwe mhudumu wa kutunza faili za ofisini.

Lakini, baadaye ofisa huyo baada ya kumweleza alinishauri nikafanye kazi kwenye kituo hicho cha afya kwa lengo la kusaidia watu, ndipo nilipokubali na kurudi nyumbani na baadaye nilianza kazi.

***Swali: Umejipangaje na elimu zaidi?***

**Jibu:** Siwezi kuendelea tena kusoma, kutokana na majukumu mengi ya kifamilia, maisha na umri, labda kupata mafunzo ya muda mfupi tu au semina.

***Swali: Jamii inakupokeaje katika utendaji kazi wako na mwajiri?***

**Jibu:** Jamii inanikubali utendaji kazi wangu na inataka niendelee kuwasaidia kinamama. Inanipenda mtaani jina langu maarufu huitwa 'Mama Ibra' kila kona, lakini hata kazini wananikubali nachapa kazi kwa kushirikiana na wauguzi na madaktari.

***Swali:Je, watoto uliowahudumia wanakupokeaje na familia zao?***

**Jibu:** Watoto ambao wanatambua kwamba wamezaliwa na wazazi wao kutokana na huduma zangu, wananifurahia wakiniona kila kona huniita 'Mama Ibra' kwa sababu wengi wanasoma shule za msingi, sekondari,vyuo hadi vyuo vikuu na wengine wanafanya shughuli zao za kijasiriamali.

***Swali: Je, wewe kama mzazi pia ulikuwa ukipata ujauzito, ilikuwaje wakati wa kujifungua?***

**Jibu:** Swali zuri. Kwanza niseme 'mganga hajigangi' ni msemo unaofahamika. Mimi ninapopatwa na jambo hilo, huenda kujifungulia katika Hospitali ya Kanda ya Rufani Bugando na ninahudumiwa vizuri tu na mwaka 2004 nilipata operesheni ya kujifungua.

Vilevile mwaka 1998 nilienda Bugando kujifungua nikiwa wodini, alikuwamo mama mmoja ambaye aliumwa uchungu wa kujifungua, lakini wauguzi walikuwa mbali, hivyo nililazimika kumsaidia na walipokuja, walikuta tayari amejifungua wakashangaa.

***Swali: Kitu gani usichokipenda na kipi unachopenda katika fani yako?***

**Jibu:** Kitu ambacho sikipendi katika kazi yangu, ni pale inapotokea muuguzi anahangaika kuokoa maisha ya mama mjamzito wakati wa kujifungua, kutokana na mjamzito kuwa ametumia dawa chungu za kienyeji kabla ya kujifungua, ambazo wakati mwingine husababisha 'uhatari' wa mama na mtoto kupoteza maisha, hivyo baadaye muuguzi hulaumiwa.

Lakini wakati mwingine wanapotumia dawa hizo za miti shamba, husababisha hata mimba kutoka au mfuko wa uzazi kuweza kupasuka na kutokwa damu nyingi au kuzaliwa mtoto akiwa amefia tumboni.

Kitu ninachokipenda katika fani yangu ni kuwasaidia kinamama wajawazito na wagonjwa wengine, bila ya kuwabagua na kuwapa elimu ya kuachana na matumizi ya dawa hizo wajawazito na kwenda hospitali.

***Swali: Tukio lipi limekufurahisha ama kukuudhi katika kazi ya ukunga?***

**Jibu:** Tukio linalonifurahisha katika kazi ya ukunga ni kuona wale watoto waliozaliwa kupitia huduma yangu wakiwa na afya njema wengine wako shule za msingi, sekondari na wengine vyuo vikuu.

***Swali: Changamoto zipi ulizokumbana nazo katika ukunga?***

**Jibu:** Wakati naanza sikuwa na vifaa vya kuzalishia na sehemu ya kuzalisha, pamoja na kitanda cha kumlaza mama mjamzito wakati wa kujifungua.

- ***Endelea na sehemu nyingine Alhamis wiki ijayo.***

***Mwandishi anapatikana kwa baruapepe: anthonygervas@yahoo.com na simu: (+255) 0682 869244***



Mkunga, Ziada Ngwere nje ya nyumbani kwake, jijini Mwanza.
**PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

AFYA

# Madhara matatu anayopata mtoto pindi inapotokea ajali

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAKATI unaendesha gari huku mtoto wako akiwa amekaa pembeni, umewahi kufikiria madhara yanayoweza kumpata pindi gari litakaposimama, ghafla au kupata ajali?

Magonjwa ya akili ulemavu na kifo ni miongoni mwa madhara makubwa, yanayompata mtoto inapotokea hali hiyo.

Imekuwa kawaida kwa wazazi na walezi kufunga mikanda wa wapo kwenye gari inayowasaidia, kujikinga pindi ajali inapotokea.

Lakini, kwa mtoto hali ikoje? Hili ni swali ambalo halipewi nafasi kwenye fikra za watu huku wengine wakiwaweka kwenye viti vya mbele, bila ya kujali usalama wao.

Vizuizi vya watoto ni viti maalum vyenye mikanda mahsusi ya kumlinda mtoto na vimetengenezwa kulingana na uzito, urefu na umri wa mtoto.

Mtoto anayepaswa kukaa kwenye kiti cha kawaida kwenye gari ni yule anayeanzia miaka 10 na kuendelea na chini ya miaka hiyo, anapaswa kutumia kizuizi awapo kwenye gari.

Licha ya umuhimu wa viti hivyo kwenye magari, Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, haijaweka wazi kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa kumlinda mtoto dhidi ya hatari inayoweza kutokea kwenye gari.




Watoto wakipatiwa elimu ya barabarani. **PICHA: MTANDAO.**

### DAKTARI BINGWA

Daktari bingwa wa magonjwa ya dharura ikiwamo ajali katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. George Dilunga, anasema pindi mtoto anapopata ajali kuna madhara makubwa matatu anayoyapata.

Anasema, madhara hayo ni magonjwa ya akili, ulemavu na kifo kutokana na kutofunga mkanda au kufungwa mkanda ambao sio wa rika lake.

Daktari huyo anasema, kumekuwa na tabia ya wazazi kuwafunga mikanda watoto ambayo hailingani na mwili na umri wao na hivyo ajali inapotokea mtoto anapata madhara hayo.

"Kuna risk kwanza ya kuumizwa na mkanda kama akifungwa mkanda wa mtu mzima anaweza kupata majeraha yanayosababishwa na mkanda kwa sababu sio 'standard' (kipimo) yake wala saizi yake, anaweza kuumizwa maeneo ya shingoni, usoni au tumboni," anasema.

Anabainisha kwamba, kama mtoto akiwa hajawekwa kwenye kiti chake maalum, anaweza kutupwa nje ya gari pindi ajali inapotokea na kumsababishia madhara.

"Akitupwa, anaweza kuumia au hata kufa na akipona anaweza kupata ulemavu au ugonjwa wa akili," anasema.

> **"Kuwapo sheria itakayomshurutisha mtu ili pale askari wa usalama barabarani anaposimamisha gari na kukuta mtoto amekalishwa kiti cha mbele wakati umri wake wa kuwa kwenye kiti maalum achukuliwe hatua kama wanavyofanya wenzetu wenye sheria ya vizuizi vya watoto," anasema.**

### USHAURI

Anashauri elimu itolewe kwa jamii kupata uelewa wa matumizi ya viti maalum vya watoto na kutambua umuhimu wake.

"Tunashauri watu wenye magari ni vyema wakawa na viti vya watoto vinasaidia kuwazuia kupata madhara makubwa pindi ajali inapotokea na ahakikishe anakitumia maana wengine wanavyo lakini wanawaweka watoto siti za mbele,"anasema.

Pamoja na hayo, anasema kuna umuhimu wa kuwa na sheria inayolazimisha matumizi ya viti maalum kwa watoto.

"Kuwapo sheria itakayomshurutisha mtu ili pale askari wa usalama barabarani anaposimamisha gari na kukuta mtoto amekalishwa kiti cha mbele wakati umri wake wa kuwa kwenye kiti maalum achukuliwe hatua kama wanavyofanya wenzetu wenye sheria ya vizuizi vya watoto," anasema.

### HAWAWAJUI WATOTO

Mkazi wa Nkuhungu, Jacqueline Victor, anasema yeye hafahamu kuhusu matumizi ya vizuizi vya watoto na amekuwa akiona kwenye mitandao kama vile matumizi hayo ni ufahari.

"Kwa kweli mimi hata sifahamu matumizi ya vizuizi vya watoto naona kama wanaotumia wanaiga wazungu," anasema.

Mkazi wa Uhindini, Shafte Ally, anasema teknolojia ya kuweka vizuizi vya watoto imechelewa kufika Tanzania na wachache ndio wenye mwamko wa kutumia.

"Kuna mtu anajiuliza ninunue kiti cha mtoto cha nini? Kwanza kinauzwa bei kubwa na inategemea umri wa mtoto, mimi sioni hata umuhimu wa kutumia naona mambo ya wazungu," anasema.

### KAULI YA TBS

Ofisa Viwango Mwandamizi wa Shirika la Viwango nchini (TBS), Yona Afrika, anasema shirika hilo lina mpango wa kuweka kiwango cha ubora kinachotakiwa kwenye vizuizi hivyo vya watoto vinavyowakinga wasipate madhara makubwa pindi wanapopata ajali.

Anasema, kwa sasa hakuna kiwango kwenye bidhaa hiyo nchini, lakini wameona kuna umuhimu ili kuwaweka watoto salama.

"Mpango wa kuwa na viwango kwenye vizuizi vya watoto tunatarajia kufanya mwaka ujao wa fedha," anasema.

### USALAMA BARABARANI

Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Kikosi cha Polisi Usalama Barabarani, Deus Sokoni, anasema ripoti ya jeshi la polisi ya mwaka 2018 inaonyesha kuwa kwa wastani, watoto wawili hufariki dunia kwa mwezi huku wengine wanne, anasema kutokana na ajali za barabarani, sababu ya madhara hayo ni kutotumia vizuizi vya watoto.

Anasema katika ripoti hiyo inaonesha mwaka huo watoto wenye umri kati ya miaka saba hadi 12, 21 walifariki na 48 walijeruhiwa kutokana na ajali hizo.

"Kati ya waliokufa, 12 walikuwa wanawake na wanaume 9, wakati wale waliojeruhiwa ni pamoja na wanaume 32 na wengine 16 walikuwa wanawake, "anasema Sokoni.

Sokoni anabaini kuwa sheria ya Usalama barabarani ya mwaka 1973, iko kimya kwenye viti vya gari vya watoto, hivyo kusababisha watu wasiwajibike kuwa navyo.

### RIPOTI WHO

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani(WHO), kuhusu usalama barabarani ya mwaka 2018, inabainisha nchi 84 kati ya 175 zina sheria ya vizuizi vya watoto. Tanzania, haina sheria hiyo.

Taarifa hiyo ya WHO, inaeleza nchi 33 kati ya 175 ndio zenye sheria nzuri ya vizuizi vya watoto huku nchi 41 pekee zinazungumzia kwenye sheria zao mtoto anayetakiwa kutumia kiti hicho angalau awe na umri usiozidi miaka 10.

Pia, Nchi 52 kati ya 175 ndio zinataja kiwango kinachotakiwa kwenye vizuizi, huku nchi 114 zikiainisha ni mtoto wa umri au urefu gani anatakiwa kukaa kiti cha mbele ambapo Tanzania haipo.

Inaeleza watoto wenye umri kati ya miaka mitano hadi 14 na vijana wenye umri ya miaka miaka 15 hadi 29, ndio majeruhi wakubwa wa ajali za barabarani na kusababisha vifo vyao.

Taarifa ya WHO inakadiria kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka wa 2018, takribani watoto 82,000 kati ya miaka mitano hadi 14, walifariki kwa ajali za barabarani.

Aidha, ripoti hiyo inasema mtoto akiwekwa katika kizuizi kwa usahihi anaweza kupunguza madhara ya ajali kwa asilimia 70 ambao kwa watoto wachanga ni asilimia 54 hadi 80 kwa watoto wadogo.




Mazoezi ya kulinda afya yakiendelea.

# Fahamu tofauti za maumbile katika kumudu shinikizo damu

**Na Michael Eneza**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetangaza hivi karibuni nia ya kuzindua mpango wa kufanya kampeni ya uelimishaji kuhusu magojwa yasiyo ya kuambukizwa nchini, kutokana na kuongezeka vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukizwa.

Hali hiyo inajitokeza zaidi katika miaka ya karibuni, ambako idadi ya vifo vinavyotokana na magonjwa yanayoenea kwa kasi kama malaria na ukimwi vimepungua na badala yake vinaongezeka vifo vinavyotokana na mfumo wa maisha ya kisasa.

Uwezo wa kumudu maisha unaubebesha mwili kazi ngumu ya kuchuja na kuondoa usichohitaji na unajaza akiba kama ya mafuta na sukari.

Wakati vyombo vya habari vinaanza kutafakari tangazo hilo la serikali, wafanyakazi wa maeneo tofauti wanafahamu jinsi inavyotokea na hata kujikuta msibani katika muda mfupi, hata kabla ya hapo alikuwa ofisini anachapa kazi.

Ni hali inayotokea mara nyingi hata haihitaji kutaja vielelezo, kwani vinakuja kichwani mtu yeyote akianza kufikiria, iwe sehemu za ajira au biashara.

Suala ni kuwa awe mtu ambaye mnaonana kila wakati, unakumbuka fika mara ya mwisho alikuwa buheri wa afya, afe ghafla tu.

Ni vifo vinavyoleta mshituko na misononeko ya kina, kwani ni tofauti na mazingira ambayo mtu anakuwa mgonjwa wa muda mrefu.

Iwapo kifo kinatokea, mtu anaweza walau kujiridhisha kwamba huenda jitihada zilikwama, lakini mtu akiugua kwa siku moja au mbili na akafa, inakuwa vigumu kuamini.

Kifo cha aina hiyo ni kielelezo cha janga la magonjwa yasiyoambukiza, kwa maana ni vigumu sana kuoanisha mahitaji ya maisha bora, ambayo kila mmoja anapigania kuupata, kuacha uzembe asilia mwilini kujilinda na mtu anapofanikiwa kupata maisha bora.

Mlo unaojitosheleza ni muhimu, lakini mtu asipate tabu zaidi na kujinyima mlo sahihi, pia inaaswa mwili usipate raha zaidi kujaza akiba ya mafuta na sukari, vikaleta madhara.

kunaelezwa ahueni ya madhara hayatokei kwa kila anayeishi kwa raha kiwango fulani, kwa sababu kuna vianzishi tofauti, hivyo baadhi wanaponea.

Moja ya mshangao kuhusu mwili, ni dhana ya kuchapa kazi. Mara nyingi mwili unafuata kanuni za baiolojia ilivyo.

Mwili unaweza kuharibiwa kisaikolojia na mwisho ubongo ukashindwa kufanya kazi, kitu ambacho katika maisha kinatokea katika sura ya mzaha. Kwa mfano, kinachoitwa 'Chinese Water Torture,' yaani mateso ya Kichina kutumia maji.

Kisayansi kudondokewa na tone la maji katika paji la uso labda kunaweza kuleta karaha ya kulowa kiasi fulani baada ya muda na siyo madhara ya ngozi, kichwa au ubongo, lakini ndicho hasa kinatokea kisaikolojia.

Siyo rahisi kueleza ugonjwa wa kudondokewa na tone la maji. lakini hali hiyo inapoendelea, inazaa kuchanganyikiwa, kupiga mayowe na shinikizo la damu.

Wataalamu wanasema, msingi wa shinikizo la damu ni kubadilika mishipa ya damu kutokuwa rahisi kupinda, kutanuka.

Ikiwa laini, damu inapita bila vizuizi kupeleka lishe na hewa ya oksijeni kwenye viungo muhimu na misuli mwilini. Endapo presha inaongezeka, kuna athari kadhaa. Kwa mfano, kuzibwa mishipa midogo kunazuia damu kupita kwa urahisi, hali inayoweza kuunda vifundo vya mafuta katika damu, kisha kupita kwa urahisi kutoa lishe inakotakiwa. Presha inaweza kuchana kifundo.

Wakati hali hiyo inajijenga mwilini, mtu anaweza kuwa na uchovu wa kiasi fulani, lakini akafanya shughuli zake kama kawaida.

Inashauriwa anayepaswa kufika katika kituo cha afya au zahanati kupata ushauri kutokana na uchovu wa hapa na pale. Unakuta mara moja daktari anashangaa 'umefikaje hapa, ulileta na gari?'

Hali ya kushangaza kimaumbile kwa mtu ambaye msukumo wa damu ukipungua au kupanda, inamwathiri kwa haraka na ni dhaifu kuliko mwingine ambaye anachukua muda mrefu zaidi kusikia tofauti hiyo mwilini.

Kwa sababu hiyo, udhaifu una maana mtu atatafuta ushauri wa daktari kwa haraka zaidi, kuliko ambaye anamudu shinikizo la ziada, bila ya kujisikia vibaya.

Mazingira ya pili ya shinikizo, hufikia pagumu bila ya kutazamia. Ndiyo maana, katika maisha na katika kumudu magonjwa, au raha na tabu za maisha, kila mtu ana aina fulani ya mchanganuo wa 'mema na mabaya' anaouweza tofauti na mwingine.

Cha kushangaza, hutokea hata watu wawili wanaofanana kimaumbile, wanaweza kukutanishwa na kuunda familia na vinasaba vyao vya lishe na athari zake vinafanana.

Ndiyo maana kampeni za magonjwa yasiyoambukizwa huwa ni ngumu kuziendesha na daima hakuna sayansi ya jumla ya kuenea au mfumo wa magonjwa.



Mgonjwa wa moyo akilalamikia afya yake. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



# Maiti zatupwa ndani ya makaro majitaka

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

BAADHI ya watu wasiofahamika wanadaiwa kutupa miili pamoja na nguo chakavu katika miundombinu ya majitaka inayomilikiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA).

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Mamlaka, Ndele Mengo, wakati wa kikao cha watendaji wa Mbeya- WSSA na maofisa watendaji wa kata na mitaa yote ya Jiji la Mbeya kilicholenga kujadiliana kuhusu matumizi ya mabaya ya miundombinu hiyo.

"Watu wamekuwa wakilalamika kuwa chemba (makaro) zinavuja maji taka, lakini tukizibua ili kufanyia usafi tunakuta kuna miili ya watoto, watu wazima pamoja na nguo chakavu vitu ambavyo ni hatari hata kwetu," alisema Mengo.

Alisema vitu hivyo ambavyo havitakiwi kutupwa maeneo hayo vinasababisha kuziba kwa mabomba na kusababisha chemba (makaro) kuvuja na majitaka kusambaa kwenye makazi ya watu.

Alieleza kuwa wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi kwa njia mbalimbali, lakini bado vitendo hivyo vinaendelea kufanyika.

Aliwaambia kuwa inakuwa changamoto kubwa pia kwa mamlaka hiyo wakati wa kurekebisha miundombinu hiyo iliyojaa taka za miili ya binadamu.

Aliwataka wananchi kuepuka kutumia vitu vigumu kwenye miundombinu ya vyoo yakiwamo mawe, nguo na magunzi ambavyo alidai haviyeyuki na haviozi hivyo kuziba miundombinu hiyo na kusababisha kero kubwa.

Aliwaomba wananchi kuzichoma moto nguo hasa za ndani zilizochakaa au kuzitupa kwenye majalala badala ya kuzitumbukiza kwenye vyoo na kusababisha kuziba kwa mitaro.

Vilevile aliwaomba maofisa watendaji wa kata na mitaa kushirikiana na mamlaka hiyo kutoa elimu na kuwafichua wanaotupa vitu ambavyo havistahili kwenye miundombinu hiyo.

Nao baadhi ya maofisa watendaji waliitaka mamlaka hiyo kuchukua hatua za haraka pale wanapopata taarifa za kuwapo kwa chemba za maji taka zinazovuja ili zisilete madhara kwa wananchi hasa wa mabondeni.

Mmoja wa maofisa hao, Upendo Mtenzi ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mbalizi Road, alisema chemba hizo zinavuja na kuchanganyika na maji yanayotumiwa na wakazi wa mabondeni, kuhatarisha afya zao.

Alizitaja baadhi ya chemba zinazoleta kero kubwa kwa wananchi kuwa ni ya Mabatini pamoja na iliyopo jirani na kitengo cha kutuliza ghasia.

"Kuna hatari wananchi wakapata magojwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na magojwa ya tumbo, sasa tunawaomba mkipata taarifa mjitahidi kuwahi kushughulikia ili kuepusha shida hizo," alisema.

Aliongeza kuwa makaro ya Mabatini ni kero kwa sababu ni eneo la wanafunzi.

Mwenyekiti wa maofisa watendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Jumanne Mwasenga, alisema wataendelea kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya miundombinu ya majitaka ili kuepusha changamoto za kuziba kwa miundombinu. Vilevile alisema wataendelea kuikumbusha mamlaka ya maji kutekeleza wajibu wake ili kuwaondolea kero wananchi na kwamba watawahamasisha pia kulipa gharama za huduma za maji.



Waendesha Bajaj wakiwa wameegesha vyombo vyao nje ya ukumbi wa Mkapa, jana jijini Mbeya, walipofanya kikao na Jeshi la Polisi kuhusu mambo mbalimbali yakiwamo ya usalama barabarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Madereva Bajaj sasa kushtakiwa

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, limewatahadharisha madereva wa Bajaj wanaokiuka sheria za usalama barabarani kuwa litaanza kuwashtaki mahakamani.

Akizungumza na madereva hao jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema wameamua kuacha kuwatoza faini madereva hao wanaokiuka sheria na badala yake wanawapeleka mahakamani.Aliyataja baadhi ya makosa ya madereva wa bajaji ambayo yamekithiri kuwa ni kubeba abiria zaidi ya watatu, kuendesha bajaji bila leseni pamoja na kubeba mafuta ya petroli ndani ya vyombo hivyo licha ya kwamba wana abiria.

Kamanda Matei alisema mengine ni kuweka ngao kwenye bajaji hizo ambazo zinasababisha uharibifu wa vyombo vingine vya moto ikiwamo magari na pikipiki na hivyo akawaagiza kuziondoa kabla msako haujaanza.

"Mkuu wetu wa mkoa alikagua na kubaini kuwa zaidi ya asilimia 50 ya madereva wa bajaji hawana leseni, sasa ametuonyesha njia. Naomba kila anayeendesha vyombo hivi awe na leseni kabla hatujaanza msako," alisema Kamanda.

Vilevile alisema wamebaini kuwa baadhi ya madereva wa bajaji ni wadogo umri ambao hauwaruhusu kufanya kazi hiyo, hivyo akawatahadharisha wamiliki wa vyombo hivyo kuwa watachukuliwa hatua wao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bajaji wa Jiji la Mbeya, Iddy Ramadhani, aliliomba Jeshi la Polisi kuendelea kushirikiana nao kupambana na matukio ya uhalifu likiwamo wizi wa vyombo hivyo.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakiiba bajaji katika maeneo mbalimbali nchini na kuzipeleka jijini Mbeya, kufanyia kazi ama kuziuza mkoani humo na hivyo kusababisha changamoto kubwa ya kiuhalifu.

# Halmashauri zote kuwa na barabara

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

UJENZI wa barabara zote za halmashauri zote za mkoa wa Mbeya unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa baada ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), kusaini mikataba 43 na makandarasi watakaofanya kazi hiyo.

Mikataba hiyo yenye thamani ya Shilingi bilioni saba, ilisainiwa jana jijini Mbeya mbele ya Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila na makandarasi hao wakatakiwa kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Chalamila aliwaonya makandarasi hao wasifanye kazi chini ya kiwango kwa maelezo yake athari zake ni kubwa kwao na jamii.

Alisema ujenzi wa madaraja unatakiwa kufanyika kitaalamu na kwa umakini mkubwa ili kuepuka maafa kama yaliyotokea hivi karibuni jijini Mbeya baada ya daraja la Mto Simba kusombwa na mafuriko na kuua watano.

"Tambueni kwamba tukijenga madaraja chini ya kiwango na yakasababisha maafa sisi sote tutakuwa tumefanya uhalifu na tutatakiwa kuwajibika," alionya Chalamila.

Alisema kuwa Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa, imetabiri kuwa mwaka huu kutakuwapo na mvua nyingi, hivyo ni lazima kazi ya ujenzi wa barabara na madaraja ifanyike kwa viwango vinavyokubalika.

Meneja wa Tarura Mkoa wa Mbeya, Gerald Matindi, aliwaasa mameneja wa mamlaka hiyo katika halmashauri zote kuwasimamia makandarasi wanaofanya kazi kwenye maeneo yao ili kazi zote zifanyike na kumalizika kwa wakati.

Pia aliwataka waliosaini mikataba kusimamia kazi hiyo wenyewe na sio kuwaachia wasaidizi kwa madai kuwa endapo kazi itafanyika chini ya kiwango watakaowajibika ni makandarasi wahusika.

"Simamieni hii kazi wenyewe kwani mbali na kuhakikisha kazi inafanyika vizuri, pia itasaidia kudhibiti wizi wa vifaa kwenye miradi yenu ambao unaweza ukakwamisha utekelezaji wa miradi," alisema Matindi.

Alisema fedha zilizotolewa na serikali ni nyingi na zinatakiwa zifanye kazi iliyokusudiwa ili kuepuka kuanza kukumbana na mkono wa sheria, huku akisisitiza kuwa serikali ya sasa haina masihara na wabadhirifu.

Baadhi ya makandarasi ambao wamepata zabuni za ujenzi wa barabara mkoani humo, waliahidi kufanya kazi kitaalamu na kwa uadilifu ili jamii na serikali ione matokeo chanya yatakayotokana na fedha hizo.

Mmoja wa makandarasi hao, James Kitalima, alisema atafanya kazi ambayo itamfanya aendelee kuaminiwa na serikali na pengine kupewa kazi nyingine endapo zitatokea.

Alisema ana wataalamu wa kutosha na hivyo kazi aliyopewa itakamilika ndani ya wakati kwa mujibu wa mkataba aliosaini.

Miradi hiyo inatarajiwa kupunguza changamoto za usafiri na usafirishaji Mbeya kutokana na maeneo mengi kukabiliwa na matatizo ya ubovu wa barabara na madaraja.





# Katibu Alat ahimiza kilimo cha mboga

**Na Augusta Njoji,** MPWAPWA

VIJANA wametakiwa kukitumia kituo cha Kilimo, Mawasiliano na Taaluma kilichoko Mpwapwa mkoani Dodoma, kupata ujuzi wa kilimo cha mboga na maua ili kuondokana na tatizo la ajira.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (Alat), Elirehema Kaaya, alisema hayo jana alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya mradi unaoendelea wa uboreshaji katika kituo hicho cha mafunzo ya kilimo Kibakwe wilayani hapa.

Alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 240, huku Halmashuari ya Wilaya ya Mpwapwa ikitoa zaidi ya Sh. milioni 90.

Kaaya alsiema kituo hicho ni miongoni mwa miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) inayotekelezwa katika mikoa ya Dodoma na Kigoma kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na Ubalozi wa Denmark.

Alishauri vijana wanaomaliza kidato cha nne wajifunze kwenye kituo hicho ili kuondokana na malalamiko ya kukosa ajira.

"Hakuna ajira lakini wajue hakuna ajira inayozidi kilimo cha aina hii. Hii elimu wanayopata hapa wakaifanye wakati wanasubiri matokeo ya kuendelea na elimu ya juu," alisema.

Kaaya alisema kumekuwa na mwamko mdogo wa vijana kuchangamkia mafunzo yanayotolewa na kituo hicho na wengine kuona kama kilimo ni utumwa wakati kinaweza kuwakwamua kiuchumi.

Aliagiza kujengwa kwa mfumo wa kuvuna maji ya mvua kwenye majengo ya kituo hicho ili kukabiliana na upungufu wa maji.

"Changamoto zilizobainisha ni pamoja na kutokuwa na maji ya kutosha, uzio na kutokuwa na nguvu kazi. Wakihitajika vibarua hawapatikani," alisema.

Alitoa rai kwa halmashauri na jamii kuhakikisha kila familia, shule na ofisi mbalimbali zinaweka mfumo wa kuvuna maji ili kutumika kwa shughuli zingine.

Awali, Mkuu wa Kituo hicho, Samson German, akitoa taarifa, alisema kituo hicho kinatoa huduma za kilimo na mifugo kwa wakulima katika eneo husika.

Alisema changamoto iliyopo ni vijana wanaozunguka eneo la kituo kutotaka kujishughulisha kufanya kazi hasa kilimo.

"Wanaona kama kazi si za kwao wanataka kazi zenye kipato kikubwa. Tunalazimika kupata vijana wa kufundishwa kutoka mbali lakini wao wanaotoka hapa hawapatikani. Hata kazi za kupalilia ukimwita kijana wa eneo hili, anaona kazi haimfai kwa sababu haina kipato kikubwa na kituo chetu hakina uwezo wa kuwalipa kiasi kikubwa," alisema.

"Mpaka sasa kituo kimetoa elimu kwa vitendo kwa wanafunzi 30 wa mafunzo ya ujuzi waliotoka Chuo cha Kilimo na Mifugo Visele Mpwapwa, pia wakulima 60 kutoka vijiji vya Kibakwe, Iyenge na Chamtumile juu ya kanuni za kilimo bora cha mboga ili kuboresha lishe na kuongeza kipato," alisema. Naye Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Mpwapwa, Edson Kileo, alisema kuna mwitikio mdogo kwa wakulima kujifunza.



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Semistocles Kaijage, akizungumza wakati wa mkutano na wadau wa uchaguzi mkuu, mkoa wa Dodoma jana. Tume hiyo, inatarajia kuanza kuboresha daftari la kudumu la mpigakura la uchaguzi mkuu kwa mkoa huo, kuanzia Oktoba 26, mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakiwa kuacha kupanga bidhaa maeneo ya watembea kwa miguu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA jijini Dodoma wametakiwa kuacha kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi, yakiwamo yanayotumiwa na watembea kwa miguu ili kujiepusha na ajali zisizo za lazima.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa wafanyabishara na wamachinga kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kutumia maeneo hayo.

Yuna aliwataka wafanyabiashara hao kutokuwa chanzo cha migogoro kati yao na halmashauri kwa kukiuka kanuni na taratibu walizowekewa za kutofanya biashara zao kwenye maeneo hayo.

"Ninawasihi tuheshimu kanuni na maelekezo mnayotakiwa kufanya shughuli zenu za biashara. Si kila eneo mnapanga bidhaa zenu, kumbukeni kuna baadhi ya maeneo si rafiki kwenu kwa kufanya biashara kwa kuwa mengine mnayofanya ni hatarishi kwenu na biashara zenu.

Kama ilivyo mnavyopanga bidhaa zenu kandokando ya barabara ni hatari kwa vyombo vya moto," alisema.

Ofisa huyo alisema wafanyabiashara wanapanga biashara hadi kwenye njia za watembea kwa miguu kando ya barabara hali inayohatarisha usalama wao pia.

Kwa upande wao, wafanyabiashara wanaojishughulisha na kufanya biashara mitaani na pembezoni mwa barabara, kwenye mitaa mbalimbali ya jiji, walisema wanalazimika kupanga bidhaa kwenye maeneo yasiyo rasmi kutokana na kukosa nafasi maeneo yaliyotengwa.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Shabani Mtopwa, alisema wana sababu ya kuingia kwenye mvutano na halmashauri bali changamoto iliyopo kwao ni ukosefu wa eneo la kufanyia biashara.

"Tunaheshimu serikali yetu ambayo imetupa heshima kubwa ya kufanya biashara bila kubugudhiwa ila changamoto tuliyo nayo ni maeneo ya kufanyia biashara zetu ndiyo maana baadhi yao wanajikuta wakikiuka maelekezo na taratibu zilizowekwa za Halmashauri ya Jiji," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Soko la Jioni la Nyerere Square, Baraka Mrisho, aliwataka wamachinga kuheshimu mipaka iliyowekwa na Halmashauri ya Jiji ili wafanye kufanya biashara zao kwa uhuru.

## Wakulima wa alizeti wafundwa mbegu bora

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Wasindikaji Mafuta ya Alizeti Tanzania (Tasupa) kimewataka wakulima kutumia mbegu bora na za kisasa za alizeti ili kuondokana na kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Tasupa, Ringo Iringo, alisema hayo juzi baada ya kubaini wakulima wengi kulima maeneo makubwa lakini ni kilimo kisichokuwa na tija kinachosababisha Tanzania kuagiza mafuta hayo tani 300,000 kwa mwaka ili kukidhi mahitaji ya wananchi.

Iringo alisema wakulima wana kila sababu ya kulima kisasa na kitaalamu kutokana na kwamba wanahitaji kukidhi mahitaji ya wasindikaji mafuta hayo ili nao wafanye uzalishaji wa kutosha utakaokidhi mahitaji nchini.

Alifafanua kuwa kwa mwaka Tanzania inazalisha tani milioni 1.7 za alizeti ambazo asilimia kubwa ya wakulima ni wale wanaolima kienyeji jambo ambalo wangeweza kuzalisha zaidi ya hizo endapo wangelima na kupanda kwa kutumia mbegu bora na za kisasa.

"Tukilima kilimo chenye tija kwa muda wa miaka miwili tutatosheleza kwa mafuta. Tukifanya hivyo basi hatutakuwa na ratiba ya kuagiza mafuta nje, hivyo maofisa kilimo wanatakiwa kuwaelimisha wakulima kuhusu matumizi ya mbegu bora," alisema Iringo. Hata hivyo, Iringo alisema chama hicho msimu ujao hakitanunua alizeti iliyozalishwa kwa mbegu za kienyeji, hivyo akawataka wakulima kuacha kutumia mbegu za kienyeji ambazo hazina ubora.

Aliwataka wakulima wa zao hilo kuacha tabia ya kurudia mbegu zile zile kila wakati kwa kuwa zimeshuka ubora na kusababisha kupata mazao kidogo.

"Hili suala msimu huu hatulitaki kabisa maana inatuletea hasara wasindikaji na hata wakulima mnapata hasara acheni kilimo cha kienyeji," alisema Iringo.

Naye mkulima kutoka Hombolo, Mmota Ipya, alisema ili kuwanusuru wakulima kutumia mbegu za kienyeji mawakala wa pembejeo za kilimo wanapaswa kutembelea maeneo hayo ili kuwasaidia wakulima jinsi ya kuzipata mbegu bora.

Alisema wakulima wanalima zao hilo kwa wingi, lakini wanatumia mbegu za kienyeji kutokana na kwamba wanashindwa kuzifuata kuzitapa.





## Wawezeshwa mashine za kukoboa mpunga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kuwaunga mkono na kuwawezesha wakulima, Serikali ya Mkoa Mjini Magharibi, imewaahidi kuendelea kushirikiana nao na kuwapatia vitendea kazi ili kuondoa matatizo ya kijamii na kiuchumi yanayowakabili wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, mara baada ya kukabidhi vinu vitano vya kusagia mpunga, Katibu Tawala Saleh Mohammed Juma, akiwa ofisini kwake Vuga alisema hatua hiyo itawarahisishia upatikanaji wa huduma hiyo katika maeneo yao.

Alisema uongozi wa serikali ya mkoa huo imeendelea na mikakati yake ya kuwasogezea karibu wananchi huduma mbalimbali za kijamii katika sekta ya elimu, afya na kilimo ili kuona wanajiimarisha kiuchumi.

"Hii ni hatua moja ya kufanikisha mipango yetu ya kuwasaidia wananchi wetu katika sekta tofauti lakini kwa leo tupo hapa kuwakabidhi wananchi wetu mashine hizi za kukoboa mpunga hasa katika wilaya zetu mbili za Magharibi "A" na "B" hasa kwa nia ya kuendeleza na kuinua kilimo cha mpunga," alisema Katibu Juma.

Aidha, Katibu Tawala aliwataka wanajumuiya hao kuzitumia na kuzitunza mashine hizo ziweze kutumika kwa muda mrefu ili azma ya serikali ya kuwaletea maendeleo wananchi wake itimia.

"Niwaombe wanajumuiya vinu hivi vya kukobolea mpunga mkavitumie kikamilifu, lakini kwa umakini mvitunze ili viweze kutumika kwa muda mrefu. Lakini pia viwapunguzie changamoto ya kufuata huduma hii kwa kutembea masafa marefu," alisema Juma.

Wawakilishi wa jumuiya za wakulima waliopata msaada huo walisema vinu hivyo vitaimarisha jumuiya zao kwa kuwaongezea kipato na zitarahisisha upatikanaji wa huduma hiyo katika maeneo yao na kupunguza kazi ngumu ya kuzifuata mashine za kukoboa katika maeneo ya mbali kama ilivyokuwa zamani.

Waliushukuru uongozi wa Mkoa Mjini Magharibi kwa kuwajali wananchi na kuuomba kufanya ziara za mara kwa mara kuzikagua jumuiya zao ili kujua maendeleo na changamoto zinazowakabili.

Jumla ya vinu vitano vya kusagia mpunga vilikabidhiwa kwa jumuiya tano za wakulima wa Mkoa wa Mjini Magharibi.

Walionufaika ni jumuiya za wakulima wa Mtwango, wakulima wa mpunga na umwagiliaji maji wa Bumbwisudi, Kizimbani, Tupendane, Tomondo na Mwevuli ya Kijichi.

# Aahidi kuwasaidia kuleta maendeleo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango Zanzibar, Balozi Mohammed Ramia, amesema serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zote za wananchi za kujiletea maendeleo na kujikwamua na umaskini.

Alisema hayo katika taarifa yake hiyo kwa vyombo vya habari, katika kuelekea Wiki ya Kupambana na Umaskini Duniani, ambapo siku hiyo huadhimishwa kila mwaka Oktoba 17 (leo).

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu kwa hapa Zanzibar ni "Tushirikiane kuwawezesha watoto, familia zao na jamii katika kumaliza umaskini Zanzibar".

Aidha, allisema anaamini kuwa kwa kuwa na umoja na ushirikiano huo miongoni mwa wananchi, kutasaidia kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa na kuvuka lengo la serikali la kuondokana na umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2020 kama inavyoelekeza dira ya maendeleo ya Zanzibar.

Alisema serikali inayoongozwa wa Rais Ali Mohammed Shein, inafanya jitihada mbalimbali za kupambana na umaskini katika nyanja tofauti ikiwamo afya, elimu, kilimo, uwezeshaji wa wananchi hususani vijana, wanawake, wazee, wenye ulemavu na watoto.

Vile vile, taarifa hiyo ilisema kupitia jitihada hizo za kupambana na umaskini zimeleta mafanikio mbali mbali yakiwamo kupunguza asilimia ya idadi ya watu wanaoishi kwenye ufukara na kukosa huduma za msingi kutoka asilimia 61 kwa mwaka 2000 hadi asilimia 30.4 mwaka 2014/2015.

Hata hivyo, Balozi Ramia alisema jitihada hizo zimetokana na kukua kwa uchumi wa nchi na kufikia asilimia 7.1 mwaka 2018, pamoja na kukua kwa kipato cha mtu mmoja mmoja kutoka Sh. 2,104,000 mwaka 2017 na kufikia Sh. 2,323,000 mwaka 2018.

Halikadhalika, Balozi Mohammed Ramia alibainisha: "Kiwango hicho kinakaribia kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha kati kama matarajio yetu kupitia lengo la Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwala 2020."



Washiriki wakiwa katika ufunguzi wa mradi wa kuwawezesha wanawake na watoto kujua haki zao katika ofisi za Tamwa, Tunguu Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali kusaidia shule binafsi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI inakusudia kuendelea kushirikiana na shule binafsi visiwani Zanzibar, ili kuhakikisha lengo la kuwapatia watoto na vijana elimu linafikiwa.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohd Said, aliyasema hayo katika mahafali ya kidato cha nne, darasa la sita na ya darasa la maandalizi yaliyofanyika katika Shule ya Stone Town International, iliyoko Migombani mjini Unguja.

Alisema Wizara ya Elimu Zanzibar, inatambua mchango umuhimu wa kuwapo kwa shule binafsi nchini na kwamba kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, itaendelea kuzipatia usajili pamoja na miongozo mbalimbali.

Aliongeza kuwa lengo ni ili shule hizo ziweze kutoa elimu bora kwa vijana ambao ndiyo viongozi wa sasa na kesho.

Alisema kila mtoto ana haki ya kupata elimu iliyo bora, hivyo ni vyema wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao shule wakiwa na umri sahihi unaoelekezwa na Wizara ya Elimu ambao ni kuanzia miaka minne kwa ngazi ya maandalizi na darasa la kwanza akiwa na umri wa miaka sita.

Aidha, aliizungumzia kuhusu usalama wa wanafunzi wanapokwenda shuleni akisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya madereva wa magari yanayowahudumia wanafunzi wa shule binafsi.

Alionya kuwa wanawapakia watoto kupita kiasi na idadi iliyopangwa, jambo ambalo alisema ni kinyume na sheria na pia ni hatari kwa maisha ya watoto hao na kuwataka waache mara moja.

"Madereva wa mabasi ya shule wanaojaza wanafunzi kupita idadi inayotakiwa hii ni hatari kutokana na mrundikano wa wanafunzi unaweza kusababisha wakapata matatizo kwani hewa haiwatoshi kikamilifu, ni vyema shule zikaliangalia hili tatizo na kufuata sheria za usalama barabarani, wanapowapakia wanafunzi katika mabasi hayo." Alionya.

Mkurugenzi wa Shule ya Stone Town International, Jamila Gulam Hussein, aliwataka wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne kujiendeleza zaidi katika masomo yao na kutoridhika na walipofikia kwani kumaliza kidato cha nne si kumaliza masomo.

# Viongozi ushirika matatani upotevu ufuta wa mamilioni

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi, inawashikilia kwa mahojiano viongozi wanane wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) Kata ya Nyangamara, wilayani Lindi, kwa tuhuma mbalimbali zikiwamo upotevu wa kilo za ufuta 138,894 zenye thamani ya Sh. 47,822,200 za wakulima.

Mkuu wa taasisi hiyo mkoani hapa, Stephen Chami, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Aliwataja wanaoshikiliwa ni Mwenyekiti, Said Mohamedi Nahonyo na makarani Fikiri Mchokwe, Mohamedi Kunyata (Nyanggamara B), Lucas P. Lucas na Hassani H. Nnyiyanda (Nyanggamara A).

Wengine ni Anuary Hassani Nahoda, George Solo na Ahamadi Kulowa Chama cha msingi Kilidu katika Kata na Tarafa ya Nyangamara, ambapo wakulima wasiopungua 62 wanalalamikia viongozi hao kutowalipa fedha zao zinazotokana na mauzo ya ufuta wao msimu 2019/2020.

Chami alisema viongozi hao wanakabiliwa na tuhuma mbalimbali, zikiwamo kushirikiana na makarani wa vyama vya msingi kutoa taarifa za uongo juu ya uwapo wa tani za ufuta katika maghala, kuorodhesha majina hewa ya wakulima yanayoonyesha wamelipwa wakati sio kweli na kiwango cha kilo zilizokusanywa na makarani hao.

Tuhuma zingine ni utofauti wa kiwango cha ufuta unaokusanywa na zinazosafirishwa, upotevu wa ufuta kwenye matawi ya vyama ushirika vya msingi na ushirika unaosababishwa na makarani hao, kusafirishwa zao hilo la wakulima bila ya uwapo wa kumbukumbu zozote na kujilipa fedha kinyume cha sheria na taratibu.

Chami alisema Said Nahongo na karani wake Fikiri Mchokwe wanadaiwa kujilipa kinyume cha utaratibu Jumla ya Sh. 4,433,200, huku wakionyesha waliuza kilo 1,712 msimu wa mwaka 2019/2020.

Alisema Kolowa anadaiwa kupoteza kilo 10,239 za zenye thamani ya Sh. 27,645,3000 kwa maelezo alikusanya kilo 131,321, lakini kiwango alichosafirisha kinaonyesha ni kilo 121,082 tu, huku Solo akielezwa kupoteza kilo 2,966 zenye thamani ya Sh. 8,008,200 na kufanya upotevu wa kilo 5,880 zenye thamani ya Sh. 15,876,000 hazijulikani ziliko.

Lucas, Kunyata na Nahoda wanadaiwa kupoteza kilo 496 za zenye thamani ya Sh. 1,139,200 mali za wakulima wasiopungua 62 wa Tarafa ya Nyangamara.

Chami alieleza baada ya kuwabana watuhumiwa hao, jumla ya Sh. 7,000,000 walizirejesha na zinatarajiwa kukabidhiwa kwa Mrajisi wa vyama vya Ushirika, ambapo ataandaa utaratibu wa malipo kwa wakulima ambao hawajalipwa.

"Wakati wa urejeshaji wa fedha hizo ukiendelea, Takukuru kwa mamlaka iliyopewa tumefunga akaunti za Chama cha Nyangamara zisiendelee kutumika," alisema.

Ametaja sababu za kuzuia Akaunti ya Chama hicho kuepusha viongozi wake kutumia kiasi cha fedha kilichopo katika Akaunti hiyo kinyume cha utaratibu, huku akimtaka karani wa Chama cha msingi Utimbe Amcos kujisalimisha mwenyewe Ofisi ya Takukuru.

Alisema baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, wataangalia utaratibu mwingine ikiwamo kuwafikisha mahakamani watakaohusika na upotevu wa mali na fedha za wakulima.




Ofisa wa Bima wa Benki ya NBC, Emarynziana Mtega (kulia), akitoa elimu kuhusu umuhimu wa kujiwekea bima za aina mbalimbali zitolewazo na benki hiyo, kwa mmoja wa wateja kutoka Kampuni ya Mogas Tanzania Ltd, Grayson Kazeni, katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC awataka wazee wa Rukwa kubadilika kifikra kuhusu mila

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amewataka wazee mkoani Rukwa kubadilika kifikra kuachana na baadhi ya imani za jadi.

Badala yake wametakiwa wazingatie chanjo mbalimbali zinazotolewa na serikali kwa nia ya kukabiliana na magonjwa ambayo yamekuwa yakiwakabili watoto wadogo.

Kauli hiyo aliitoa jana katika kikao maalumu cha maandalizi ya uzinduzi wa kampeni ya jumuishi ya chanjo ya surua.

Alisema anatambua kuwa baadhi ya magonjwa yamekuwa yakitibiwa kwa kutumia dawa za jadi tangu zamani, lakini baadhi ya magonjwa ambayo yanasababishwa na virusi daima hayana tiba, hivyo ni vizuri kupata chanjo.

Wangabo alisema wazee wa mila na desturi hususan machifu wa makabila yote ya Wafipa wana jukumu la kuhakikisha wananchi wajitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuwapeleka watoto ili wakapate chanjo hizo.

"Nafahamu kwa mfano ugonjwa wa surua, tangu zamani watu walikuwa wanapewa dawa za jadi wanapougua, hata mimi niliwahi kupewa nikiwa mtoto, lakini hivi sasa kuna chanjo, hivyo ni vyema watoto wakapelekwa kwenye vituo ili wakapatiwe chanjo, uwakinge na magonjwa hayo," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Dk. Boniface Kasululu, alisema ugonjwa wa surua umekuwa ukisababisha sana vifo kwa watoto wengi wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Alisema katika mkoa huo, watoto wapatao 163,564 wenye umri wa kati ya miezi tisa hadi 59 wanatarajiwa kupatiwa chanjo na watoto 92,879 wenye umri wa kati ya miezi 18 hadi 42 pia wanatarajiwa kupatiwa chanjo ya polio ya sindano.

## Maonyesho ya wajasiriamali

**Na Happy Severine,** BARIADI

WAJASIRIAMALI zaidi ya 300 waliodhaminiwa na mifuko ya uwezeshaji, programu na vikundi vya kifedha nchini, wameshiriki maonyesho ya tatu ya mifuko hiyo, yanayofanyika kwa siku tatu mkoani Simiyu.

Maonyesho hayo yenye kauli mbiu ya mitaji ni chachu ya kujenga uchumi wa viwanda Tanzania yanafanyika kitaifa mkoani Simiyu yakiwa ni maonyesho ya awamu ya tatu yakiwa na lengo kutoa elimu na kuwakutanisha wajasiriamali hao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika viwanja vya maonyesho vya Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Ofisa Uwezeshaji na Uwezeshaji kutoka Baraza la Uwezeshaji, Edward Kessy, alisema wajasiriamali hao wamekutana ili kubadilishana uzoefu na kuwa mashuhuda wanufaika wa mifuko hiyo ili na wajasiriamali wengine waweze kujua manufaa ya kuwezeshwa na mifuko hiyo. "Baraza la uwezeshaji wananchi kiuchumi limeandaa maonyesho hayo ikiwa ni sehemu ya kubadilishana uzoefu na kuwaonyesha kwa vitendo wajasiriamali wengine ambao hawajanufaika na mifuko hiyo ili na wao wajue watanufaika vipi na kuboresha bidhaa zao," alisema. Aliongeza kuwa katika maonyesho hayo yanayofanyika kwa siku tatu, mgeni rasmi siku ya kufunga maonyesho hayo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa.

Naye Ofisa kutoka Taasisi ya Pass, Faustine Paul, alisema wanajukumu la kuwaunganisha wajasiriamali wote nchi nzima pamoja na mifuko hiyo ambapo kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kufanya hivyo.

Alisema mbali na kuwaunganisha wajasiriamali hao, pia wanajukumu la kuwasaidia na kuwaelimisha wajasiriamali namna ya kukuza na kuongeza thamani biashara zao.

Edista Njau ofisa kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), alisema wao wakiwa ni moja kati ya mifuko ya fedha iliyowawezesha wajasiriamali wengi nchi nzima tangu wameanzisha programu hizo, wameshatoa mikopo ya Sh. trilioni 1.7 kwa wajasiriamali wa nchi nzima.

## Majeneza ya kale 20 yapatikana

**CAIRO, Misri**

WIZARA ya Mambo ya Kale Misri imesema wanaikolojia wamepata majeneza ya kale zaidi ya 20 yaliyokuwa yamefukiwa karibu na Mji wa Luxor nchini humo.

Majeneza hayo yaliyo na rangi ya kuvutia na ambayo bado michoro yake inaonekana, yalipatikana eneo la Asasif, katika ukingo wa magharibi mwa mto Nile.

Wataalamu hao wameeleza kuwa majeneza hayo yalikuwa kwenye matabaka mawili, huku ile ya juu ikipatana na ile ya chini.

Wizara hiyo imetaja ugunduzi huo kama moja ya ugunduzi muhimu katika miaka ya hivi karibuni.

Hata hivyo, wizara hiyo imeeleza kuwa maelezo ziadi kuhusu majeneza hayo yatatolewa kwa vyombo vya habari siku ya Jumamosi.

Makaburi mengi katika eneo la Asasif, ambalo liko karibu na bonde la Kings, ni ya kale (664-332BC).

Wiki iliopita, wizara ya vito za kale ilitangaza kuwa wanaikolojia wamevumbua eneo la viwandani la kale katika bonde la magharibi mwa Luxor.

Eneo hilo lilijumuisha nyumba za kuhifadhi na kuosha samani, ambapo nyingi zilikuwapo tangu utawala wa kifalme wa karne ya 18.

**BBC**

## Maswali lukuki ndege ya serikali ikianguka

**KINSHASA, Congo**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi Tshilombo, amekutana na familia ya waathiriwa wa ajali ya ndege ya serikali Antonov 72.

Dereva wake na maofisa wake kadhaa wa ulinzi walikuwa katika ndege hiyo.

Ofisi ya Rais ilithibitisha rasmi mwanzoni mwa wiki hii kuwa mabaki ya ndege hiyo yamepatikana katika eneo la Sankuru na kuahidi kufanya juhudi ili ukweli kuhusu mazingira ya ajali hiyo ujulikane.

Miili ya kwanza iliyopatikana karibu na mabaki hayo yamesafirishwa na kikosi cha Umoja wa Mataifa nchini DRC, MONUSCO.

Mamlaka nchini Congo imethibitisha kuwa miili ya watu wanne imepatikana, huku rubani amethibitishwa kupatikana akiwa hai.

Maswali yameibuka kuhusu ajali ya ndege hiyo ya Jeshi la DRC, ambayo ilikuwa imetumiwa na ofisi ya rais kwa kusafirisha gari ya rais na walinzi wake wa karibu Mashariki mwa DRC.

Ndege hiyo ilipotea siku ya Alhamisi ikiwa na watu watano, mmoja wapo akiwa dereva maalumu wa Rais Tshisekedi.

Awali palikuwa na taarifa kinzani kuhusu mahali ndege hiyo ilipo pamoja na idadi ya watu waliokuwamo.

**RFI**

# Kenya yazindua reli nyingine ya SGR

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amezindua Mradi wa Reli ya Kisasa maarufu SGR utakaounganisha Uwanja wa Kimataifa wa Jommo Kenyatta hadi jijini Nairobi.

Imeelezwa kuwa reli hiyo itapunguza msongamano mkubwa wa magari na kugharimu dola milioni sita.

Barabara hiyo ya moja kwa moja ni sehemu ya mpango wa serikali wa kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Nairobi ambalo idadi ya watumiaji wa magari inazidi kuongezeka.

Benki ya Dunia (WB) ilikisia kuwa Kenya hupoteza kima cha dola 5,000 kila siku kutokana na msongamano ya magari huku watu wakipoteza muda wao kwenye msongamano huo.

Msongamano wa magari pia huchangia wasafiri kukosa safari zao za ndege katika uwanja huo wa kimataifa wa Jommo Kenyatta.

Rais Kenyatta akizindua mradi huu baada ya Benki ya Dunia kujiondoa kwenye ubia na serikali ya Kenya alisema:

"Wengine wanasema ooh! Hii reli inaenda wapi? Hakuna kitu kibaya kama ujinga wa mtu ambaye fikra zake ni namna hii. Sasa sisi tukisema tunajenga hii kusaidia wananchi tatizo liko wapi?" Alisema Kenyatta.

Mradi huo ni matokeo ya ziara ya Rais Kenyatta Septemba mwaka jana katika taifa la China, kwenye kongamano lililowaleta pamoja viongozi wa Afrika pamoja na wawekezaji.

Mradi huu utatekelezwa na kampuni ya ujenzi wa barabara na madaraja ya China, kwa ushirikiano wa serikali ya Kenya na mashirika ya kibinafsi.

Inakadiriwa kuwa magari 60,000 hutumia barabara hiyo kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jommo Kenyatta hadi Westlands kila siku.

Reli hiyo pindi ikikamilika idadi ya watumiaji magari itaongezeka kwa magari 25,000.

Pia itakuwa na urefu wa kilomita 17. Badala ya kuchukua saa nyingi kufika uwanja wa kimataifa, Reli hiyo itakapokamilika mtumiaji atatumia dakika 10 au 15 kutoka katikakati ya Jiji.

Hata hivyo, wataalamu wanasema kuwa mradi huo ni ghali sana ikilinganishwa na gharama inayostahili kuchukuliwa huku ushirikiano kati ya China na Afrika ukiendelea kupanuka.

***DW***



Rais wa Marekani, Donald Trump, akiongea na waandishi wa habari White House hivi karibuni. **PICHA: VOA**

# Kesi dhidi ya Rais Trump yapamba moto

**WASHINGTON, Marekani**

KESI dhidi ya utawala wa Rais wa Marekani, Donald Trump ya madai ya kuzuia uchunguzi inazidi kupamba moto.

Mwakilishi wa Chama cha Democrat, Adam Schiff, anasema kuwa kuongezeka kasi kwa kesi hiyo kunatokana na wanachama wa ngazi ya juu na mwanasheria wa Rais Trump binafsi, Rudy Giuliani kupuuza hati ya wito juu ya shauri la uchunguzi linalotaka kumwondoa madarakani.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Mike Pence, imeuita uchunguzi wa baraza la wawakilishi linaloongozwa na wa Democrat, ni utashi wao wenyewe na hati ya kuitwa kujibu maswali ni pana mno.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani Pentagon, imesema haina uwezo kutoa ushirikiano kwa muda huu kutokana na sababu za kisheria.

Ofisi ya Bajeti ya White House nayo imekataa ombi la baraza hilo, na Mwanasheria binafsi wa Rais Trump, Rudy Giuliani.

Pia amekataa kuitikia wito wa hati inayomtaka kutoa nyaraka zinazohusiana na juhudi za kuishinikiza Ukraine kumchunguza Makamu wa Rais wa zamani na mgombea urais wa Democrat hivi sasa, Joe Biden.

Juzi, Mwakilishi wa Baraza la Wawakilishi, Michael McCaul, kiongozi wa Chama cha Republican katika Kamati ya Mambo ya Nje, alisema uchunguzi wa kumwondoa Rais madarakani unaoendelea kwa faragha, ilitakiwa ufanyike hadharani.

"Namtaka spika aweke azimio hilo hadharani ili tuendelee katika njia ya uwazi na suala hili hali ya kuwa watu wote wa Marekani wanafahamu kile kinachoendelea kwa sababu mwisho wa siku, ni wao ambao wataathirika na mchakato usiokuwa wa haki," alisema McCaul.

Lakini, Schiff alisema wanachama wa Republican wamewakilishwa ipasavyo katika mahojiano hayo ya faragha, akisema wanapewa kila fursa kuwahoji mashahidi na kuona ushahidi.

***VOA***

# Wafanyakazi Tigo wahukumiwa kifungo cha nje miezi 6

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam imewahukumu watu watano wakiwamo wafanyakazi wa Kampuni ya Simu ya Tigo na wafanyabiashara wawili kutumikia kifungo cha nje cha miezi sita na kulipa fidia ya Sh. milioni 20.3 walizojipatia kutoka kwa wateja wa kampuni hiyo.

Kadhalika mahakama hiyo imesema simu na laini zake 13 zilizotumika kujipatia fedha hizo na sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kuwa mali ya serikali. Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile, baada ya washtakiwa hao kumwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kukiri makosa yao.

Hakimu Rwizile alisema amesikia hoja za pande zote mbili, makosa waliyotenda washtakiwa si mepesi kwa mujibu wa sheria aliyepatikana na hatia katika makosa hayo atatumikia kifungo.

Alisema lazima adhabu kali itolewe ili iwe fundisho kupunguza makosa ya mtandao.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Awamu Mbagwa, alidai kuwa upande wa Jamhuri hauna kumbukumbu na makosa ya nyuma dhidi ya washtakiwa, kwamba ni wakosaji wa mara ya kwanza. Alidai kuwa washtakiwa wameingia makubaliano na DPP Jamhuri haipendekezi adhabu kubwa.

"Mheshimiwa hakimu washtakiwa wamekubali kulipa kiasi hichi cha fedha na mpaka wanatia saini makubaliano tayari fedha zimeingizwa kwenye akaunti ya serikali," alidai Mbagwa.

Washtakiwa kwa nyakati tofauti walidai kuwa ni wakosaji wa mara ya kwanza wameingia makubalinao na DPP na kwamba tayari wameshalipa fedha zote, mahakama ione malipo hayo kama adhabu tosha dhidi yao.

Wafanyakazi wa Tigo katika kesi hiyo ni Kokubelwa Karashani, mtoa huduma kwa wateja, Godfrey Magoye, wakala na Khalfan Milao, mtoa huduma kwa wateja. Wengine ni Mohamed Abdallah mfanyabiashara na Moses Kilosa.

Mapema mahakamani hapo, Mbagwa alidai kuwa, Kati ya Januari Mosi 2018 na Juni 20, 2019, katika maeneo tofauti Kati ya Dar es Salaam na Arusha, washtakiwa hao walijipatia Sh. 20,378,627 mali ya wateja wa kampuni ya Tigo ambazo walizitoa kutoka Tigopesa bila kuwa na kibali chao.



Wafanyausafi wakizoa mchanga katika Barabara ya Nyerere, eneo la Mtava, jijini Dar es Salaam jana, uliosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tanapa yapeleka maji bwawa la viboko

**Na Enock Charles**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (Tanapa), limeanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kupeleka maji kwenye eneo la viboko walioko kwenye Hifadhi ya Katavi.

Hivi karibuni, Rais Magufuli akiwa mkoani Katavi alitembelea hifadhi hiyo na kujionea wanyama hao wanavyoteseka kwa kukosa maji kwa kuwa nyakati za mchana wanapaswa kuwa ndani ya maji kutokana na ulaini wa ngozi zao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kamishana Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi na Mawasiliano wa Tanapa, Paschal Shelutete, alisema ukosefu wa maji uliokuwa ikisababisha viboko kufa sasa halipo tena kwa kuwa shirika limechukua hatua ya kupeleka maji ya kutosha.

Shelutete pia alisema alisema shirika limeanza kutoa elimu ya viumbe hai kwa wananchi walio jirani na hifadhi hiyo.

"Sasa tunapeleka maji ya kutosha kwa kadri yanavyohitajika, hakuna tena hiyo changamoto," alisema.

Kuhusu shughuli za kibinadmu, alisema wanatoa elimu kwa wananchi wanaozunguka hifadhi ili kuwe na mgawanyo sawa wa maji kati ya binadamu na wanyama.

Akiwa hifadhini humo, Rais aliagiza Tanapa kupeleka maji kwa wanyama hao huku akieleza faida kubwa kwa Taifa ikiwemo kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Akizungumza na wananchi wa Mpanda mjini ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake, alisema amepita katika hifadhi ya Katavi na kuona maji yakiwa yamekauka kwenye mto wenye viboko, ivyo kusababisha viboko hao kuanza kupasuka kutokana na kupigwa na jua.

# Wadau wajadili mfumo uagizaji mbolea pamoja

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

SERIKALI imeelezea kuridhishwa na mfumo wa uagizaji wa mbole kwa pamoja licha ya uwapo wa changamoto kadhaa zikiwamo za ucheleweshaji wa mbolea kuwafikia wakulima pamoja na suala la bei elekezi.

Kauli hiyo ilitolewa jana Mjini Morogoro na Ofisa Kilimo Idara ya Mazao Kitengo cha Pembejeo kutoka Wizara ya Kilimo, Joseph Lyafwila, wakati wa warsha ya wadau wa Sekta ya Kilimo iliyokuwa ikijadili matokeo ya utafiti uliofanywa kuhusu mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja ulioandaliwa na Baraza la Kilimo Tanzania.

"Kwetu kwenye sekta ya kilimo mfumo huu ni mpya na tayari tumeona mafanikio yake ndani ya kipindi cha miaka mitatu, hivi sasa mbolea inafika nchini kwa wakati na wakulima pia inawafikia kwa wakati, ni ukweli kwamba bado kunachangamoto kadhaa," alisema.

"Tunajua pia wakulima wamekuwa wakilalamikia suala la bei na hii inatokana na ukweli kwamba kuna baadhi ya vijiji viko mbali sana, na inafanya bei kupanda kidogo ingawa Serikali bado inaangalia changamoto zote zinazoendelea kujitokeza katika mfumo huu ili tuweze kuzishughulikia," alisema. Joseph.

Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utetezi kutoka Baraza la Kilimo Tanzania, Timothy Mmbaga, alisema waliamua kufanya utafiti huo kuhusu maendeleo ya mfumo ili kuona namna inavyoweza kuishauri Serikali namna bora zaidi ya kuendelea na mfumo huo.

"Kabla ya mfumo huu kulikuwa na changamoto nyingi sana watu walikuwa wanauziwa mbolea feki wengine walikuwa wanauziwa hadi siment, lakini Baraza la Kilimo tulipiga sana kelele na tunaishukuru Serikali ililiona hili na hatimaye kuja na mfumo huu."

"Tunajua mahitaji ya mbolea yanazidi kuongezeka hivi sasa inakadiriwa kufikia tani 400,000 ingawa kupitia mfumo huu ni tani 70,000 pekee ndio inayoagizwa ingawa tunajua kuna njia nyingine nyingi za uagizaji wa mbolea zaidi ya DAP na UREA zinazoagizwa kupitia mfumo huu," alisema Mmbaga.

Mshauri Mwelekezi katika utafiti huo, Dk. Lutengano Mwinuka, akizungumzia matokeo ya utafiti huo kuhusu Mpango wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja, alisema tangu kuanza kwa mfumo huo umesaidia kuongezeka kwa tija katika uzalishaji.

"Tulichokiona huu mfumo ni mzuri na una uwezo wa kuongeza tija katika kilimo na tuomeona kumekuwa na wigo mkubwa sana wa upatikanaji wa mbolea hasa katika mbolea hizi za DAP na UREA" alisema Dk. Mwinuka.

Dk. Mwinuka ambaye pia ni Mhadhari wa Kitivo cha Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, alisema huu ni wakati mwafaka kwa wafanyabiashara kuanzisha vituo maalum katika maeneo mbalimbali hasa vijijini, lengo ni kumfikia mkulima wa chini zaidi.

"Katika utafiti wetu pia tumegundua usafirishaji wa reli ndio njia pekee inayoweza kusaidia bei ya mbolea kushuka zaidi na hii itasaidia tu endapo miundombinu ya reli itazidi kuelimishwa zaidi," alisema Dk. Mwinuka.

"Mfumo huu wa uagizaji ni bora zaidi kwa sababu wakulima wote wanapata mbolea kwa bei moja ambayo ni elekezi na zamani mfumo wa ruzuku ulikuwa unalenga wakulima wachache sana ingawa pia mfumo ule ulikuwa na magendo mengi ukilinganisha na mfumo wa sasa," alisema Joshua Ivan kutoka kampuni ya mbolea ya OCP.

"Nadhani ni wakati sasa wa makadirio sahihi ya uhitaji ya pembejeo yakafanyika mapema kabla ya kupanga bei elekezi, na kutoa tenda kwa msambazaji, lakini pia ni muhimu kwa serikali kuanza kufanya kazi kwa karibu zaidi na wasambazaji," alisema Benedict Masasi, msambaji wa pembeejo kutoka Njombe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA


**SHAMBA LINAUZWA**, Hekari 25@Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**JAMES ENOCK MKAYULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0377/0784** kilichotolewa na LUGALO J.W.T.Z CENTER mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1662/13.**

115463102

## KUPOTEA KWA CHETI



**CONSTANTINE ATHANAS KIONDO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0781/0035 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1997 katika Shule ya Sekondari Arusha .

yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa : AR/RB/2745/2019**

115462702

## KUPOTEA KWA KADI

**MARK KASTABU MREMA** anatanga kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili MC 247 AWR aina FEKON, yenye chasis namba LDAPAJ0B8FGB09235.

Yeyote atakaeipna atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: WMB/RB/9145/2019

115462902

**JAHMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**ILIYOPO DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MAOMBI YA KUMBUKUMBU NA. 12 YA 2019**

**TANZANIA FERTILIZER COMPANY LTD............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

1. RUVUMA EXPORTS COMPANY (T) LTD
2. STANDARD COMMERCIAL TOBBACO SERVICE (T) LTD (STANCOM).........WAJIBU MAOMBI POPOTE WALIPO

Mnajulishwa kwamba Shauri la Maombi ya Kumbukumbu tajwa hapo juu limepengwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 23/10/2019 saa tatu kasorobo asubuhi (2:45).

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakam hii leo hii tarehe 30/9/2019

115462602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA:**
**TALAKA No. 48/2019**

**MDAI: CHARLES NORBERT KAHOZA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: WILCHISTER PAULO LUKINYA WA DAR ES SALAAM.**

AMRI: Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 17/10/2019 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo **IJUMAA tarehe 27 mwezi 09/2019.**

115463802


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO




# DE LIGT:

## SINA FURAHA NA KIWANGO CHANGU JUVE

**TURIN, Italia**

BEKI kinda Matthijs De Ligt amesema kwamba, hana furaha na kiwango chake hadi sasa pale Juventus msimu huu.

De Ligt mwenye umri wa miaka 20, alijiunga na Juventus akitokea Ajax kipindi cha majira ya joto kwa euro milioni 75, na kumfanya kuwa beki ghali zaidi katika historia ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi ameanza na wakati mgumu wa maisha pale Turin na amesema anahitaji kujiimarisha zaidi.

"Nikiwa Ajax, nilihisi nipo kwenye kiwango bora, leo hii ni tofauti," alisema akiambia Fox Sports.

"Lakini nafikiri ni kawaida kwa sababu kila kitu kipya kwangu mimi. Ninaendelea kujiimarisha na sina hofu kabisa.

"Sijui mwenyewe kwa nini sichezi vizuri kama ilivyokuwa mwanzo. Ninachoweza kufanya ni kuhakikisha ninacheza vizuri ili kufikia ubora wangu, kufanya zaidi kujifunza kutoka kwa wachezaji wenzangu.

"Ninacheza na hicho ndio kitu muhimu, kwa sababu mwishoni kila kitu kitakuwa sawa na natakiwa kuwa na mtazamo chanya wakati wote."

De Ligt alisababisha penalti wakati wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Inter Milan kwenye Uwanja wa San Siro wikendi iliyopita.

Pia alikanusha ripoti kwamba kocha wa Juventus, Maurizio Sarri amemwambia kupunguza uzito kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

De Ligt aliiongoza Ajax kushinda mataji mawili ya nyumbani msimu uliopita na pia kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## UEFA YAIADHIBU LAZIO KWA UBAGUZI

**ROME, Italia**

LAZIO imepewa adhabu ya kucheza mechi moja ya Uefa bila mashabiki kwenye uwanja wake wa nyumbani baada ya mashabiki wake kuonyesha ishara za kibaguzi kwenye mchezo wa Kombe la Ligi ya Europa dhidi ya Rennes.

Mashabiki walipiga kelele za kibaguzi kwenye Uwanja wa Olimpico, wakati Lazio ilitoka nyuma na kushinda mabao 2-1 Oktoba 3, mwaka huu.

Bodi ya udhibiti, maadili na nidhamu ya Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), imeikuta na hatia Lazio kupitia vifungu 46, 47, 48 na 49 na wametakiwa kuweka bango la 'la usawa' katika mchezo wake ujao wa Europa.

Lazio pia lazima ilipe faini ya euro 20,000 na watafungiwa mchezo mmoja wa Uefa kucheza kwenye uwanja wao kama wakionekana kuvunja sheria mwaka ujao.

Miamba hao wa Serie A, wamebainisha kwamba, watawachukulia hatua za kisheria mashabiki wake wote waliohusika na kelele hizo za ubaguzi wa rangi.



## TONALI AJIFANANISHA NA PIRLO, GATTUSO AKICHEZA ITALIA

**MILAN, Italia**

SANDRO Tonali amesema yeye ni mchanganyiko wa Andrea Pirlo na Gennaro Gattuso wakati akijilinganisha yeye mwenyewe na magwiji hao wa Italia baada ya kuanza kuichezea mechi yake ya kwanza timu hiyo ya taifa.

Tonali alitokea benchi kuingia kwenye kikosi cha Italia kilichoibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Liechtenstein kwenye mchezo wa kufuzu kwa Euro 2020, Jumanne wiki hii.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, akitokea klabu ya Brescia - ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na mabingwa wa Italia, Juventus, Manchester United na Fiorentina alipaza sauti yake mara baada ya mchezo huo.

"Nafikiri nafanana na mmoja wa mabingwa hao," alisema Tonali baada ya Rai Sport kumlinganisha na kina Pirlo, Gattuso na Daniele De Rossi.

"Pengine kuwachanganya wote litakuwa jambo jema zaidi. Nafikiri




kuna mfano na Pirlo kwa namna fulani, lakini pia unaweza kuongeza mfanano zaidi na Gattuso."

Italia iliendeleza rekodi kwenye michuano hiyo ya kufuzu kwa kushinda mechi tisa, wakiwa tayari wameshafuzu kucheza michuano ya Euro 2020 baada ya ushindi wake dhidi ya Ugiriki Jumamosi.

Kocha wa Italia, Roberto Mancini aliwaanzisha wachezaji vijana kwenye mchezo huo katika dimba la Rheinpark, akiwaweka kikosi cha kwanza, Federico Bernardeschi, Andrea Belotti, Alessio Romagnoli na Stephan El Shaarawy na wote walifunga.

Pia kulikuwa na nafasi ya Tonali kuanza kuichezea nchi yake hiyo kwa dakika 16 zilizobaki na alionyesha hisia za ajabu wakati akiingia kuchukua nafasi ya Bernardeschi.

"Nilijihisi kitu fulani cha maajabu kuichezea timu ya taifa. Kwa sekunde 30 nilihisi kama ni ndoto," aliongeza Tonali.

"Kocha alituambia kuwa tayari kucheza, hivyo nikawa na wazo la kuhakikisha nacheza tu. Wachezaji wote kwenye kikosi walikuwa msaada kwangu."

# RASHFORD

## AANDALIWA KUMRITHI SUAREZ BARCA




**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imefuta mpango wake wa kumsajili nyota wa Liverpool, Roberto Firmino sasa imemgeukia mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford.

Barcelona inamwona Rashford ni bora zaidi ya Firmino aliyekuwa katika mipango yao ya awali.

Rashford alitia saini mkataba wa miaka minne unaomwezesha kulipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, lakini kinda huyo mwenye miaka 21 ameonekana bora zaidi ya Firmino.

Klabu hiyo inasaka mchezaji wa kuziba pengo la Luis Suarez na miongoni mwao yumo nahodha wa England na Spurs, Harry Kane pamoja na Kylian Mbape wa Paris Saint Germain.

Katika orodha hiyo yumo mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Suarez (33), anajiandaa kuondoka Nou Camp katika usajili wa majira ya kiangazi msimu ujao.

## Pochettino amrudisha Vorm langoni Spurs

**LONDON, England**

GOLIKIPA Michel Vorm amerejeshwa kwenye kikosi cha Tottenham Hotspurs, baada ya kuachwa mwishoni mwa msimu uliopita wakati mkataba wake na klabu hiyo ulipofikia mwisho.

Vorm amerudi klabuni hapo kwa mkataba maalum na anatarajiwa kuwa langoni mwishoni mwa juma hili katika mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Watford.

Vorm raia wa Uholanzi, amepewa nafasi hiyo baada ya kuumia kwa golikipa namba moja, Hugo Lloris, alipokua kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Brighton.

Kocha wa Spurs, Mauricio Pochettino amependekeza kurejeshwa kwa golikipa huyo mwenye umri wa miaka 35, ili asaidiane na Paulo Gazzaniga ambaye alikua chaguo la pili baada ya Lloris.

"Sijaona tofauti kubwa kurejea hapa, klabu hii ni kama nyumbani na ninaahidi kupambana ili kusaidia kufikia malengo," alisema Vorm baada ya kukamilisha usajili wake akiwa kama mchezaji huru.

"Nilipigiwa simu ya kunitaka kurudi hapa, na mimi sikukataa kufanya hivyo kwa sababu ninahitaji kuwa sehemu ya mafanikio ya klabu hii.

"Tunahitaji kushikamana kwa pamoja, kila mmoja atambue mchango wa mwingine ili kufikia lengo," aliongeza Vorm, ambaye amesisitiza kuwa tayari kwa mapambano ya kuwania nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Spurs.

Vorm atavaa jezi namba 13, ambayo aliitumia wakati akiwa klabuni hapo, kabla ya kuondoka mwishoni mwa msimu uliopita.

Kwa mara ya kwanza Vorm alisajiliwa klabuni hapo mwaka 2014, na alifanikiwa kucheza mechi 47.



## Kocha wa Bulgaria aichokonoa England

**SOFIA, Bulgaria**

KOCHA wa timu ya Taifa ya Bulgaria, Krasimir Balakov amekanusha taarifa za kuwapo kwa vitendo vya ubaguzi wa rangi, wakati wa mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Ulaya dhidi ya England, akidai hakuona kitu kama hicho.

Balakov amekanusha uwapo wa vitendo hivyo alipozungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo, ambapo amesema hakusikia wala kuona mashabiki wakishiriki kwenye kadhia hiyo inayopigwa vita michezoni.

Alisema kilichotokea ni zogo la kawaida kutoka kwa mashabiki, ambalo mara kadhaa hutokea katika viwanja vya michezo, lakini si kwa kisingizio cha ubaguzi wa rangi ambao umedaiwa ulikuwapo kwenye Uwanja wa Taifa wa Vasil Levski, uliooshuhudia wenyeji Bulgaria wakichabangwa mabao 6-0.

"Binafsi sikuona wala kusikia vitendo vya kibaguzi, kilichotokea ni zogo la mashabiki ambao siku zote wamekuwa wakifanya hivyo kwenye viwanja vya michezo," alisema Balakov.

"Kama vilitokea vitendo kama hivyo vya ubaguzi wa rangi, huenda nilikuwa katika umakini wa kufuatilia timu yangu ilikuwa inapambana vipi uwanjani, lakini kusikia jambo kama hilo, sikulisikia kabisa.

"Tulikuwa wengi uwanjani, huenda kila mmoja amesikia alichosikia, ila ninarudia tena kwangu sikusikia chochote kuhusu ubaguzi wa rangi ambao unadaiwa kufanywa dhidi ya wachezaji wa timu pinzani."

Mabao ya England katika mchezo huo yalipachikwa wavuni na Raheem Sterling, Ross Barkley (mawili kila mmoja), huku Marcus Rashford na Harry Kane wakifunga bao moja kila mmoja.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE GEA AUMIA, SHAKANI KUIKOSA LIVERPOOL J'PILI

●●●Kocha wa Hispania aeleza awalia alitibiwa wakati wa mapumziko, lakini akaamua...

**Stockholm, Sweden**

KIPA David de Gea yupo shakani kutoitumikia Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Liverpool Jumapili baada ya kulazimika kuelekea benchi wakati akiichezea Hispania juzi kufuatia kuumia.

De Gea alianza katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Sweden baada ya kusugua benchi dhidi ya Norway wiki iliyopita.

Kipa huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 28, alionekana kujitonesha misuli yake ya paja wakati wa mechi hiyo dhidi ya Sweden ambapo alilazimika kutoka nje na nafasi yake kuchukuliwa na mlinda mlango wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga baada ya saa moja ya mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Friends Arena, Stockholm wakati huo wakiwa nyuma kwa bao 1-0.

Kocha wa Hispania, Robert Moreno amethibitisha kuumia kwa De Gea katika mechi hiyo, taarifa hizo zikiwa ni pigo kubwa kwa Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer kuelekea mechi ya Jumapili kwenye Uwanja wa Old Trafford.

"De Gea alitibiwa wakati wa mapumziko na akaamua kuendelea," Moreno alielezea baada ya kipa huyo wa United kuonekana kutokuwa sawa kufuatia kazi kubwa aliyoifanya kipindi cha kwanza.

Katika mechi hiyo, mtokea benchi Rodrigo Moreno alisawazisha bao hilo dakika za majeruhi, hivyo kufanya matokeo kuwa 1-1 na Hispania kufuzu rasmi Euro 2020.

Kuumia kwa De Gea kulikuwa katika hali ya kutofanyiwa madhambi na mara moja akashika nyuma ya mguu wake baada ya kuicheza pasi ya nyuma kutoka kwa mchezaji mwenzake.

Alikaa chini maguu sita ndani ya boksi kabla ya kuanza safari ya kutoka nje akiwa sambamba na daktari wa timu.

United ipo katika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na haijashinda katika mechi zake tatu za ligi hiyo zilizopita.

Jumapili watakaribisha Liverpool ambayo itakuwa ikilenga kushinda mechi ya 18 mfululizo kwenye Ligi Kuu, idadi ambayo itaifanya kuifikia rekodi inayoshikiliwa na Manchester City.

De Gea alikosoa kiwango cha timu yao msimu huu baada ya mechi iliyopita kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Newcastle - akisema: "Msimu mzima haukubali kwetu.

"Tuna majeruhi, lakini haiwezi kuwa kisingizio. Sisi ni Manchester United. Tunahitaji kujifua sana kuendelea kupigana na kuanza kushinda mechi."

Kama De Gea hataweza kuanza mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Old Trafford mwishoni mwa wiki, kipa Muargentina Sergio Romero ambaye amekuwa akitumika kwenye mechi za Europa League na Kombe la Ligi ['Carabao Cup'] msimu huu, anaweza kuziba pengo lake.

## KWA UFUPI

**MADRID HAIPOI KWA KANTE**

Real Madrid inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 86 pamoja na kiungo Mcolombia James Rodriguez, 28, ili kupata baraka kutoka Chelsea za kumsajili kiungo wao Mfaransa N'Golo Kante. ***(El Desmarque - in Spanish)***

**ARSENAL ILIVYOMKOSA GRIEZMANN**

KITENDO cha Arsenal kushindwa kufuzu kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya mwishoni mwa msimu wa 2016-17, kuliwagharimu kukosa nafasi ya kumsajili mshambuliaji Mfaransa Antoine Griezmann kutoka Atletico Madrid. Straika huyo mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na Barcelona majira haya ya joto. ***(Star)***

**MANDZUKIC AONYWA UNITED**

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Croatia, Mario Mandzukic, 33, anatakiwa na Manchester United, lakini amekuwa akionywa kwamba atalazimika kushuka mshahara anaohitaji ili kukamilika kwa dili hilo. ***(ESPN)***

**JUVE YAMKANUSHIA RONALDO**

MKURUGENZI wa Michezo wa Juventus, Fabio Paratici amekanusha tetesi kwamba mshambuliaji wa kimataifa wa Ureno, Cristiano Ronaldo, 34, anaweza kustaafu na kueleza kwamba mchezaji huyo ni mwenye furaha katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Star)***

**RAKITIC AIMULIKA UTD, JUVE**

KIUNGO wa Barcelona na Croatia, Ivan Rakitic, 31, anazingatia kujiunga na Juventus ama Manchester United. ***(Marca)***

**EMERY HATAENDA SOKONI**

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery hatazami uwezekano wa kuongeza nguvu kikosi chake katika dirisha la usajili la Januari. ***(The Athletic)***

**COUTINHO NAFASI IPO LIVER**

KIUNGO wa Brazil, Philippe Coutinho, 27, bado anaweza kurudi Liverpool - kama Bayern Munich itaamua kutomsajili jumla majira ya joto yajayo. Kwa sasa anawachezea kwa mkopo mabingwa hao wa Ujerumani akitokea Barcelona. ***(AS)***

**SPURS YAJIONGEZA KWA MOURINHO**

Tottenham wameongeza harakati zao za kuipata huduma ya Jose Mourinho, huku kukiwa na sintofahamu kuhusu nafasi ya Manchester United kumuwinda Mauricio Pochettino. ***(Express)***

**INCE AISHUKIA BULGARIA**

NAHODHA wa kwanza mweusi katika kikosi cha timu ya Taifa ya England, Paul Ince, amesema angewaongoza wachezaji wenzake kutoka nje ya uwanja kama angekuwa anacheza mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 ya Bulgaria vs England Jumatatu, huku kukiwa na vitendo vya kibaguzi kutoka kwa mashabiki. ***(Times)***

**GIROUD KUSEPA CHELSEA**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud, 33, anajiandaa kuondoka klabuni hapo Januari mwakani kama hatapata nafasi ya kucheza zaidi. Inter Milan na Vancouver Whitecaps ya Canada ni miongoni mwa klabu zinazomhitaji. ***(Sun)***

**BALE AMPA SOMO MODRIC**

KIUNGO wa Croatia, Luka Modric ameombwa na mchezaji mwenza wa Real Madrid, Gareth Bale, 30, kubaki klabuni hapo baada ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Wales kuwapo katika nafasi kubwa ya kuondoka majira ya joto yaliyopita. ***(Independent)***

**PALACE YAMFUATILIA BARBOSA**

Crystal Palace inavutiwa na mshambuliaji wa Inter Milan, Gabriel Barbosa, 23, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu yao nyumbani kwao, Flamengo ya Brazil. ***(PassionInter, via TeamTalk)***

## HABARI MICHEZO

# KIWALE, MSAUZI KUZICHAPA BONDENI

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa hapa nchini, Sunday Kiwale, anatarajia kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kupigana na Daluxolo Mangxotya katika pambano litakalofanyika Novemba 20, mwaka huu jijini Johannesburg.

Pambano hilo litakuwa la uzito wa Super fly weight (kilo 52) na litakuwa la kuwania mkanda wa WBA.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kocha wa bondia huyo, Rajab Mhamila, alisema Kiwale ataondoka nchini Novemba 16 na tayari ameshaanza maandalizi kwa lengo la kufanya vema kwenye pambano hilo.

Mhamila alisema kuwa anaamini bondia wake atakwenda kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika pambano hilo.

Naye Kiwale aliliambia gazeti hili kuwa amejiandaa vema na anaahidi kurejea nyumbani na mkanda wa pambano hilo.

"Nimejiandaa vizuri kwa ajili ya kwenda kushindana huko Afrika Kusini, ninaahidi Watanzania nitarudi na ushindi," alisema Kiwale.

# WAMBURA APEWA MAJUKUMU MAPYA, MIRAMBO RASMI TFF

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Boniface Wambura, sasa atakuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Masoko wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) huku Oscar Mirambo akitangazwa rasmi kuwa mkurugenzi wa ufundi wa shirikisho hilo.

Kabla ya kwenda Bodi ya Ligi, Wambura, Mwenyekiti wa zamani wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (TASWA), aliwahi kuwa Ofisa Habari wa TFF.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema kuwa Wambura amepewa majukumu hayo mapya baada ya kumaliza mkataba wake wa kuitumikia Bodi ya Ligi.

Kidao alisema kuwa katika idara hiyo, Wambura atasaidiana na Clifford Ndimbo katika upande wa habari wakati Aaron Nyanda, atafanya naye kazi za kutafuta masoko.

"Shirikisho linaamini kwa uzoefu aliokuwa nao Wambura, atafanya vema kwenye idara hiyo, tunataka kuwa na idara yenye weledi na kufanya vema zaidi hapa Afrika, ikiwezekana tutachukua wanahabari wengine wenye uzoefu zaidi kuungana na Wambura ili kufikia malengo ya shirikisho," alisema Kidao.

Aliongeza kuwa kuanzia leo, TFF itatoa tangazo rasmi katika vyombo mbalimbali vya habari kutoa fursa kwa Watanzania wengine kuomba kuajiriwa katika nafasi hiyo.

Wakati Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi akianza kusakwa, bodi hiyo imeanza mchakato mwingine wa kuziba nafasi sita za wajumbe wao, ambao zitapatikana katika uchaguzi mdogo utakaofanyika Desemba 7, mwaka huu hapa jijini.

Bodi ya Ligi sasa inaongozwa na Mwenyekiti wa Coastal Union, Stephen Mnguto, ambaye kwa mujibu wa katiba anatambulika pia kama Makamu wa Pili wa Rais wa TFF.

Aidha, Mirambo aliyekuwa Kocha Mkuu wa Timu ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), ambaye alikuwa akikaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Ufundi wa TFF akirithi mikoba iliyoachwa na Ammy Ninje, ambaye aliamua kuvunja mkataba kwa sababu ya kubanwa na majukumu ya kifamilia, sasa ametangazwa rasmi kupewa majukumu hayo. Akizungumzia uamuzi huo, Kidao alisema uteuzi wa Mirambo umepitishwa kutokana na kuridhishwa na sifa na uzoefu aliokuwa nao, mchezaji huyo wa zamani wa Serengeti Boys.

Kidao alisema katika kumwongezea uwezo wa kufanya kazi hiyo, Mirambo anatarajiwa kwenda mafunzo maalumu yatakayotolewa kwa wakurugenzi wa ufundi wapya wa nchi mbalimbali kuanzia Novemba 25 hadi 30, mwaka huuu jijini Kigali, Rwanda.

"Baada ya hapo, Mirambo atakuwa chini ya mkufunzi mwingine kutoka Fifa, ambaye atakuwa hapa nchini kumpa maelekezo na malengo ya kusimamiwa ni kutaka wakufunzi hao kufanya kazi zao kwa weledi," alisema Kidao.

Aliongeza kuwa Mirambo alifanya kazi yake ya ukocha kwa muda mrefu akiwa chini ya wakurugenzi waliopita ambao ni Sunday Kayuni, Salum Madadi na Ninje.



Washindi wa Simu Janja kutoka Dar es Salaam baada ya kukabidhiwa simu zao aina ya Samsung A10s. Kushoto ni Meneja wa Huduma za Kidijitali, Ikunda Ngowi akifuatiwa na Balozi wa SportPesa, Edward Kumwembe na wa kwanza kulia ni mchezaji wa timu ya Yanga, Papy Tshishimbi. Promosheni ya Faidika na Jero bado inaendelea na mwisho itatolewa zawadi ya gari aina ya Renault Kwid. **MPIGAPICHA WETU**

# ZFF yamfungia shabiki Mafunzo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limempiga faini ya Sh. 100,000 na kutohudhuria uwanjani katika mechi tano, shabiki wa Mafunzo FC, Kapama Kauga, kutokana na kitendo chake cha kumfanyia fujo mwamuzi aliyechezesha mechi kati ya timu yake na JKU.

Shabiki huyo wa Mafunzo, alimzonga mwamuzi, Abdi Kombo "DECO" wakati wakiwa wanaelekea katika vyumba vya mapumziko, kitendo ambacho ni makosa.

**Kwa mujibu wa barua iliyotolewa na Katibu wa Kamati ya Mashinda no, Hussein Ahmada Vuai, imeeleza kuwa adhabu ya shabiki huyo imetolewa kwa kufuata kanuni ya mashindano kifungu cha 31 na 19.**

Vuai alisema kuwa Kauga anatakiwa kulipa faini hiyo ndani ya siku saba tangu alipoandikiwa barua ya adhabu yake hapo Oktoba 16, mwaka huu.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa kamati haitamvumilia shabiki wa timu yoyote atakayefanya fujo iwe kwa waamuzi au kwa timu pinzani na kuwataka mashabiki wa klabu zote kuwa wastahamilivu.

Katika mchezo huo uliochezwa Oktoba 13, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Mao A, Mafunzo waliibuka na ushindi wa bao 1-0.

# Tigo, SportPesa kugawa gari mwezi huu

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya SportPesa kwa kushirikiana na kampuni ya mtandao wa simu za mikononi ya Tigo, mwishoni mwa mwezi huu zitamtangaza mshindi wa zawadi ya gari mpya aina ya Renault Kwid wakati huu, simu aina ya Samsung A10s zikiendelea kutolewa kila siku kupitia promosheni ijulikanayo kama Faidika na Jero.

Mpaka sasa kupitia promosheni hiyo, washindi 26 wamezawadiwa simu aina ya Samsung A10s.

Akizungumza baada ya droo ya wiki ya nne, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa SportPesa, Sabrina Msuya alisema: "Kupitia droo za kila wiki hii tumeweza kupata washindi kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Dodoma, Morogoro pamoja na Mbeya.

"Promosheni bado inaendelea na wiki ijayo tunatarajia kupata washindi wengine saba na washindi wa wiki hii watakabidhiwa simu zao siku hiyo hiyo."

Sabrina aliwataja washindi wa wiki hii kuwa ni Gervas Mgaya kutoka Morogoro, Meshack Sanga (Mbeya), Brighton Mbundo (Pwani), Hatibu Shabani, Enea Mtosa, Khalfan Juma na Ramadhani Tindwa (wote kutoka Dar es Salaam.

Alisema watumiaji wapya na endelevu wa mtandao wa Tigo wanapaswa kuweka pesa kwenye akaunti ya SportPesa kupitia huduma ya Tigopesa ili kuweza kushiriki na kujishindia zawadi kabambe kwa ajili yao.

Michezo
Alhamisi Oktoba 17, 2019
Nipashe



De Gea aumia, shakani kuikosa Liverpool J'pili

HABARI UK 30

TUMEFUZU...



Mshambuliaji wa Hispania, Rodrigo Moreno (Jezi namba 19) akishangilia sambamba na mchezaji mwenza, Rodri baada ya kuisawazishia timu yake dhidi ya Sweden kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Friends Arena mjini Stockholm na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, matokeo yaliyoiwezesha Hispania kufuzu michuano hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# FIFA YASHAURI TFF SASA ISUKWE UPYA

●●●Wajumbe Kamati ya Utendaji kufyekwa kutoka 22 hadi 13, huku mkutano mkuu ukihudhuriwa na wajumbe...

**Na Somoe Ng'itu**

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linatarajia kupitisha panga katika safu yake ya uongozi baada ya kutoa mapendekezo ya marekebisho ya katiba yake ambayo endapo yatapitishwa itashuhudiwa idadi ya Wajumbe wa Kamati ya Utendaji na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wakipungua.

TFF inatarajia kufanya mkutano mkuu wa mwaka Desemba 21, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema uamuzi wa kupunguza idadi ya wajumbe hao watakaoingia katika Kamati ya Utendaji, inalenga kuongeza ufanisi wa maendeleo ya soka na shirikisho.

Kidao alisema kwa mujibu wa mapendekezo hayo ambayo yametolewa na Shirikisho la Soka duniani (Fifa), kwa wanachama wake, wajumbe wa Kamati ya Utendaji watakuwa 13, badala ya 22 walioko hivi sasa.

Alisema kwa mfumo huo, TFF iliyokuwa na Kanda 13, sasa mikoa itaunganishwa na kubakia na Kanda 6 tu.

"Katiba kuhakikisha wajumbe wanafanya kazi kwa ufanisi zaidi, sasa vikao vya Kamati ya Utendaji, vitaongezeka, badala ya kukutana kila baada ya miezi mitatu, sasa watakutana kila baada ya miezi miwili, tunaamini wadau watakubaliana na mapendekezo haya kwa maslahi ya nchi," Kidao alisema.

Hata hivyo, Kidao alisema kuwa mabadiliko hayo ya katiba, hayatagusa vyama shiriki, kwa kueleza kwamba imewapendelea zaidi wanawake, ambao awali walikuwa wanawakilishwa na wajumbe watatu, sasa hivi wataingia wanawake wanne katika mkutano mkuu.

"Hadi hivi tunavyoongea kwa Afrika, ni Tanzania na Botswana tu, ndio tumebaki, ndio katiba zake zimebaki haziendani na katiba ya Fifa, kwa mfano sasa hivi Mkutano Mkuu wa Nigeria unahudhuriwa na wajumbe 39 tu, wakati hapa kwetu tuna wajumbe zaidi ya 130," alisema Kidao.

Aliongeza kuwa pia mfumo wa kamati ndogondogo za shirikisho hilo utaendelea kuwapo kwa ajili ya kuendelea kufanya shughuli za maendeleo kulingana na mahitaji husika.

"Kwa mfano katiba iliyopitishwa Arusha (Februari mwaka huu), ilipitia taratibu zote, hii pia tunaamini wajumbe watafuata, nakumbuka hata hoja ya katibu mkuu kuajiriwa, ilipata changamoto, lakini baadaye ilipita," alimaliza Kidao.

Alisema pia agenda za mkutano mkuu unaokuja, zitakuwa ni za kawaida na tayari, wajumbe wameshaandikiwa wito wa kushiriki katika mkutano huo.

## Sababu Warundi kuishika Simba

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Simba jana ilimaliza ziara yake ya mechi za kirafiki mkoani Kigoma kwa kutoka sare ya bila kufungana na Aigle Noir ya Burundi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini humo.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems ameendelea kueleza ubovu wa uwanja ni moja ya sababu ya timu yake kushindwa kucheza vizuri katika mechi hiyo na ile ya awali dhidi ya Mashujaa waliyoshinda kwa bao 1-0.

Simba ndiyo iliyofanya mashambulizi mengi langoni mwa wapinzani wao, lakini inaonekana kukosekana kwa mastraika wao tegemeo, Meddie Kagere na Miraji Athumani kuliwaangusha.

Katika mechi ya kwanza kwenye uwanja huo, Simba ilishinda bao 1-0 dhidi ya Mashujaa ya Kigoma lililowekwa nyavuni na Ibrahim Ajibu.

Kipindi cha kwanza Simba ilifanya shambulio hatari moja tu, wakati straika wake, Mbazil Wilker Henrique da Silva alipopiga kichwa akiwa karibu na goli kutokana na pasi ndefu ya Ajibu, lakini iliishia kwenye mikono ya kipa wa Aigle Noir, Ndizeye Aime ambaye alikuwa kikwazo kwa wachezaji wa Simba.

Kipindi cha pili, Simba ilifanya mabadiliko kwa kumtoa Francis Kahata na kumwingiza Deo Kanda, pia Rashid Juma aliingia kuongeza nguvu na mchezaji huyo alikosa mabao matatu ya wazi kama angetulia. Faulo ya Ajibu nusura izae bao dakika ya 57, lakini ikazaa kona tasa.

Rashid alikosa mabao dakika ya 71, 72 na 87, alipokuwa akibaki yeye na kipa, lakini ukomavu ulimwangusha na kupiga mashuti dhaifu, yaliyokuwa mboga kwa Ndizeye.

Simba imeendeleza rekodi yake ya kutopoteza mechi yoyote ile tangu ilipofungwa kwenye Uwanja wa Uhuru dhidi ya Kagera Sugar kwa bao la kujifunga la Mohamed Hussein 'Tshabalala' Mei 9, mwaka huu kwenye Ligi Kuu msimu uliopita.

Tangu wakati huo Simba haijapoteza mechi yoyote, badala yake imekuwa ikishinda au kutoka sare, huku ikishinda mechi zote nne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >